
# Mlima Wa Baraka



**Uhamishoni Ughaibuni Mtandaoni Majumbani**

# WALIOFANIKISHA KAZI HII

Wengi wamehusika kusaidia hii kazi, kwa Maombezi, Kutafsiri, Kuhariri, Kutia moyo, Kusaidia mambo ya kiufundi n.k “Watu 1000 Wote wataamini, siku moja wataamini, kwa ule ujumbe wa kimya wa machapisho”.


Musa Budodi-One Soul Audience
Grace Momadi Masaka-Jersey, Marekani
Daniel Nyangaresi Masaka-Kisii, Kenya
Judi na John Mugane-Boston, Marekani
Mbusi Mpagalushu
Sandra Barron-North Carolina, Marekani
Daudi Masaka-Carolina, Marekani

# Roho ya Unabii

Tafsiri kutoka Thoughts From Mounts of Blessings

E. G. White

## YALIYOMO

**DIBAJI**..........................................................................................................................ii
**SURA YA 1**
**JUU MLIMANI**.................................................................................................................. 2
**SURA YA 2**
**MIBARAKA ALIYOITOA BWANA**.....................................................................................5
**SURA YA 3**
**SHERIA INAVYOYAHUSU MAMBO YA KIROHO**.........................................................30
**SURA YA 4**
**SABABU YA KWELI KATIKA HUDUMA**.........................................................................51
**SURA YA 5**
**SALA YA BWANA**............................................................................................................ 66
**SURA YA 6**
**SIYO KUHUKUMU BALI KUFANYA**................................................................................ 79

# DIBAJI

Yale mahubiri mlimani ni baraka za Mungu kwa ulimwengu—sauti kutoka kwenye kiti cha enzi cha Mungu. Yalitolewa kwa wanadamu ili kuwa kanuni ya kazi kwao, na nuru ya mbinguni, tumaini na kitulizo chao wanapokata tamaa, furaha na faraja yao katika mabadiliko yote na hali yao ya maisha. Hapa Mkuu wa wahubiri wote, Mwalimu Mkuu, anatamka Maneno yale aliyopewa na Baba kusema.**[MB vii.1]**

Mibaraka hii ni salamu ya Kristo, si kwa wale tu wamwaminio, bali kwa wanadamu wote. Aelekea kana kwamba alikuwa amesahau kidogo kuwa bado Yuko duniani, si mbinguni; Naye atumia salamu ijulikanayo na wale wa ulimwengu wa nuru. Mibaraka humiminika kutoka midomoni Mwake kama mkondo ububujikao wa maisha bora ambao ulikuwa umezuiwa kwa muda mrefu.**[MB vii.2]**

Kristo hatuachi mashakani tusijue tabia ambazo siku zote atazikubali na kuzibariki. Kutoka kwa wale wenye kutamani na kuzipenda anasa za dunia, awageukia wale wanaowakataa, akiwataja hao wote kuwa wa heri waipokeao nuru na uzima Wake. Kwa maskini wa roho, wenye upole, wanyenyekevu, wenye huzuni na huzuni, wenye kudharauliwa na wenye kuteswa, Yeye huinyosha mikono Yake ambayo ni kimbilio, akisema, "Njoni Kwangu…Nami nitawapumzisha."**[MB vii.3]**

Kristo aweza kuiangalia hali mbaya ya huzuni ya walimwengu, bila moyo Wake kuona hata chembe ya majuto kwa kumwumba mwanadamu. Ndani ya moyo wa mwanadamu,Yeye huona kitu kingine zaidi ya dhambi, na zaidi ya hali mbaya ya taabu na huzuni. Kwa hekima Yake isiyo na mwisho, na upendo Wake usio na kikomo, Yeye huona vile mwanadamu awezavyo kuwa, kimo ambacho aweza kukifikia. Yeye Ajua kwamba, ijapokuwa wanadamu wametumia vibaya rehema zao na kuharibu heshima waliyopewa na Mungu, hata hivyo, Muumbaji hana budi kutukuzwa kwa ukombozi wao.**[MB vii.4]**

Kwa nyakati zote Maneno yale aliyoyasema Kristo katika mlima wa baraka yatakuwa na nguvu yake. Kila sentensi ni kito cha thamani kitokacho kwenye nyumba ya hazina ya ile Kweli. Kanuni hizi zilizotangazwa katika mahubiri haya zahusu zamani zote, na ni kwa watu wa kila aina.

Kwa nguvu za Mungu, Kristo ameonesha imani na matumaini Yake alipokuwa akionesha kundi moja baada ya jingine la wale ambao wa heri kwa sababu ya kujenga tabia za haki. Kuishi maisha ya Mtoaji-wa-Uzima kwa njia ya kumwamini Yeye, kila mmoja aweza kukifikia upeo ulioweka katika Maneno Yake.**[MB viii.1]**

WACHAPAJI.

Kwa Wafuasi Wake ambao Bwana angali akiwaita kuchagua ufalme wa kiroho badala ya ufalme wa dunia hii. Kitabu hiki kidogo kimewekwa wakfu ikitumainiwa kwamba kurasa zake zitawafafanulia wazi zaidi utukufu wa mambo yale yasiyoonekana.**[MB viii.2]**

## SURA YA 1

## JUU MLIMANI

Zaidi ya karne kumi na nne kabla ya kuzaliwa Kwake Yesu katika mji wa Bethlehemu, Waisraeli walikusanyika katika bonde zuri la Shekemu; nao wakasikia sauti za makuhani wakisimama milimani pande mbili na kutangaza mibaraka na laana—"Baraka ni hapo mtakapoyasikiza maagizo ya BWANA, Mungu wenu…..na laana ni hapo msipoyasikia maagizo ya BWANA, Mungu wenu." Kumbukumbu la Torati 11:27,28. Kwa hiyo mlima ule ambao Maneno ya mibaraka yalitolewa, ukaja kujulikana kama *Mlima wa Bara*ka. Lakini haikuwa juu ya Gerizimu ambapo Maneno hayo yalisemwa ambayo yamekuwa kama mbaraka kwa ulimwengu wenye dhambi na huzuni. Waisraeli walishindwa kukifikia kipimo cha ukamilifu walichowekewa mbele yao. Akatakiwa mtu mwingine asiye Yoshua kuwaongoza watu Wake katika raha ya imani iliyo ya kweli. Gerizimu hautajwi tena kuwa Mlima wa Mibaraka, ila ni mlima ule usiojulikana ulio kando ya Ziwa la Genesareti, Yesu alipowatolea wanafunzi Wake na makutano Maneno ya mibaraka.**[MB 1.1]**

Hebu kimawazo turudi nyuma kwenye tukio lile, na tuketipo pamoja na wanafunzi wa Yesu kule mlimani, hebu tuingie katika mawazo na hisia zao zilizoijaza mioyo yao. Tukifahamu maana ya Maneno ya Yesu mioyoni mwa wale walioyasikia, twaweza kutambua ndani yake udhahiri na uzuri mpya, tena twaweza kujipatia mafundisho Yake yenye kina kirefu.**[MB 1.2]**

Mwokozi alipoanza huduma Yake, dhana iliyoshikiliwa na wengi kumhusu Masihi na kazi Yake ilikuwa haifai kabisa kuwawezesha watu hawa kumpokea. Moyo wa kumwabudu Mungu kweli-kweli ulikuwa umepotezwa kwa mapokeo na taratibu za ibada, na unabii ulitafsiriwa kwa kanuni zilizosukumwa na mioyo yenye kiburi, ipendayo dunia. Wayahudi walimtazamia Yule Ajaye, si kama Mwokozi atakayewatoa katika dhambi, bali kama mtawala mkuu atakayeyaweka mataifa yote chini ya mamlaka kuu ya Simba aliye wa kabila la Yuda. Ikawa kazi bure kwa Yohana Mbatizaji, aliyekuwa na uwezo wa manabii wa kale uchomao mioyo, kuwaita ili wapate kutubu. Ikawa kazi bure kwake, kando ya mto Yordani, kuwaelekeza kwa Yesu kama Mwana-Kondoo wa Mungu, aichukuaye dhambi ya ulimwengu. Mungu alikuwa akijaribu kuwaelekeza mawazo yao kwenye unabii ule wa Isaya wa Mwokozi anayeteseka, lakini hawakutaka kusikia.**[MB 1.3]**

Waalimu na viongozi katika Israeli endapo wangejitia chini ya neema Yake

ibadilishayo maisha, Yesu angekuwa amewafanya kuwa wajumbe Wake kati ya watu. Ilikuwa ni katika Yudea ambako kuja kwa ufalme wa Mungu kulitangazwa kwanza, na wito wa kutubu ulikuwa umetolewa. Katika kitendo kile cha

kuwafukuza wale waliolitia unajisi hekalu la Mungu pale Yerusalemu, Yesu alikuwa amejitangaza Mwenyewe kuwa Ndiye Masihi—Yule ambaye angeutakasa moyo kutokana na unajisi wa dhambi, na kuwafanya watu Wake kuwa hekalu takatifu la Bwana. Lakini viongozi wale wa Kiyahudi hawakukubali kujishusha mioyo na kumpokea Mwalimu huyu masikini na mnyenyekevu aliyetoka Nazareti. Alipokwenda mara ya pili kule Yerusalemu alishtakiwa mbele ya Baraza Kuu la Kiyahudi, na kwa ajili tu ya kuwaogopa watu wenye hadhi ya juu, hawa walizuiwa wasijaribu kumwua. Ndipo ikawa baada ya kuondoka Yudea, akaanza kazi ake ya huduma, kule Galilaya.**[MB 2.1]**

Kazi Yake kule iliendelea kwa miezi kadhaa, kabla ya kutolewa Mahubiri yale ya Mlimani. Ujumbe aliokuwa ameutangaza nchini kote, akisema, “Ufalme wa mbinguni umekaribia” (Mathayo 4:17), ulikuwa umeivuta/umeivuta mioyo ya watu wa kila aina, na bado ukawa umeongeza sana moto wa hamu ya matumaini yao. Sifa ya yule Mwalimu mpya ilikuwa imeenea kupita mipaka ya nchi ya Palestina, na, licha ya msimamo wa wakuu wa nchi, hisia ilienea kote kwamba Huyu huenda akawa Ndiye Mkombozi waliyemtarajia. Umati mkubwa wa watu ulimsongasonga Yesu alipotembea, na hamu kubwa ya watu wengi ikazidi kuongezeka..**[MB 2.2]**

Wakati ukawa umewadia kwa wale wanafunzi waliokuwa wameshirikiana kwa karibu sana na Kristo kujiunga moja kwa moja katika kazi Yake, ili umati huo mkubwa wa watu usiachwe bila ya kuhudumiwa, kama kondoo wasio na mchungaji. Baadhi ya wanafunzi hao walikuwa wamejiunga Naye tangu mwanzo wa huduma Yake, na karibu wale wote kumi na wawili walikuwa wameshirikiana pamoja kama watu wa familia ya Yesu. Hata hivyo, wao pia, wakiwa wamepotoshwa na mafundisho ya waalimu wa Kiyahudi, walikuwa na mawazo yale yale maarufu, yaliyopendwa na wengi ya kutarajia kuwa na ufalme wa kidunia. Hawakuweza kufahamu mienendo ya Yesu. Tayari walikuwa wamechanganyikiwa na kusumbuka moyoni kwa kuwa alikuwa hajafanya jitihada yoyote kuiimarisha kazi Yake kwa kujipatia msaada wa makuhani na waalimu wakuu wa Kiyahudi, na ya kwamba hakufanya lolote kuanzisha mamlaka Yake kama mfalme wa kidunia. Lakini kazi kubwa ilipasa ifanywe mioyoni mwa wanafunzi hawa kabla hawajaweza kuwa tayari kuifanya kazi yenye amana takatifu, watakayokabidhiwa ambayo ingekuwa yao hapo Yesu atakapopaa mbinguni. Hata hivyo, walikuwa wamevutwa na upendo wa Kristo, na ingawa mioyo yao ilikuwa mizito kuamini, Yesu aliona ndani yao kuwa ni watu anaoweza kuwafundisha na kuwatayarisha kuifanya kazi Yake ile kubwa. Na sasa kwa kuwa walikuwa wamekaa pamoja Naye muda mrefu wa kutosha kuweza kuiimarisha imani yao, kwa kiwango fulani, kuhusu aina ya utume Wake wa

Kiungu, na watu pia walikuwa wamepokea ushahidi wa uwezo Wake ambao hawakuweza kuutilia mashaka, njia ikawa imetayarishwa kwa kuzieleza waziwazi kanuni za ufalme Wake ambazo zingeweza kuwasaidia kuuelewa ulivyo hasa..**[MB 3.1]**

Akiwa peke Yake huko mlimani karibu na Bahari ya Galilaya, Yesu alikuwa amekesha usiku wote ili akiwaombea wateule Wake hawa. Kulipopambazuka akawaita Kwake, na, kwa Maneno ya sala na mafundisho, akaweka mikono Yake juu ya vichwa vyao na kuwabariki, akiwatenga kwa ajili ya kazi ya injili. Ndipo akaenda pamoja nao pwani, mahali ambapo umati mkubwa ulikuwa tayari umeanza kukusanyika mapema asubuhi.**[MB 4.1]**

Mbali na kundi la kawaida lililotoka katika miji ya Galilaya, palikuwapo na idadi kubwa ya watu kutoka Yudea, na kutoka Yerusalemu kwenyewe; kutoka Perea, na kutoka Dekapoli, ambao watu wake walikuwa nusu makafiri; kutoka Idumea, mbali kusini ya Yudea, na kutoka Tiro na Sidoni, miji ile ya Kifoinike katika mwambao wa Mediterania. "Waliposikia habari za mambo yote aliyokuwa akiyatenda" wakaja ili "kumsikiliza na kuponywa magonjwa yao; na wale waliosumbuliwa na pepo wachafu; waliponywa... kwa sababu uweza ulikuwa ukimtoka ukiwaponya wote." Marko 3:8; Luka 6:17-19.**[MB 4.2]**

Ndipo, kwa sababu pwani ile ilikuwa nyembamba, yaani haikuwa na nafasi ya kusimama kuweza kusikia sauti Yake kwa wale wote waliotaka kumsikia, Yesu akatangulia mbele yao na kwenda kando ya mlima. Na walipofika mahali palipofaa kwa mkutano ule mkubwa,Yeye aliketi juu ya majani, na wanafunzi Wake na ule mkutano wakafuata mfano Wake..**[MB 4.3]**
Wakiwa na hisia kwamba jambo fulani lisilo la kawaida lingeweza kutazamiwa kutokea, wanafunzi wale wakasongamana kumzunguka Mwalimu wao. Kutokana na matukio ya asubuhi ile walikuwa wamejenga imani kwamba tangazo fulani lilikuwa karibu kutolewa kuhusu ufalme ambao, walitarajia kwa matumaini yao ya kijinga, naam, Yeye atausimamisha hivi karibuni. Hisia ya kutazamia kutokea kitu fulani ilienea pia kwa mkutano ule, na nyuso zenye hamu zilionyesha ushahidi wa kuwa na shauku kubwa mioyoni mwao.**[MB 4.4]**

Walipoketi kando ya kilima kile cha kijani, wakingojea Maneno ya Mwalimu Mtakatifu, mioyo yao ikajazwa na mawazo ya utukufu wa baadaye. Walikuwapo Waandishi na Mafarisayo walioitazamia siku ile watakapokuwa na mamlaka juu ya Warumi waliowachukia, na kupata utajiri na fahari ya kuwa na dola kuu ya ulimwengu. Wakulima maskini na wavuvi walitumaini kuhakikishiwa kuwa vibanda vyao vile vibaya, chakula cha shida yaani kidogo, maisha ya kufanya kazi kwa taabu, hofu ya kupungukiwa, mambo hayo yangebadilishwa kwa kupewa majumba makubwa ya kifahari yenye chakula tele na siku za raha mustarehe. Mahali pa vazi moja baya ambalo walijifunika mchana na usiku lilikuwa ndilo blanketi lao, walitumaini kwamba Kristo angeweza kuwapa mavazi ya kitajiri na ya gharama ya wale waliowateka na kuwatawala.**[MB 5.1]**

Mioyo yao wote ilifurahi sana kuwa na tumaini lenye majivuno kwamba Israeli ingeheshimiwa baada ya muda mfupi mbele ya mataifa kama wateule wa Bwana, na Yerusalemu kukuzwa kuwa mji mkuu wa ufalme wa ulimwengu mzima..**[MB**

5.2]

# SURA YA 2 MIBARAKA ALIYOITOA BWANA

**"Akafumbua kinywa Chake, akawafundisha, akisema, Heri walio maskini wa roho; maana ufalme wa mbinguni ni wao." Mathayo 5:2,3.**

Kama jambo fulani geni na jipya, Maneno haya yalianguka katika masikio ya umati ule mkubwa uliopigwa na mshangao. Mafundisho kama hayo yalikuwa kinyume kabisa na yote waliyopata kuyasikia kwa kuhani au mwalimu awaye yote. Ndani ya maneno hayo hawakuona kitu chochote cha kujivunia ama cha kuichochea nia yao ya kutumaini kujipatia makuu. Lakini kumzunguka Mwalimu huyu mpya kulikuwa na uwezo uliovuta usikivu wao hata wakatekewa. Utamu wa upendo wa Mungu ulifurika kutoka Kwake kama harufu nzuri ya maua. Maneno Yake yalianguka "kama mvua juu ya majani yaliyokatwa: kama manyunyu yainyweshayo nchi." Zaburi 72:6. Wote waliona moyoni mwao kwamba pale alikuwapo Mmoja asomaye siri za moyoni, lakini Yule ambaye huwakaribia kwa moyo wa huruma uliojaa upendo. Wakamfunulia mioyo yao, na wakati walipomsikiliza, Roho Mtakatifu alijaribu kuwafunulia maana ya fundisho lile ambalo wanadamu wote katika vizazi vyote wanapaswa kujifunza sana.**[MB 6.1]**

Katika siku za Kristo viongozi wa dini waliona kama walikuwa matajiri katika mambo ya kiroho. Sala ya yule Farisayo aliposema, "Ee Mungu, nakushukuru kwa kuwa mimi si kama watu wengine," (Luka 18:11), ilidhihirisha jinsi watu wa tabaka lake walivyojiona, na, kwa sehemu kubwa, taifa lile zima. Lakini miongoni mwa umati ule mkubwa uliomzunguka Yesu walikuwamo wengine waliojiona kuwa ni maskini wa roho. Katika kitendo kile cha kuwapata samaki wengi kwa njia ya mwujiza uweza wa Mungu ulidhihirishwa, Petro alianguka chini ya miguu ya Mwokozi, akisema kwa mshangao, "Ondoka Kwangu, kwa kuwa mimi ni mtu mwenye dhambi, Bwana," (Luka 5:8); hivyo miongoni mwa watu waliomkusanyikia mlimani, walikuwamo wengine ambao, mbele ya utakatifu Wake Yesu, walijiona kuwa ni "wanyonge na wenye mashaka, na maskini, na vipofu, na uchi" (Ufunuo 3:17); Hawa watu, wakatamani kupata "neema ya Mungu iwaokoayo wanadamu" (Tito 2:11). Ndani ya watu hawa Maneno haya ya salamu kutoka kwa Kristo yaliamsha matumaini yao; waliona kwamba maisha yao yalikuwa chini ya baraka ya Mungu.**[MB 6.2]**

Yesu alikuwa amewapa kikombe cha baraka wale waliojiona kuwa walikuwa "matajiri, wamejitajirisha" (Ufunuo 3:17), wala hawakuwa na haja ya kitu, nao, kwa dharau, na wakageuka na kuiacha zawadi ile nzuri. Yule anayejiona kuwa yu kamili, anayedhani kwamba ni mwema kiasi cha kutosha, naye ameridhika

na hali yake, mtu huyo huwa hajitahidi kuwa mshiriki wa neema na haki Yake Kristo.

Mwenye kiburi haitambui haja yake, na kwa hiyo anaufunga moyo Wake usimpokee Kristo, wala mibaraka Yake isiyo na kikomo aliyokuja kumpa. Hakuna nafasi kwa Yesu moyoni mwa mtu kama huyo. Wale ambao hujiona machoni pao kuwa ni matajiri na waheshimiwa huwa hawaombi kwa imani, wala hawaupokei mbaraka wa Mungu. Huona kuwa wameshiba, na kwa hiyo huenda zao mikono mitupu. Wale wanaojua kwamba hawawezi kujiokoa wenyewe, au kutenda tendo lolote la haki wao wenyewe, hao ndio wanaouthamini msaada uwezao kutolewa na Kristo. Hao ndio maskini wa roho ambao Yesu alisema wana heri.**[MB 7.1]**

Yule ambaye Kristo humsamehe, kwanza anamfanya awe na moyo wa toba, halafu, inakuwa ni kazi Yake Roho Mtakatifu kumsadikisha dhambi yake. Wale ambao mioyo yao imechomwa na Roho wa Mungu wanaona kwamba hakuna wema wo wote ndani yao wenyewe. Huona kwamba mema yote waliyopata kutenda yamechangamana na ubinafsi na dhambi. Kama yule mtoza ushuru, wanasimama mbali, wasithubutu hata kuinua macho yao mbinguni, na kulia, "Ee Mungu, uniwie radhi mimi mwenye dhambi" (Luka 18:13). Nao hubarikiwa. Kuna msamaha kwa yule atubuye; kwa maana Kristo Ndiye "Mwana-Kondoo wa Mungu, aichukuaye dhambi ya ulimwengu" (Yohana 1:29). Ahadi ya Mungu ni hii: "Dhambi zenu zijapokuwa nyekundu sana, zitakuwa nyeupe kama theluji; zijapokuwa nyekundu kama bendera, zitakuwa kama sufu." "Nami nitawapa ninyi moyo mpya …nami nitatia Roho wangu ndani yenu." Isaya 1:18; Ezekieli 36:26,27.**[MB 7.2]**

Juu ya wale walio maskini wa roho Yesu asema, "Ufalme wa mbinguni ni wao." Ufalme huu, si kama ule walioutarajia wale walioyasikia maneno ya Kristo, haikuwa dola ya ulimwengu waliyoifikiria. Kristo alikuwa akiwafunulia wanadamu ufalme wake wa kiroho uliojaa upendo wake, neema yake, haki yake. Ishara ya utawala wa Masihi hujulikana kwa mfano wa Mwana wa Adamu. Watu wake ni maskini wa roho, wenye upole, na wateswao kwa ajili ya haki. Ufalme wa mbinguni ni wao. Ingawa haujatimilika bado, kazi imeanzishwa ndani yao itakayowafanya wapokee "sehemu ya urithi wa watakatifu katika nuru" (Wakolosai 1:12).**[MB 8.1]**

Wote wanaojiona kuwa ni maskini sana wa roho, waonao kuwa hawana wema wo wote ndani yao wenyewe, waweza kupata haki na uwezo kwa kumtazama Yesu. Yeye asema, "Njoni kwangu, ninyi nyote msumbukao na wenye kulemewa na mizigo" Mathayo 11:28. Akuambia ubadili umaskini wako kwa utajiri wa neema yake. Sisi hatustahili kupewa upendo wa Mungu; bali Kristo, dhamana yetu, anastahili, tena aweza kuwaokoa kabisa wote wajao kwake. Si kitu kama maisha yako yaliyopita yalikuwaje, na hata kama hali yako ya sasa ni ya kukatisha tamaa namna gani, ukimwendea Yesu jinsi ulivyo, ukiwa dhaifu, bila msaada, na bila

tumaini, Mwokozi wetu Mwenye huruma atakulaki ukiwa mbali, na kukukumbatia

na kukuvika mavazi ya haki. Hutuweka mbele ya Baba hali tumevikwa mavazi meupe ya tabia yake mwenyewe. Hutuombea mbele ya Mungu akisema: Mimi nilikuwa badala ya mwenye dhambi. Basi usimwangalie huyu aliye mpotovu, bali uniangalie mimi. Kama Shetani angetushtaki kuwa tu wenye dhambi na kudai kuwa sisi ni watu wake halali, damu ya Kristo hutuombea kwa nguvu nyingi zaidi.**[MB 8.2]**

“Mmoja ataniambia, kwa Bwana, peke yake, iko haki na nguvu:…Katika Bwana wazao wote wa Israeli watapewa haki, na kutukuka.” Isaya 45:24,25.**[MB 9.1]**

## “Heri Wenye Huzuni: Maana hao Watafarijika.” Mathayo 5:4.

Huzuni inayotajwa hapa ni huzuni ya kweli moyoni kwa ajili ya dhambi. Yesu asema, “Nami nikiinuliwa juu ya nchi nitawavuta wote kwangu.” Yohana 12:32. Na mtu anapovutwa kumtazama Yesu aliyeinuliwa juu ya msalaba, anatambua kwamba binadamu ni wenye dhambi. Anaona kwamba ni dhambi iliyompiga na kumsulibisha Bwana wa utukufu. Anaona kwamba, ingawa yeye amekuwa akipendwa kwa huruma nyingi isiyoneneka, maisha yake yamekuwa yakionesha picha ya utovu wa shukrani na uasi. Amemwacha Rafiki yake aliye bora kabisa, tena ameidharau zawadi hiyo ya mbinguni iliyokuwa ya thamani sana. Amemsulibisha Mwana wa Mungu mara ya pili kwa nafsi yake, na kuuchoma tena moyo ule uliokuwa ukitoka damu na kupigwa. Ametengwa mbali na Mungu kwa shimo la dhambi ambalo ni pana na jeusi na lenye kina kirefu, naye anahuzunika sana kwa moyo uliopondeka.**[MB 9.2]**

Wenye huzuni kama hiyo “watafarijika.” Mungu hutudhihirishia jinsi tulivyo wenye hatia ili tumkimbilie Kristo, na kwake tupate kuwekwa huru kutoka katika utumwa wa dhambi, na kuufurahia uhuru wa watu wa Mungu. Kwa moyo uliopondeka kweli twaweza kuuendea msalaba na kuuacha pale mzigo wetu wa dhambi.**[MB 10.1]**

Maneno ya Mwokozi yana ujumbe wa faraja kwa wale pia wanaopata mateso au waliofiwa. Huzuni zetu haziji bila sababu. “Maana …(Mungu) hapendi kuwatesa wanadamu. Wala kuwahuzunisha.” Maombolezo 3:33. Mungu anapoachilia tupatwe na majaribu na mateso ni “kwa faida yetu, ili tuushiriki utakatifu wake.” Waebrania 12:10. Likipokewa kwa imani, jaribu lile linalodhaniwa kuwa ni chungu sana na gumu kulivumilia, litaonekana kuwa ni mbaraka. Lile pigo la kikatili linalozimisha furaha zetu hapa duniani, litakuwa njia ya kuyageuza macho yetu kuangalia juu mbinguni. Ni wangapi ambao wasingemjua Yesu kama huzuni isingewaongoza kutafuta faraja ndani Yake! **[MB 10.2]**

Majaribu tunayopata maishani mwetu ni watenda kazi wa Mungu, ambao wanatoa uchafu na ukali katika tabia zetu. Ni njia iletayo maumivu kwetu yanapotusonga,yanapotufanya tuwe pembe mraba, na kutukata-kata, na kutukwatua na kutung'arisha; si jambo rahisi kukandamizwa chini ya jiwe la kunolea. Lakini basi, jiwe hilo, likiwa limetayarishwa hivyo, linaletwa ili kujaza mahali pake katika hekalu la mbinguni. Bwana hafanyi kazi yake hiyo kwa makini na kwa ukamilifu juu ya jiwe lolote lisilofaa. Ni mawe Yake tu ya thamani yanayong'arishwa, ili yafanane na yale ya jumba la kifalme.**[MB 10.3]**

Bwana atatenda kazi hii kwa wale wote wanaoweka tumaini lao ndani Yake. Ushindi wa thamani, upitao kiasi utapatikana kwa wale walio waaminifu. Watu watajifunza, Mafundisho yenye thamani kubwa mno- Uzoefu mkubwa mno wa maisha wataupata **[MB 11.1]**

Baba yetu aliye mbinguni si msahaulifu kamwe wa wale ambao huzuni imewagusa. Daudi alipopanda Mlima wa Mizeituni huku "akilia alipokuwa akipanda; naye alikuwa amejifunika kichwa chake, akaenda hana viatu" (2 Samweli 15:30), Bwana alikuwa akimwangalia na kumhurumia. Daudi alivaa mavazi ya gunia, naye alikuwa akiteseka sana katika dhamiri yake. Ishara zile za nje za kujidhili kwake zilishuhudia majuto aliyokuwa nayo moyoni mwake. Kwa machozi na kuvunjika moyo akaliweka tatizo lake mbele za Mungu, na Bwana hakumwacha mtumishi wake. Kamwe Daudi hakupata kupendwa zaidi moyoni mwa Mungu mwenye upendo kama wakati ule, dhamiri yake ilipokuwa ikimtesa sana, alipokimbia kuokoa maisha yake kutoka kwa adui zake, ambao walikuwa wamechochewa kufanya uasi ule na mwanawe mwenyewe. Bwana asema hivi, "Wote niwapendao mimi nawakemea, na kuwarudi; basi uwe na bidii, ukatubu." Ufunuo 3:19. Kristo huuinua moyo ulioshushwa kwa kujuta na kuutakasa moyo unaoomboleza hata kuufanya uwe makao Yake.**[MB 11.2]**

Lakini dhiki inapotujia, ni wangapi wetu tunaofanana na Yakobo! Tunafikiri kwamba huo ni mkono wa adui; na katika giza tunapigana mweleka kama vipofu mpaka nguvu zetu zote zimekwisha, nasi hatuoni faraja yo yote, wala ukombozi. Kwake Yakobo mguso ule wa Mungu wakati wa mapambazuko ulimdhihirisha yule Mmoja aliyekuwa akishindana naye—yaani, yule Malaika wa Agano; ndipo yeye, akilia kwa kutokuwa na msaada wo wote, akajitupa kifuani mwa Mungu mwenye upendo, na kuupokea mbaraka ule ambao moyo wake ulikuwa ukiutamani sana. Nasi pia inatubidi kujifunza kwamba majaribu yanamaanisha faida kwetu, wala tusidharau kurudiwa na Bwana, wala tusizimie tunapokemewa naye (Waebrania 12:5).**[MB 11.3]**

"Yu heri mtu yule Mungu amwadhibuye;…Kwani Yeye huumiza, lakini tena

huuguza; Yeye hutia jeraha, na mikono Yake huponya. Yeye atakuokoa na mateso sita; naam, hata katika saba hapana uovu utakaokugusa.” Ayubu 5:17-19. Kwa kila mmoja aliyejeruhiwa, Yesu huja na huduma Yake ya uponyaji. Maisha ya mfiwa, na mwenye maumivu, na yule anayeteseka yanaweza kuchangamka kwa kuwako Kwake Yeye aliye wa thamani sana.**[MB 12.1]**

Mungu hataki tuendelee kukandamizwa na huzuni ya kipumbavu, wala kuwa na mioyo inayoendelea kujeruhiwa na kukata tamaa. Yeye angependa sisi tuangalie juu na kuuona uso wa upendo wa mpenzi wetu. Mwokozi aliyebarikiwa anasimama kando ya wengi ambao macho yao yamepofushwa mno kwa machozi yao kiasi kwamba hawamtambui. Anatamani sana kuishika mikono yetu, kutufanya tumwangalie yeye kwa imani ya kawaida, tukimruhusu atuongoze. Moyo Wake U wazi kupokea misiba yetu, huzuni zetu, na majaribu yetu. Ametupenda kwa upendo wa milele, na pande zote ametuzungushia fadhili zake. Twaweza kuukaza moyo wetu Kwake na kuzitafakari fadhili Zake siku nzima. Naye ataiinua mioyo yetu juu ya huzuni na mahangaiko ya kila siku, na kutuingiza katika uwanja wa amani.**[MB 12.2]**

Fikirini haya, enyi watoto wake mpatao mateso na huzuni, furahini mkiwa na tumaini. "Na huku ndiko kushinda kuushindako ulimwengu, hiyo imani yetu." 1 Yohana 5:4.**[MB 12.3]**

Heri wale pia waliao pamoja na Yesu wakiuhurumia ulimwengu huu katika huzuni zake, na kuhuzunika kwa sababu ya dhambi zake. Katika maombolezo kama hayo hakuna kujifikiria binafsi. Yesu alikuwa Mtu wa Huzuni nyingi, alistahimili maumivu makali sana rohoni mwake ambayo hakuna lugha yo yote iwezayo kuyaelezea. Roho yake iliraruriwa na kuchubuliwa kwa sababu ya makosa ya wanadamu. Alifanya kazi ngumu kwa moyo wenye bidii inayomla ili kuwapunguzia wanadamu dhiki na mateso yao, na moyo Wake ukawa mzito sana alipowaona makutano wengi wasiotaka kuja kwake ili wapate kuwa na uzima. Wote ambao ni wafuasi wa Kristo watashiriki uzoefu huo. Watakapoushiriki upendo Wake, wataingia katika taabu Yake aliyokuwa nayo kwa ajili ya kuwaokoa waliopotea. Wakishiriki hapa mateso ya Kristo, watashiriki pia utukufu Wake utakaofunuliwa. Wakiwa pamoja Naye kazini Mwake, wakinywa pamoja Naye kikombe cha huzuni Yake, watakuwa washiriki pamoja Naye pia katika furaha Yake.**[MB 12.4]**

Ilikuwa kwa njia ya mateso Kristo alipata huduma ya kuwafariji watu. Katika mateso yote ya wanadamu Yeye anateseka; na "kwa kuwa Mwenyewe aliteswa alipojaribiwa, aweza kuwasaidia wao wanaojaribiwa."Isaya 63:9; Waebrania 2:18. Katika kazi hii kila mtu aliyeingia katika ushirika wa mateso Yake anayo fursa ya kushiriki. "Kwa kuwa kama vile mateso ya Kristo yanavyozidi kwetu, vivyo hivyo faraja yetu inazidi kwa njia ya Kristo." 2 Wakorintho 1:5. Bwana anayo neema maalumu kwa yule anayeomboleza, na nguvu Yake huyeyusha mioyo ili ipate kuwaleta watu Kwake. Upendo Wake hufungua njia na kuingia ndani ya moyo uliojeruhiwa na kuchubuliwa, na kuwa dawa ya kuponya kwa wale wahuzunikao. "Baba wa rehema, Mungu wa faraja yote; atufarijiye

katika dhiki zetu zote ili nasi tupate kuwafariji wale walio katika dhiki za namna zote, kwa faraja hizo tunazofarijiwa na Mungu.” 2 Wakorintho 1:3,4.**[MB 13.1]**

### “Heri Wenye Upole” Mathayo 5:5.

Katika mibaraka hii yote kuna mkondo unaoonesha maendeleo katika ukuaji wa maisha ya Kikristo. Wale ambao wameona jinsi wanavyomhitaji Kristo, wale ambao wameomboleza kwa sababu ya dhambi na kuketi pamoja na Kristo katika shule ya mateso, watajifunza upole kutoka kwa Mwalimu huyu atokaye kwa Mungu.**[MB 13.2]**

Kuwa na uvumilivu na upole wakati mtu anatendewa mabaya zilikuwa ni tabia ambazo hazikuthaminiwa sana na Mataifa wala na Wayahudi. Usemi uliotolewa na Musa chini ya uvuvio wa Roho Mtakatifu, kwamba alikuwa mpole sana kuwapita wote duniani, usingefikiriwa na watu wa siku zake kuwa ulikuwa sifa njema; badala yake ungeamsha moyo wa kumhurumia au kumdharau. Lakini Kristo anauweka upole miongoni mwa sifa za kwanza za kuingia katika ufalme wake. Katika maisha na tabia Yake, uzuri wa utakatifu wa tabia hii ya thamani unadhihirishwa.**[MB 14.1]**

Yesu, mng’ao wa utukufu wa Baba Yake, hakuona “kule kuwa sawa na Mungu kuwa ni kitu cha kushikamana nacho, bali alijifanya kuwa hana utukufu, akatwaa namna ya mtumwa.” Wafilipi 2:6,7. Katika maisha yote yaliyokuwa duni alikubali kuyapitia, akatembea kati ya wana wa wanadamu, sio kama mfalme, astahiliye kuheshimiwa, bali kama mmoja ambaye utume Wake ulikuwa ni kuwatumikia wengine. Katika mwenendo Wake hakuwa na waa lolote la kuwa na ushupavu wa dini, wala ukali usio na huruma. Mkombozi huyu wa ulimwengu asili Yake ilikuwa ni zaidi ya ile ya malaika, lakini kufungamana na utukufu Wake wa Uungu ulikuwa ni ule upole na unyenyekevu Wake uliowavuta wote Kwake.**[MB 14.2]**

Yesu alijifanya hana utukufu, na katika yote aliyofanya hakujikweza kamwe. Aliyaweka mambo yote chini ya uongozi wa mapenzi ya Baba Yake. Kazi Yake hapa duniani ilipokuwa karibu kumalizika, aliweza kusema, “Nimekutukuza duniani, hali nimeimaliza kazi ile uliyonipa niifanye.” Yohana 17:4. Atwambia, “Mjifunze Kwangu; kwa kuwa Mimi ni mpole na mnyenyekevu wa moyo.” “Mtu yeyote akitaka kunifuata na ajikane mwenyewe” (Mathayo 11:29; 16:24); Hebu ubinafsi uondolewe kabisa, kutoka kwenye kiti cha enzi na wala nafsi isiendelee tena kupata ukuu, ubinafsi usitawale moyo.**[MB 14.3]**

Yule anayemwangalia Kristo katika kujikana nafsi Kwake, unyenyekevu Wake wa moyo, atalazimika kusema, kama Danieli alivyosema zamani, alipomtazama Yule

aliyefanana na wana wa wanadamu, “Uzuri wangu uligeuzwa ndani yangu kuwa uharibifu.” Danieli 10:8. Kujitegemea kwetu na kujiona tu watu wakubwa sana, mambo hayo tunayojisifia huonekana katika ubaya wake halisi kama dalili za

utumwa wetu kwa Shetani. Tabia ya asili ya kibinadamu inajitahidi daima kujidhihirisha, ikiwa tayari kushindana; lakini yule anayejifunza kwa Kristo nafsi yake haionekani, wala kiburi, wala kupenda ukubwa, na mo yoni mwake kuna utulivu. Nafsi yake inawekwa chini ya udhibiti wa Roho Mtakatifu. Hapo ndipo sisi huwa hatuna hamu ya kuikalia nafasi ya juu kabisa. Hatutakuwa na tamaa ya kutaka kujionesha kwa watu; lakini tutaona kwamba mahali petu pa juu kabisa ni miguuni pa Mwokozi wetu. Tunamwangalia Yesu, huku tukiungojea mkono wake utuongoze, tukiisikiliza sauti yake ituongoze. Mtume Paulo alikuwa katika hali hiyo, naye alisema, "Nimesulibiwa pamoja na Kristo, lakini ni hai; wala si mimi tena, bali Kristo yu hai ndani yangu; na uhai nilio nao sasa katika mwili, ninao katika imani ya Mwana wa Mungu, ambaye alinipenda akajitoa nafsi yake kwa ajili yangu." Wagalatia 2:20.**[MB 15.1]**

Tumpokeapo Kristo kama mgeni wetu wa kukaa ndani ya mioyo yetu daima, "amani ya Mungu, ipit ayo akili zote, itatuhifadhi mioyoni mwetu na nia zetu katika Kristo Yesu" (Wafilipi 4:7). Maisha ya Mwokozi wetu alipokuwa hapa duniani, ingawa aliishi kati ya mashindano mengi, yalikuwa ni maisha ya amani. Adui zake wenye hasira walipokuwa wakimfuatia ili wamkamate, aliwaambia, "Aliyenipeleka yu pamoja nami; hakuniacha peke yangu; kwa sababu nafanya siku zote yale yampendezayo." Yohana 8:29. Dhoruba yo yote ya kibinadamu au ya Shetani haikuweza kuivuruga amani aliyokuwa nayo moyoni mwake kutokana na mawasiliano yake kamili na Mungu. Naye atwambia, "Amani nawaachieni; amani yangu nawapa." "Jitieni nira yangu, mjifunze kwangu; kwa kuwa mimi ni mpole na mnyenyekevu wa moyo; nanyi mtapata raha nafsini mwenu." Yohana 14:27; Mathayo 11:29. Istahimilini nira hii ya huduma pamoja nami kwa utukufu wa Mungu na kwa ajili ya kuwaelimisha wanadamu, nanyi mtaiona nira hii kuwa ni laini na mzigo kuwa ni mwepesi.**[MB 15.2]**

Ni kule kujipenda sisi wenyewe kunakoharibu amani yetu. Utu wetu wa zamani ukiwa ungali hai ndani yetu, tunakuwa tayari kila mara kuulinda usidhalilishwe wala usifedheheshwe; lakini tunapokufa, na uhai wetu unapofichwa pamoja na Kristo katika Mungu, hatutaumia moyoni wasipotujali au wakitudharau. Tutakuwa viziwi wakitushutumu na vipofu wakitudharau na kutufedhehesha. "Upendo huvumilia, hufadhili; upendo hauhusudu; upendo hautakabari; haujivuni; haukosi kuwa na adabu; hautafuti mambo yake; hauoni uchungu; hauhesabu mabaya; haufurahii udhalimu, bali hufurahi pamoja na kweli; huvumilia yote; huamini yote; hutumaini yote; hustahimili yote. Upendo haupungui neno wakati wo wote." 1 Wakorintho 13:4-8.**[MB 16.1]**

Furaha inayopatikana katika vyanzo vya kidunia yaweza kubadilikabadilika kulingana na mazingira yanavyobadilika; lakini amani ya Kristo ni amani ya

kudumu inayokaa moyoni. Hiyo haitegemei hali ya aina yo yote katika mazingira

ya maisha yetu, wala wingi wa vitu tulivyo navyo, wala idadi ya marafiki tulio nao. Kristo ni chemchemi ya maji ya uzima, na furaha inayopatikana Kwake haiwezi kukoma kamwe-Haiwezi kufeli.**[MB 16.1]**

Unyenyekevu wa Kristo, ukidhihirishwa nyumbani, utawafanya waliomo wawe na furaha; hauchochei ugomvi, hautoi jibu lo lote kwa hasira, ila huutuliza moyo ulioghadhabika, na kueneza moyo wa upole uwagusao wote walio ndani ya familia hiyo iliyochangamka. Po pote utunzwapo moyo huu wa unyenyekevu, unazifanya familia za humu duniani kuwa sehemu ya familia ile kubwa ya mbinguni.**[MB 16.2]**

Ni afadhali tuvumilie kusingiziwa na watu kuliko kujilitea wenyewe mateso makali yatokanayo na kulipiza kisasi kwa adui zetu. Moyo wa chuki na kulipiza kisasi ulianzia kwa Shetani, na unaweza kuleta maovu tu kwa yule anayekuwa nao. Unyenyekevu wa moyo, yaani, ule upole ambao ni tunda la Kristo akaaye moyoni mwetu, ndiyo siri ya kweli ya kubarikiwa. "Huwapamba wenye upole kwa wokovu." Zaburi 149:4.**[MB 17.1]**

Wenye upole "watairithi nchi." Ilikuwa ni kwa njia ya tamaa ya kujikweza dhambi iliingia duniani, na wazazi wetu wale wa kwanza wakapoteza utawala wao juu ya dunia hii nzuri, yaani, ufalme wao. Ni kwa njia ya kujikana nafsi Kristo anakikomboa kile kilichopotea. Naye asema kwamba sisi tunapaswa kushinda kama Yeye alivyoshinda. Ufunuo 3:21. Kwa kujinyenyekeza na kujisalimisha nafsi zetu tunaweza kuwa warithi pamoja Naye wakati ule "wapole wata[kapo]irithi nchi." Zaburi 37:11.**[MB 17.2]**

Nchi iliyoahidiwa kwa wapole haitakuwa kama hii ya sasa, iliyotiwa giza kwa kivuli cha mauti na laana. "Kama ilivyo ahadi yake, tunatazamia mbingu mpya na nchi mpya, ambayo haki yakaa ndani yake." "Wala hapatakuwa na laana yo yote tena. Na kiti cha enzi cha Mungu na cha Mwana-Kondoo kitakuwamo ndani yake; na watumwa wake watamtumikia." 2 Petro 3:13; Ufunuo 22:3.**[MB 17.3]**

Hakuna kukatishwa tamaa, hakuna huzuni, hakuna dhambi, hakuna mtu awaye yote atakayesema, Mimi mgonjwa; hakuna misafara ya mazishi, hakuna maombolezo, hakuna mauti, hakuna kutengana, hakuna mioyo iliyovunjika; ila Yesu yuko kule, amani iko kule. Kule "hawataona njaa, wala hawataona kiu; hari haitawapiga, wala jua; kwa maana yeye aliyewarehemu atawatangulia, naam, karibu na chemchemi za maji atawaongoza." Isaya 49:10.**[MB 17.4]**

**“Heri Wenye Njaa na Kiu ya Haki; Maana hao Watashibishwa.” Mathayo 5:6.**

HAKI ni utakatifu, yaani, ni kufanana na Mungu, na “Mungu ni upendo.” 1 Yohana 4:16. Ni kuifuata kabisa Sheria ya Mungu, kwa maana “maagizo Yako yote ni ya haki” (Zaburi 119:172), na “pendo ndilo utimilifu wa Sheria” (Warumi 8:10). Haki ni upendo, na upendo ndiyo nuru na uzima wa Mungu. Haki ya Mungu imo ndani ya Kristo. Tunaipokea haki hiyo kwa kumpokea Yeye.**[MB 18.1]**

Haki hii haipatikani kwa kujitahidi sana kwa maumivu, wala kwa kufanya kazi ngumu inayochosha sana, wala kwa kutoa zawadi, wala kwa kujitoa mhanga; bali inatolewa bure kwa kila mtu mwenye njaa na kiu anayetaka kuipokea. “Haya, kila aonaye kiu, njoni majini, naye asiye na fedha; njoni, nunueni, mle; naam, njoni, nunueni …bila fedha na bila thamani [gharama].” “Haki yao inayotoka Kwangu Mimi, asema BWANA,” “na Jina Lake atakaloitwa ni hili, BWANA NI HAKI YETU.” Isaya 55:1; 54:17; Yeremia 23:6.**[MB 18.2]**

Hakuna mjumbe ye yote wa kibinadamu awezaye kutoa kile kitakachomshibisha mtu na kuikata kiu iliyomo moyoni mwake. Lakini Yesu asema: “Tazama, nasimama mlangoni, nabisha; mtu akiisikia sauti Yangu, na kufungua mlango, nitaingia kwake, Nami nitakula pamoja naye, na Yeye pamoja Nami.” “Mimi Ndimi chakula cha uzima; yeye ajaye Kwangu hataona njaa kabisa, naye Mimi, aniaminiye hataona kiu kamwe.” Ufunuo 3:20; Yohana 6:35.**[MB 18.3]**

Tunavyohitaji chakula ili kuihifadhi nguvu ya mwili wetu, ndivyo tunavyomhitaji Kristo, Mkate (chakula) ulioshuka kutoka mbinguni, ili kuendeleza maisha yetu ya kiroho na kutupatia nguvu ya kufanya kazi za Mungu. Kama mwili wetu unavyoendelea daima kupokea lishe inayoendeleza uhai wetu na nguvu, ndivyo roho zetu zinavyopaswa daima kuwasiliana na Kristo, kujitoa Kwake na kumtegemea Yeye kabisa.**[MB 19.1]**

Kama vile msafiri aliyechoka sana anavyotafuta chemchemi jangwani, naye, akiisha kuiona, anakata kiu yake kali sana, ndivyo Mkristo atakavyoona kiu na kujipatia yale maji safi ya uzima, ambayo Kristo Ndiye chemchemi yake.**[MB 19.2]**

Tunapotambua ukamilifu wa tabia ya Mwokozi wetu, tutatamani kubadilishwa kabisa na kufanywa upya kwa mfano wa utakatifu wake. Kadiri tutakavyozidi kumjua Mungu, ndivyo kadiri kitakavyopandishwa juu zaidi kiwango cha tabia tunayotarajia kuwa nayo, nasi tutakuwa na ari kubwa zaidi katika shauku yetu ya kuidhihirisha tabia Yake kwa wengine. Nguvu ya Mungu inaunganika na ile ya mwanadamu wakati ule nafsi ya mtu inapomtafuta sana Mungu, hapo ndipo moyo wenye shauku uwezapo kusema, “Nafsi yangu, umngoje Mungu peke yake kwa kimya, tumaini langu hutoka Kwake.” Zaburi 62:5.**[MB 19.3]**

Kama unajisikia kwamba unayo haja moyoni mwako, kama unaona njaa na kiu ya haki, huo ni ushahidi kwamba Kristo amefanya kazi yake moyoni mwako, ili atafutwe kwa madhumuni ya kukusaidia wewe, kwa njia ya kukupa wewe Roho Mtakatifu, ili akuwezeshe kufanya mambo yale ambayo hayawezekani kabisa kwako kujifanyia mwenyewe. Hatuna haja ya kutuliza kiu yetu kwenye vijito vyenye maji haba, kwani chemchemi kuu yenye maji mengi tunayoweza kunywa bure iko juu yetu, ambayo, kama tutapanda juu zaidi kwa njia ya imani, tutaweza kunywa bila kukoma.**[MB 19.4]**

Maneno ya Mungu ni chemchemi za maji ya uzima. Na kadiri unavyozitafuta chemchemi hizo za maji ya uzima, utaletwa, kwa njia ya Roho, katika ushirika na Kristo. Kweli zinazofahamika zitakuja katika moyo wako kwa njia mpya, mafungu ya Maandiko yatajitokeza kama nuru inayomulika ghafula mbele yako yakiwa na maana mpya, utaona uhusiano uliopo wa zile Kweli nyingine kuhusiana na kazi ya ukombozi, nawe utajua kwamba Kristo anakuongoza wewe, yaani, Mwalimu atokaye kwa Mungu Yu kando yako.**[MB 20.1]**

Yesu alisema, “Ye yote atakayekunywa maji yale nitakayompa mimi, hataona kiu milele; bali yale maji nitakayompa yatakuwa ndani yake chemchemi ya maji, yakibubujikia uzima wa milele.” Yohana 4:14. Roho Mtakatifu anapokufunulia wewe ile kweli, utayaweka moyoni mwako mambo yale ya thamani yanayotokea katika maisha yako, nawe utatamani sana kuwaambia wengine mambo yale yaliyokupa faraja ambayo yamefunuliwa kwako. Utakaposhirikiana nao utawapa wazo fulani jipya lihusulo tabia au kazi Yake Kristo. Utakuwa na mafunuo fulani mapya ya upendo Wake wenye huruma utakayowaambia wale wampendao na wale wasiompenda Yeye.**[MB 20.2]**

“Wapeni watu vitu, nanyi mtapewa,” (Luka 6:38); kwa maana Neno la Mungu ni “chemchemi ya bustani yangu, kisima cha maji yaliyo hai, vijito vya Lebanoni” (Wimbo Ulio Bora 4:15). Moyo ule uliopata kuuonja mara moja tu upendo wa Kristo, unatamani daima kuupata kwa wingi zaidi, na wewe unapowaambia wengine utapokea kwa kipimo kizuri zaidi na kingi zaidi. Kila ufunuo wa Mungu unaokuja moyoni, unaongeza kiwango cha kujua na kupenda. Kilio cha daima toka moyoni ni hiki, “Wewe zaidi,” na jibu la Roho ni hili daima, “Zaidi sana.” Warumi 5:9,10. Kwa maana Mungu wetu hupenda kutufanyia “mambo ya ajabu mno kuliko yote tuyaombayo au tuyawazayo.” Waefeso 3:20. Kwa Yesu, aliyejifanya hana utukufu kwa ajili ya wokovu wa wanadamu waliopotea, Roho Mtakatifu alitolewa bila kipimo. Hivyo ndivyo atakavyotolewa kwa kila mfuasi wa Kristo moyo wote utakapokuwa umetolewa kabisa kwake ili apate kukaa ndani yake. Bwana wetu mwenyewe ametoa agizo hili, “Mjazwe Roho” (Waefeso 5:18), na agizo hili pia ni ahadi kuwa atalitimiza jambo hilo. Ilimpendeza sana Baba

kwamba “utimilifu wote ukae” ndani ya Kristo; “na ninyi mmetimilika katika yeye.” Wakolosai 1:19; 2:10.**[MB 20.3]**

Mungu ametumiminia upendo wake kwa wingi, kama manyunyu ya mvua yanavyoiburudisha ardhi. Anasema, “Dondokeni, enyi mbingu, toka juu, mawingu na yamwage haki; nchi na ifunuke, ili kutoa wokovu, nayo itoe haki ikamee pamoja.” “Maskini na wahitaji wanatafuta maji, wala hapana; ndimi zao zimekauka kwa kiu; mimi, Bwana, nitawasikia, mimi, Mungu wa Israeli, sitawaacha. Nitafunua vijito vya maji juu ya vilima, na chemchemi katikati ya mabonde; nitageuza jangwa kuwa ziwa la maji, na mahali pakavu kuwa vijito vya maji.” Isaya 45:8; 41:17,18.**[MB 21.1]**
“Katika utimilifu Wake sisi sote tulipokea, na neema juu ya neema.” Yohana 1:16.**[MB 21.2]**

### “Heri wenye rehema; Maana hao Watapata Rehema” Mathayo 5:7.

Kwa asili moyo wa mwanadamu u baridi, ni mwovu, wala hauna upendo; wakati wo wote mtu anapoonesha moyo wa huruma na msamaha, hafanyi hivyo yeye mwenyewe, bali huongozwa na Roho wa Mungu anayeugusa moyo wake. “Sisi twapenda kwa maana yeye alitupenda sisi kwanza” (1 Yohana 4:19).

Mungu mwenyewe ndiye chimbuko la huruma yote. Jina lake ni “mwingi wa huruma, mwenye fadhili.” Kutoka 34:6. Hatutendei sisi kulingana na vile tunavyostahili. Hatuulizi kama tunastahili kupewa upendo wake, bali hutumiminia juu yetu utajiri wa upendo wake, ili kutufanya tustahili. Mungu si mwenye kulipa kisasi. Hataki kutuadhibu, bali kutukomboa. Hata ukali unaoonekana katika maongozi yake huwa kwa ajili ya kuwaokoa wapotovu. Anatamani sana moyoni mwake, kwa shauku kubwa, kuwapunguzia wanadamu taabu zao na kuwatibu majeraha yao kwa dawa yake. Ni kweli kwamba Mungu “si mwenye kumhesabia mtu mwovu kuwa hana hatia kamwe” (Kutoka 34:7); lakini anapenda kuiondolea mbali hatia yetu.

Wenye rehema ni “washirika wa tabia ya Mungu,” na ndani yao upendo wa Mungu uliojaa huruma nyingi unaonekana. Wote ambao mioyo yao hushirikiana na moyo wa upendo wa Mungu watawatafuta na kuwaongoa wengine, siyo kuwalaumu. Kristo akikaa moyoni huwa chemchemi isiyokauka kamwe. Pale akaapo, patakuwa na mafuriko ya ukarimu.

Kilio kinapotoka kwa wapotovu, kwa wale wanaojaribiwa, kwa wahanga wabaya kabisa wa umaskini na dhambi, Mkristo haulizi, Je wanastahili? bali anasema,

Nawezaje kuwasaidia? Ndani ya wale walio wabaya kabisa, walioshushwa hadhi

yao, anaona watu ambao Kristo aliwafia ili kuwaokoa na ambao kwa ajili yao Mungu amewapa watoto wake huduma hii ya upatanisho.

Wenye rehema ni wale wanaoonesha huruma yao kwa maskini, kwa watesekao, na kwa wale wanaokandamizwa. Ayubu alisema: “Kwa sababu nalimwokoa maskini aliyenililia, yatima naye, na yule asiyekuwa na mtu wa kumsaidia. Baraka yake yeye aliyekuwa karibu na kupotea ilinijia; nikaufanya moyo wa mjane kuimba kwa furaha. Nalijivika haki, ikanifunika, adili yangu ilikuwa kama joho na kilemba. Nalikuwa macho kwa kipofu, nalikuwa miguu kwa aliyechechemea. Nalikuwa baba kwa mhitaji, na daawa ya mtu nisiyemjua naliichunguza.” Ayubu 29:12-16.
Kuna wengi ambao kwao maisha ni jitihada iwaleteayo maumivu; wanaziona kasoro walizo nazo, nao wanakosa raha, wala hawana imani; wanaona kwamba hawana kitu cho chote ambacho kingewafanya wawe na moyo wa shukrani. Maneno ya upole, mtazamo wa macho wenye huruma, kuwapa maneno yaoneshayo kuwa wanathaminiwa, kwa wengi wanaopambana na maisha na walio wapweke, maneno hayo yangekuwa kama kikombe cha maji baridi kwa mtu mwenye kiu. Neno moja la huruma, tendo moja la wema, mambo hayo yangeiondoa mizigo mizito inayowalemea mabegani mwao wale waliochoka sana na maisha. Na kila neno au tendo jema litendwalo kwao pasipo ubinafsi huonesha upendo wake Kristo alio nao kwa wanadamu waliopotea.

Wenye rehema “watapata rehema.” “Nafsi ya mtu mkarimu itawandishwa; anyweshaye atanyweshwa mwenyewe.” Mithali 11:25. Kuna amani tamu kwa mwenye moyo wa huruma, ataridhika moyoni mwake kwa maisha yake ya kutoa huduma, akijisahau mwenyewe, kwa faida ya watu wengine. Roho Mtakatifu akaaye moyoni mwake na ambaye hujidhihirisha katika maisha ya mtu huyo, atailainisha mioyo migumu na kuamsha huruma na upendo ndani yake. Utavuna kile unachopanda. “Heri amkumbukaye mnyonge;... Bwana atamlinda na kumhifadhi hai, naye atafanikiwa katika nchi; wala usimtie katika hali wamtakiayo adui zake. Bwana atamtegemeza alipo mgonjwa kitandani, katika ugonjwa wake umemtandikia.” Zaburi 41:1-3.

Yule aliyejitoa maisha yake kwa Mungu katika kuwahudumia watoto wake, huunganishwa na yeye aliyeweka chini ya udhibiti wake mali na vitu vyote ulimwenguni. Maisha yake yanafungwa pamoja na maisha ya Mungu kwa mnyororo wa dhahabu wa ahadi zake zisizobadilika kamwe. Mungu hatamwacha peke yake katika saa yake ya mateso na mahitaji. “Na Mungu wangu atawajazeni kila mnachohitaji kwa kadiri ya utajiri wake, katika utukufu, ndani ya Kristo Yesu.” Wafilipi 4:19. Na katika saa ya mahitaji yake ya mwisho yule mwenye rehema atapata kimbilio lake katika rehema zake Mwokozi mwenye huruma,

naye atakaribishwa katika makao yale ya milele.

**“Heri Wenye Moyo Safi; Maana hao Watamwona Mungu”**
**Mathayo 5:8.**

Wayahudi walikuwa waangalifu sana kuhusu usafi uliohusiana na sheria ya kafara, kiasi kwamba maagizo yao yalikuwa yakiwalemea sana watu. Akili zao zilijazwa na sheria na vizuizi vyake na hofu ya kufanya unajisi unaoonekana kwa nje, wala hawakutambua kwamba kujipenda wenyewe na kutaka kuwadhuru wengine kulitia waa moyoni mwao.

Yesu hakuutaja usafi huo wa sheria ya kafara kuwa ni mojawapo ya masharti ya kuingia katika ufalme wake, bali alionesha haja ya kuwa na usafi wa moyo. Hekima itokayo juu, “kwanza ni safi.” Yakobo 3:17. Katika mji wa Mungu hakitaingia cho chote kinachotia unajisi. Wote ambao watakuwa wakazi kule, watakuwa wamekuwa na moyo safi wakiwa hapa. Ndani ya yule anayejifunza juu ya Yesu, kutaonekana hali inayoendelea ya kuchukia tabia mbaya, lugha chafu, na mawazo yote yasiyofaa. Kristo akikaa moyoni, kutakuwa na usafi na uadilifu wa mawazo na mwenendo.

Lakini maneno haya ya Yesu, “Heri wenye moyo safi,” yana maana sana—sio tu safi katika maana ile ambayo ulimwengu unauelewa usafi, yaani, kuachana na anasa, kuwa safi mbali na tamaa mbaya za mwili, bali ni kuwa mkweli katika makusudi yaliyojificha moyo ni na sababu zake zinazopelekea kuyafanya mambo hayo, ni kuachana na kiburi na kutaka makuu, ni kuwa mnyenyekevu, asiyejipenda mwenyewe, mwenye tabia kama ya mtoto mdogo.

Ni kifananacho tu kiwezacho kukithamini kile kifananacho nacho. Usipoikubali maishani mwako kanuni ya upendo ujitoao mhanga, ambayo ni kanuni ya tabia yake, huwezi kumjua Mungu. Moyo uliodanganywa na Shetani humwona Mungu kama dikteta vile, asiye na huruma; tabia za uchoyo alizo nazo mwanadamu, hata zile alizo nazo Shetani mwenyewe, anapewa huyo Muumbaji mwenye upendo. “Ukadhani” asema yeye “ya kuwa Mimi ni kama wewe.” Zaburi 50:21. Maongozi yake hutafsiriwa kuwa ni kuonesha tabia yake ya kidikteta na ya kulipiza kisasi. Uzuri wa zile kweli zake, ambazo ni za juu kama vile mbingu ilivyo juu na zinadumu milele zote, hautambuliwi. Kwa kundi kubwa mno la wanadamu, Kristo mwenyewe ni “kama mzizi katika nchi kavu;” nao wanamwona kuwa “hana umbo wala uzuri;... hana uzuri hata wamtamani.” Isaya 53:2. Yesu alipokaa kati ya watu, akiwa ufunuo wa Mungu katika mwili wa kibinadamu, Waandishi na Mafarisayo walimwambia, “Wewe u Msamaria, nawe una pepo.” Yohana 8:48. Hata wanafunzi wake walikuwa wamepofushwa mno macho yao kwa ubinafsi uliokuwamo mioyoni mwao, hata walikuwa wazito kumwelewa ye ye aliyekuwa amekuja kwao kuwaonesha upendo wa Baba yake. Hii ndiyo maana

Yesu alitembea kati ya watu akiwa mpweke. Walimwelewa kikamilifu kule mbinguni tu.

Kristo atakapokuja na utukufu wake, waovu hawatastahimili kumwangalia. Mwanga wa kuwako kwake, ambao ni uzima kwao wampendao, ni kifo kwa waovu. Kwao matarajio ya kuja kwake ni "kuitazamia hukumu yenye kutisha, na ukali wa moto ulio tayari kuwala wao wapingao." Waebrania 10:27. Atakapoonekana, wataomba wafichwe wasiuone uso wake yeye aliyekufa ili kuwakomboa.

Lakini kwa mioyo ile iliyotakaswa na Roho Mtakatifu akaaye ndani yao, mambo yote yatakuwa yamebadilika. Hao wanaweza kumjua Mungu. Musa alifunikwa katika ufa wa mwamba utukufu wa Bwana ulipodhihirishwa kwake; na ni wakati ule tunapofichwa ndani ya Kristo, ndipo tunauona upendo wa Mungu.

"Apendaye usafi wa moyo, na neema ya midomo; Mfalme atakuwa rafiki yake." Mithali 22:11. Kwa imani tunamwangalia yeye hivi sasa. Katika mambo yale yanayotupata kila siku katika maisha yetu, tunatambua wema wake na huruma zake kwa njia ya maongozi yake yanayodhihirishwa kwetu. Tunamtambua yeye kwa tabia ya Mwanawe. Roho Mtakatifu anaichukua ile kweli inayomhusu Mungu na yeye aliyemtuma, na kuifunua katika ufahamu wetu na mioyoni mwetu. Wenye moyo safi wanamwona Mungu katika uhusiano mpya unaowafanya wampende kama Mkombozi wao; na wakati wanatambua usafi na uzuri wa tabia yake, wanatamani sana kufanana naye. Wanamwona yeye kuwa ni Mungu anayetamani sana kumkumbatia mwana aliyetubu, na mioyo yao inajawa na furaha isiyoneneka, yenye utukufu.

Wenye moyo safi wanamtambua Muumbaji katika kazi zake zilizofanywa kwa mkono wake wenye nguvu nyingi, katika vitu vizuri vilivyomo ulimwenguni. Katika Neno lake lililoandikwa wanasoma ufunuo wa rehema zake kwa wazi zaidi, wema wake, na neema yake. Kweli zile zilizofichwa kwa wenye hekima na wenye busara hufunuliwa kwa watoto wachanga. Uzuri na thamani ya ile kweli, mambo ambayo hayatambuliwi na wenye hekima wa dunia, daima huendelea kufunuliwa wazi kwa wale walio na hamu inayomtegemea kama ile ya mtoto ya kutaka kujua na kufanya mapenzi ya Mungu. Tunaitambua, sisi wenyewe, ile kweli tunapokuwa washirika wa tabia ya uungu.

Wenye moyo safi wanaishi mbele za Mungu kabisa kwa kipindi anachowapa katika ulimwengu huu. Na tena watamwona uso kwa uso siku za usoni, watakapokuwa na hali ya kutokufa milele, kama Adamu alivyokuwa nayo alipotembea na kuongea na Mungu katika Edeni. "Maana wakati wa sasa tunaona kwa kioo kwa

jinsi ya fumbo; wakati ule tutaona uso kwa uso.” 1 Wakorintho 13:12.

**“Heri Wapatanishi;**
**Maana hao Wataitwa Wana wa Mungu” Mathayo 5:9.**

Kristo ndiye “Mfalme wa amani” (Isaya 9:6), tena ni kazi yake kuirudisha duniani na mbinguni amani iliyovurugwa na dhambi. “Basi tukiisha kuhesabiwa haki itokayo katika imani, na tuwe na amani kwa Mungu, kwa njia ya Bwana wetu Yesu Kristo.” Warumi 5:1. Ye yote anayekubali kuacha dhambi, na kuufungua moyo wake ili upate kupokea upendo wa Kristo, anageuka na kuwa mshirika wa amani hii itokayo mbinguni.

Hakuna sababu nyingine ya kupata amani zaidi ya hii. Neema ya Kristo ikipokewa moyoni, itaushinda uadui uliomo moyoni; itapunguza migongano na kuujaza moyo na upendo. Yule aliye na amani na Mungu na wanadamu wenzake hawezi kuhuzunishwa. Wivu hautakuwamo moyoni mwake; kuwawazia watu mabaya hakutapata nafasi mle; chuki haiwezi kuwamo. Moyo unaopatana na Mungu unashiriki amani itokayo mbinguni, nao utaueneza pande zote mvuto wake uletao furaha kwa wote. Roho ya amani itatua kama umande juu ya mioyo iliyochoka na ile inayosumbuka kutokana na mashindano yaliyomo duniani.

Wafuasi wake Kristo hutumwa duniani na neno la ujumbe wa amani. Ye yote, ambaye kwa mvuto wake wa kimya asioujua wa maisha matakatifu, atakayeudhihirisha upendo wa Kristo; ye yote ambaye, kwa neno au tendo, atamwongoza mwingine kuiacha dhambi na kuutoa moyo wake kwa Mungu, huyo ndiye msuluhishi.

“Heri wapatanishi: maana hao wataitwa wana wa Mungu.” Amani waliyo nayo moyoni huonesha kwamba wanashirikiana na Mbingu.” Wema wa Kristo huwazunguka kama manukato. Maisha yao ya kupendeza, na uzuri wa tabia yao, huwadhihirishia walimwengu ya kuwa wao ni wana wa Mungu. Wengine huwatambua ya kuwa wamekuwa pamoja na Yesu. “Kila apendaye amezaliwa na Mungu.” “Lakini mtu awaye yote asipokuwa na Roho ya Kristo, huyo si wake;” “kwa kuwa wote wanaoongozwa na Roho wa Mungu hao ndio wana wa Mungu.” 1 Yohana 4:7; Warumi 8:9,14.

“Na hayo mabaki ya Yakobo yatakuwa kati ya kabila nyingi mfano wa umande utokao kwa Bwana, mfano wa manyunyu katika manyasi; yasiyomngojea mtu, wala kuwakawilia wanadamu.” Mika 5:7.

**“Heri Wenye Kuudhiwa kwa Ajili ya Haki: Maana Ufalme wa Mbinguni ni Wao.” Mathayo 5:10.**

Yesu hawapi wafuasi wake tumaini la kupata fahari na mali nyingi hapa duniani, na kuwa na maisha yasiyokuwa na majaribu, lakini huwaonesha faida kubwa ya kutembea pamoja na Bwana wao katika njia za kujikana nafsi na kuaibishwa, kwa sababu ulimwengu hauwatambui.

Yeye aliyekuja kuukomboa ulimwengu uliopotea alipingwa na majeshi yaliyoungana ya maadui wa Mungu na wanadamu. Katika muungano huo mwovu usio na huruma, wanadamu waovu na malaika waovu walijipanga kupigana na Mfalme wa Amani. Ingawa Maneno Yake yote na matendo yake yote yalionesha huruma ya Mungu, hali Yake ya kutofanana na walimwengu ilichochea chuki kali mno dhidi Yake. Kwa sababu yeye hakuwaruhusu wanadamu kutimiza tamaa mbaya na hasira tulizo nazo katika tabia yetu tuliyozaliwa nayo, aliamsha upinzani na uadui mkali sana. Na hivyo ndivyo ilivyo kwa "wote wapendao kuishi maisha ya utauwa katika Kristo Yesu." 2 Timotheo 3:12. Kati ya haki na dhambi, upendo na chuki, kweli na uongo, kuna pambano lisilozuilika. Mtu anapoonesha upendo wa Kristo na uzuri wa utakatifu, anawavuta kutoka kwa Shetani raia wa ufalme wake, na yule mkuu wa uovu anaamshwa na kupinga. Mateso na shutuma huwangojea wote wajazwao na Roho wa Kristo. Hali ya mateso hubadilika kufuatana na nyakati, lakini kanuni—roho iliyo nyuma yake—ni ile ile ambayo imepata kuwaua wateule wa Bwana tangu siku zile za Habili.

Wanadamu wanapojitahidi kupatana na Mungu, watagundua kwamba chuki ya msalaba haijakoma. Falme na mamlaka, na majeshi ya pepo wabaya katika ulimwengu wa roho hujipanga kupigana nao wote wanaojitoa kuitii Sheria ile ya mbinguni. Kwa hiyo, mbali na kuwaletea sononeko, mateso yangewaletea furaha wanafunzi wa Kristo, kwa maana huo ni ushahidi kwamba wao wanazifuata nyayo za Bwana wao.

Ingawa Bwana hakuwaahidi watu wake ya kuwa hawatapata majaribu, amewaahidi mambo yaliyo bora zaidi. Amesema, "Kadiri ya siku zako ndivyo zitakavyokuwa nguvu zako." "Neema yangu yakutosha; maana uwezo wangu hutimilika katika udhaifu." Kumbukumbu la Torati 33:25; 2 Wakorintho 12:9. Ukitakiwa kupita katika tanuru kali la moto kwa ajili yake, Yesu atakuwa kando yako kama vile alivyokuwa kando ya Waebrania waaminifu wale watatu kule Babeli. Wale wampendao Mkombozi wao wataifurahia kila nafasi watakayopata ya kushiriki pamoja naye aibu na shutuma. Pendo lile walilo nalo kwa Bwana wao linafanya mateso kwa ajili yake yawe matamu.

Katika vipindi vyote Shetani amewatesa watu wa Mungu. Amewaumiza vibaya sana na kuwaua, lakini katika kufa kwao walikuwa washindi. Kwa imani yao thabiti walimdhihirisha Yule mwenye nguvu kuliko Shetani. Shetani aliweza

kutesa sana na kuua mwili, lakini hakuweza kuugusa uzima uliofichwa pamoja na

Kristo kwa Mungu. Aliweza kuwatia kifungoni, lakini hakuweza kuzifunga roho zao. Waliweza kutazama mbali na giza lile nene na kuuona utukufu, wakisema, “Nayahesabu mateso ya wakati huu wa sasa kuwa si kitu kama utukufu ule utakaofunuliwa kwetu.” “Maana dhiki yetu nyepesi, iliyo ya muda wa kitambo tu, yatufanyia utukufu wa milele uzidio kuwa mwingi sana.” Warumi 8:18; 2 Wakorintho 4:17.

Kwa njia ya majaribu na mateso, utukufu—yaani, tabia ya Mungu hudhihirishwa ndani ya wateule wake. Kanisa la Mungu, lichukiwalo na kuteswa na ulimwengu, huelimishwa na kuadilishwa katika shule ya Kristo. Wanatembea katika njia ile nyembamba hapa duniani; wanatakaswa katika tanuru la mateso. Wanamfuata Kristo kupitia katika mashindano makali; wanastahimili kujikana nafsi na kuonjeshwa uchungu wa kukatishwa tamaa vibaya sana; lakini maisha yao machungu huwafundisha ubaya wa hatia na mateso yatokanayo na dhambi, nao wanaiangalia dhambi kwa chuki kubwa. Wakiwa washiriki wa mateso ya Kristo, wanakusudiwa kuwa washiriki wa utukufu Wake. Katika maono yake matakatifu nabii aliona ushindi mkubwa wa watu wa Mungu. Anasema, “Nikaona kitu kama mfano wa bahari ya kioo iliyochangamana na moto, na wale wenye kushinda,…wamesimama kandokando ya hiyo bahari ya kioo, wenye vinubi vya Mungu. Nao wauimba wimbo wa Musa, mtumwa wa Mungu, na wimbo wa Mwana-Kondoo, wakisema, Ni makuu, na ya ajabu, matendo Yako, Ee Bwana Mungu Mwenyezi; Ni za haki, na za Kweli, njia Zako, Ee Mfalme wa mataifa” “Hao ndio wanaotoka katika dhiki ile iliyo kuu, nao wamefua mavazi yao na kuyafanya meupe katika damu ya Mwana-Kondoo. Kwa hiyo wako mbele ya kiti cha enzi cha Mungu, nao wanamtumikia mchana na usiku katika Hekalu Lake; na Yeye aketiye katika kiti cha enzi atatanda hema yake juu yao.” Ufunuo 15:2,3; 7:14,15.

### “Heri Ninyi Watakapowashutumu.” Mathayo 5:11.

Tangu kuanguka kwake, Shetani amefanya kazi yake kwa kutumia njia za udanganyifu. Kama alivyomweleza Mungu vibaya, hivyo ndivyo, kupitia kwa vibaraka wake, anavyowaeleza vibaya watoto wa Mungu. Mwokozi asema, “Na laumu zao wanaokulaumu zimenipata.” Zaburi 69:9. Kwa njia iyo hiyo laumu hizo zinawaangukia wanafunzi wake.

Hajapata kuwako kamwe mtu mmoja aliyetembea kati ya wanadamu aliyesingiziwa vibaya kwa ukatili mwingi kama Mwana wa Adamu. Alidharauliwa na kudhihakiwa kwa sababu ya utii wake usiopindishwa kwa kanuni za Sheria takatifu ya Mungu. Walimchukia bila sababu yoyote. Hata hivyo, alisimama kimya mbele ya adui Zake, akatangaza kwamba shutuma ni sehemu ya urithi wa

Mkristo, akawashauri wafuasi Wake jinsi ya kupambana na mishale ya madhara iliyolengwa kwao, akiwaagiza wasife moyo wanapokuwa chini ya mateso.

*y*

Ingawa masingizio yanaweza kuichafua sifa ya mtu, hayawezi kuitia waa tabia yake. Hiyo inalindwa na Mungu. Kwa kadiri tusivyokubali kutenda dhambi, hakuna mamlaka yo yote, iwe ya wanadamu au ya Shetani, iwezayo kuitia waa roho ya mtu. Mtu yule aliyekaza moyo wake kumtegemea Mungu ni yule yule tu katika saa ya majaribu yake makali mno na katika mazingira ya kukatisha tamaa mno kama vile alivyokuwa alipokuwa amefanikiwa, yaani, wakati ule nuru na upendeleo wa Mungu vilipoonekana kuwa juu yake. Maneno yake, makusudi ya moyoni mwake, matendo yake, huenda yakaelezwa vibaya na kwa uongo, ila yeye hajali, kwa sababu ana mambo makubwa zaidi ayapendayo ambayo yako hatarini. Kama Musa, anastahimili "kama amwonaye yeye asiyeonekana" (Waebrania 11:27); haviangalii "vinavyoonekana, bali visivyoonekana" (2 Wakorintho 4:18). Kristo anajua yote yanayoeleweka vibaya na yanayoelezwa vibaya na wanadamu. Watoto wake wanaweza kumudu kungoja kwa utulivu na ustahimilivu na tumaini, haidhuru wakashifiwe na kudharauliwa vibaya mno jinsi gani; kwa maana hakuna siri ambayo haitafunuliwa, na wale wanaomheshimu Mungu wataheshimiwa naye mbele ya wanadamu na malaika.

"Heri ninyi watakapowashutumu na kuwaudhi" alisema Yesu, "Furahini, na kushangilia." Naye akawaelekeza wasikilizaji wake kwa manabii walionena kwa jina la Bwana, ili "wawe mfano wa kustahimili mabaya na wa uvumilivu." Yakobo 5:10. Habili, Mkristo wa kwanza kabisa katika watoto wa Adamu, alikufa kifo cha mfiadini. Henoko alitembea na Mungu, na ulimwengu haukumjua.Nuhu alidhihakiwa kama shupavu wa dini asiyetumia akili na mvumishaji wa mambo ya kuogofya. "Wengine walijaribiwa kwa dhihaka na mapigo, naam, kwa mafungo, na kwa kutiwa gerezani." "Lakini wengine waliumizwa vibaya hata kuuawa, wasikubali ukombozi, ili wapate ufufuo ulio bora." Waebrania 11:36,35.

Katika nyakati zote wajumbe wa Mungu aliowachagua wamedhihakiwa na kuteswa, lakini kwa mateso yao, maarifa ya kumjua Mungu yalienezwa kila mahali. Kila mwanafunzi wa Kristo hana budi kuingia katika safu za jeshi lake na kuiendeleza mbele kazi ile ile, akijua kwamba maadui wa kazi hiyo hawawezi kufanya lo lote dhidi ya hiyo kweli, bali kwa ajili ya hiyo kweli. Mungu anakusudia kwamba kweli yake italetwa mbele ya watu na kuwa somo la kuchunguzwa na kujadiliwa, hata kwa njia ya dharau inayowekwa juu yake. Akili za watu ni lazima zitikiswe sana; kila mabishano, kila shutuma, kila juhudi ya kuzuia uhuru wa dhamiri, ni njia anayotumia Mungu kuziamsha akili za watu ambazo, vinginevyo, zingeweza kulala usingizi.

Ni mara nyingi jinsi gani matokeo hayo yameonekana katika historia ya wajumbe wa Mungu! Stefano, mwenye tabia nzuri na mnenaji mwenye ufasaha, alipopigwa mawe na kufa kutokana na uchochezi wa Baraza Kuu la Kiyahudi (Sanhedrin), hapakuwa na hasara yo yote kwa kazi ya Injili. Nuru ile ya mbinguni iliyoutukuza

uso wake, huruma ya Mungu aliyoionesha katika ombi lake alipokuwa akifa,

vilikuwa kama mshale mkali uliomchoma mioyoni mwake yule Mwanabaraza la Kiyahudi aliyesimama karibu pale, na Sauli, yule Farisayo mtesaji, akawa chombo kiteule cha Mungu ili alichukue jina la Kristo mbele ya mataifa, na wafalme, na wana wa Israeli (Matendo 9:15). Na miaka mingi baadaye, Paulo, akiwa mzee, aliandika akiwa kifungoni mwake kule Rumi, alisema, "Wengine wanahubiri habari za Kristo kwa sababu ya husuda na fitina …si kwa moyo mweupe, wakidhani kuongeza dhiki za kufungwa kwangu … Yadhuru nini? Lakini kwa njia zote, ikiwa ni kwa hila au ikiwa ni kwa kweli, Kristo anahubiriwa." Wafilipi 1:15,16-18.Kwa njia ya kufungwa kwake Paulo, Injili ilienea na watu wakavutwa kwa Kristo na kuongoka moyo hata katika jumba la Kaisari mwenyewe. Kwa njia ya kujitahidi kwake Shetani, ili apate kuiharibu ile mbegu isiyoharibika, mbegu hiyo, yaani "neno la Mungu lenye uzima, lidumulo hata milele" (1 Petro 1:23), inapandwa mioyoni mwa wanadamu, kwa njia ya shutuma na mateso ya watu wake, jina la Kristo linatukuzwa, na watu wanapata kuokolewa.

Thawabu ni kubwa kule mbinguni kwa wale ambao wanamshuhudia Kristo kwa njia ya mateso na shutuma. Watu wanapotazamia kufanikiwa hapa duniani, Yesu anayaelekeza macho yao kwenye thawabu ile mbinguni. Lakini haiweki yote katika maisha yale ya baadaye; inaanzia hapa. Bwana alimtokea Ibrahimu zamani na kumwambia, "Mimi ni ngao yako, na thawabu yako kubwa sana." Mwanzo 15:1. Hiyo ndiyo thawabu ya wote wanaomfuata Kristo. Yehova Imanueli—Yeye "ambaye ndani yake …hazina zote za hekima na maarifa zimesitirika," ambaye "katika yeye unakaa utimilifu wote wa Mungu, kwa jinsi ya kimwili" (Wakolosai 2:3,9)—kumjua yeye, kuwa naye, kadiri moyo wako unavyozidi kujifunua kwake na kupokea tabia yake; kuujua upendo wake na nguvu zake, kuwa na utajiri wa Kristo usiopimika, na kuzidi "kufahamu pamoja na watakatifu wote jinsi ulivyo upana na urefu, na kimo na kina; na kuujua upendo wake Kristo, upitao ufahamu jinsi ulivyo mwingi, mpate kutimilika kwa utimilifu wote wa Mungu," (Waefeso 3:18,19)n—"huu ndio urithi wa watumishi wa Bwana, na haki yao inayotoka kwangu mimi, asema Bwana." Isaya 54:17.

Ilikuwa ni furaha hiyo iliyoijaza mioyo ya Paulo na Sila walipoomba na kumwimbia Mungu nyimbo za kumsifu usiku wa manane kule Filipi gerezani. Kristo alikuwa pamoja nao, na nuru ya kuwako kwake ikalimulika lile giza kwa utukufu uliotoka katika zile nyua za mbinguni. Kutoka Rumi Paulo, akiwa hajali minyororo yake, alipoiona Injili ilivyoenea, aliandika hivi, "Na kwa hiyo nafurahi, naam, name nitafurahi." Wafilipi 1:18. Tena maneno yale yale ya Kristo aliyoyasema juu mlimani yanatoa mwangwi wake tena katika ujumbe wa Paulo kwa Kanisa la Filipi, wakiwa katikati ya mateso yao, anawaambia, "Furahini katika Bwana sikuzote; tena nasema, Furahini." Wafilipi 4:4.

Chumvi inathaminiwa kwa sababu ya nguvu yake ihifadhiyo kitu kisioze; na Mungu anapowaita watoto wake kuwa ni chumvi, angependa kuwafundisha kwamba kusudi lake la kuwafanya wawe raia wa neema yake ni kwamba wawe wajumbe wake katika kuwaokoa wengine. Kusudi la Mungu la kuwachagua watu wake mbele ya ulimwengu wote halikuwa tu kwamba awafanye wana na binti zake, bali kwamba kupitia kwao ulimwengu huu ungeweza kuipokea neema ile iletayo wokovu. Tito 2:11. Bwana alipomchagua Ibrahimu, haikuwa tu ili apate kuwa rafiki mpendwa wa Mungu, ila awe njia ya Mungu ya kuwaletea mataifa mema ambayo yalikuwa ni haki yao kuyapata. Yesu, alipoomba sala ile ya mwisho pamoja na wanafunzi wake kabla ya kusulibiwa kwake, alisema, "Na kwa ajili yao najiweka wakfu mwenyewe, ili na hao watakaswe katika kweli." Yohana 17:19. Vilevile Wakristo wanaotakaswa kwa ile kweli watakuwa na sifa zile ziokoazo zinazouhifadhi ulimwengu huu usiharibike kabisa.

Chumvi ni lazima ichanganywe na kitu kile ambacho inaongezwa ndani yake; ni lazima ipenye ndani na kuchanganyika kabisa nacho ili ipate kukihifadhi kisioze. Hivyo kwa njia ya kukutana na kuchangamana nao, watu wanaweza kufikiwa na uweza uokoao wa Injili. Hawaokolewi katika makundi, bali kama mtu mmoja mmoja. Mvuto wa mtu binafsi una nguvu. Yatupasa kwenda karibu na wale tunaotaka kuwaletea msaada.

Ladha ya chumvi huwakilisha nguvu iliyo hai ya Mkristo—yaani, upendo wa Yesu ulio moyoni, haki yake Kristo inayoenea katika maisha yote ya mtu. Upendo wa Kristo huenea polepole katika mwili wote na kutenda kazi yake kwa nguvu. Kama umo ndani yetu, utabubujika kwenda kwa wengine. Tutakuja karibu sana nao kiasi cha kuifanya mioyo yao itiwe joto kwa vile tunavyowajali bila kuwa na ubinafsi na kuwapenda. Waumini wa kweli wanatawanya polepole nguvu yao iliyo hai, ambayo inapenya mpaka ndani na kuwapa nguvu mpya ya kimaadili watu wale wanaowahudumia. Hiyo si nguvu ya yule mtu mwenyewe, bali ni nguvu ya Ro ho Mtakatifu inayofanya kazi hiyo ya kuwabadilisha tabia.

Yesu aliongeza onyo hili zito: "Chumvi ikiwa imeharibika itatiwa nini hata ikolee? Haifai tena kabisa, ila kutupwa nje na kukanyagwa na watu."

Walipoyasikiliza maneno yale ya Kristo, watu wale waliweza kuiona chumvi nyeupe iking'aa katika njia nyingi walimokuwa wameitupa kwa sababu ilikuwa imepoteza ladha yake na hivyo ilikuwa haifai. Iliwakilisha vizuri hali waliyokuwa nayo wale Mafarisayo na athari ya dini yao kwa jamii ile. Inayawakilisha maisha ya kila mtu ambaye nguvu ya neema ya Mungu imemtoka na ambaye amegeuka na kuwa baridi na kuwa bila Kristo. Haidhuru madai yake ya dini yaweje, mtu kama huyo anatazamwa na watu na malaika kama mtu aliyepoa na asiyependeza.

Ni kwa watu kama hao Kristo asema: “Ingekuwa heri kama ungekuwa badiri au

moto. Basi, kwa sababu una uvuguvugu, wala hu baridi wala moto, nitakutapika utoke katika kinywa changu.” Ufunuo 3:15,16.

Bila kuwa na imani hai kwa Kristo kama Mwokozi wetu binafsi ni vigumu kabisa kuufanya mvuto wetu uwe na nguvu ya kuushawishi ulimwengu huu ulio na mashaka juu ya Mungu. Hatuwezi kuwapa wengine kile ambacho sisi wenyewe hatunacho. Ni kwa kiwango kile kile kinacholingana na moyo wetu wa kumtumikia na kujitoa wakfu kwa Kristo tunakuwa na mvuto unaowaletea mibaraka na kuwainua wanadamu. Kama sisi hatutoi huduma yo yote, hatuna upendo wa kweli, hatuna uzoefu wa Kikristo katika maisha yetu, basi, tutakuwa hatuna uwezo wo wote wa kuwasaidia wengine, hatutakuwa tumeunganishwa na mbingu, wala ha tutakuwa na harufu ya Kristo katika maisha yetu. Roho Mtakatifu asipoweza kututumia sisi kama wajumbe wake ambao kupitia kwetu tunaweza kuupasha ulimwengu huu habari za ile kweli kama ilivyo ndani ya Kristo, tunafanana na chumvi iliyoharibika, isiyofaa kitu. Kwa kupungukiwa kwetu na neema yake Kristo tunaushuhudia ulimwengu huu ya kuwa ile kweli tunayodai kwamba tunaiamini haina uwezo wo wote wa kutakasa; na hivyo, kadiri mvuto wetu uhusikavyo, tunalitangua neno la Mungu. “Nijaposema kwa lugha za wanadamu na za malaika, kama sina upendo, nimekuwa shaba iliayo na upatu uvumao. Tena nijapokuwa na unabii, na kujua siri zote na maarifa yote, nijapokuwa na imani timilifu kiasi cha kuweza kuhamisha milima, kama sina upendo, si kitu mimi. Tena nikitoa mali za ngu zote kuwalisha maskini, tena nikijitoa mwili wangu niungue moto, kama sina upendo, hainifaidii kitu.” 1 Wakorintho 13:1-3.

Upendo ukijaa moyoni mwetu, utafurika kwa wengine, si kwa kuwa tumepokea fadhili zao, bali ni kwa sababu upendo huo ni kanuni ya matendo yetu kwao. Upendo huibadilisha tabia yetu, huzidhibiti tamaa zote, huuzima uadui, na kuyaadilisha mapenzi yetu ya kibinadamu. Upendo huo ni mpana kama malimwengu yalivyo, tena unapatana na ule wa malaika wahudumuo. Ukitunzwa moyoni mwetu, unayafanya maisha yetu yote kuwa matamu na kuimwaga mibaraka yake juu ya wote watuzungukao. Ni huo, na huo tu, unaoweza kutufanya sisi kuwa chumvi ya dunia.

“Ninyi Ni Nuru ya ulimwengu” Mathayo 5:14.

Yesu alipowafundisha watu, alifanya mafundisho yake kuwa ma tamu na ya kuvutia kwa mawazo ya wale waliomsikiliza kwa njia ya kueleza mara kwa mara kwa mifano mingi akitumia viumbe vya asili vilivyowazunguka pande zote. Watu walikuwa wamekusanyika pamoja ilipokuwa bado ni asubuhi. Jua tukufu, likipanda juu zaidi na zaidi katika mbingu ya rangi ya samawati, lilikuwa

likivifukuzilia mbali vivuli vilivyojificha mabondeni na kati ya njia nyembamba

za milimani. Uzuri wa mbingu zile za mashariki ulikuwa bado haujatoweka. Mwangaza wa jua uliifunika nchi yote kwa mng'ao wake; uso mtulivu wa ziwa ukaakisi nuru ya rangi ya dhahabu na kurudisha kama katika kioo mawingu mekundu ya asubuhi ile. Kila tumba na ua na jani la tawi likameremeta kutokana na matone ya umande. Maumbile yakatabasamu kwa mbaraka wa siku ile mpya, na ndege wakaimba nyimbo tamu kati ya miti. Mwokozi akawatazama makutano waliohudhuria mbele yake, na ndipo akaliangalia jua lililokuwa likichomoza, na kuwaambia wanafunzi wake, "Ninyi ni nuru ya ulimwengu." Kama vile jua linavyosonga mbele katika safari yake ya upendo, likivifukuzilia mbali vivuli vya usiku na kuwaamsha walimwengu wote kuanza harakati zao za maisha, ndivyo wafuasi wake Kristo wanavyopaswa kusonga mbele katika utume wao, na kuitawanya nuru ya mbinguni juu ya wale walio katika giza la upotovu na dhambi. Katika mwanga ule mkali wa asubuhi ile, miji na vijiji, vilivyokuwa juu ya vilima vile vilivyowazunguka, vilionekana wazi. Akielekeza kidole chake kule, alisema, "Mji hauwezi kusitirika ukiwa juu ya mlima." Akaendelea kusema tena, "Wala watu hawawashi taa na kuiweka chini ya pishi, bali juu ya kiango; nayo yawaangaza wote waliomo nyumbani." Wengi sana miongoni mwa wale walioyasikiliza maneno ya Yesu walikuwa ni wakulima na wavuvi, ambao nyumba zao duni zilikuwa na chumba kimoja tu, ambacho ndani yake taa moja iliyokuwa juu ya kiango chake iliwaangazia wote ndani ya nyumba ile. Hata hivyo, Yesu aliwaambia, "Vivyo hivyo nuru yenu na iangaze mbele ya watu, wapate kuyaona matendo yenu mema, wamtukuze Baba yenu aliye mbinguni."

Tangu zamani hapajakuwako na nuru nyingine yo yote iliyoangaza au itakayoangaza juu ya mwanadamu isipokuwa ni ile tu inayotoka kwa Kristo. Yesu, ambaye ni Mwokozi, ndiye nuru pekee iwezayo kuangaza katika giza la dunia hii iliyozama katika dhambi. Juu ya Kristo imeandikwa, "Ndani yake ndimo ulimokuwa uzima, nao ule uzima ulikuwa nuru ya watu." Yohana 1:4. Ilikuwa ni kwa njia ya kupokea uzima wake, wafuasi wake wangeweza kuwa wachukuzi wa nuru. Uzima wa Kristo ukiwa moyoni, upendo wake utadhihirika katika tabia, huo nd io ungewafanya wao kuwa nuru ya ulimwengu.

Wanadamu hawana nuru yo yote ndani yao wenyewe. Tukitengwa mbali na Kristo, tunafanana na mshumaa mwembamba sana ambao haujawashwa, tunafanana na mwezi wakati uso wake unaelekea mbali na jua; hatuna nuru hata kidogo ya kuangaza katika giza la dunia hii. Lakini tunapoligeukia Jua la Haki, yaani, tunapokuwa na mahusiano na Kristo, moyo wote unawaka kwa nuru ya kuwako kwake.

Wafuasi wake Kristo wanapaswa kuwa zaidi ya nuru tu kati ya watu. Wao ndio nuru yenyewe ya ulimwengu. Yesu anawaambia wale wote wanaolitaja jina lake,

Ninyi mmejitoa wenyewe kwangu mimi, nami nimewatoa kwa ulimwengu huu

kama wawakilishi wangu. Kama Baba alivyompeleka Yesu ulimwenguni, Yesu asema, “Nami vivyo hivyo [nime]watuma hao ulimwenguni.” Yohana 17:18. Kama Kristo alivyo njia ya kumfunua Baba, ndivyo nasi tunavyopaswa kuwa njia ya kumfunua Kristo. Ingawa Mwokozi wetu ndiye chimbuko kuu la nuru, usisahau, Ee Mkristo, ya kwamba yeye hufunuliwa kwa njia ya wanadamu. Mibaraka ya Mungu hutolewa kwa njia ya wanadamu. Kristo mwenyewe alikuja hapa duniani kama Mwana wa Adamu. Ubinadamu, ukiunganishwa na tabia ya uungu, unapaswa kuugusa ubinadamu. Kanisa lake Kristo, yaani, kila mfuasi mmoja mmoja wa Bwana, ni njia iliyochaguliwa na Mbingu ya kumfunua Mungu kwa wanadamu. Malaika wenye utukufu wanangoja kupitishia kwako wewe nuru ya mbinguni na uweza kwenda kwa watu walio tayari kuangamia. Je, hivi huyo mjumbe wa kibinadamu atashindwa kutimiza kazi ile aliyopangiwa? Basi, ni kwa kiwango hicho hicho walimwengu wanaporwa mvuto wa Roho Mtakatifu ulioahidiwa kwao!

Lakini Yesu hakuwaambia wanafunzi wake, “Jitahidini kuifanya nuru yenu iangaze”; bali alisema, “Nuru yenu na iangaze.” Kristo akikaa moyoni, haiwezekani kuisetiri nuru ya kuwako kwake. Endapo wale wanaojidai kuwa ni wafuasi wa Kristo hawajawa nuru ya ulimwengu, ni kwa sababu wamepotewa na uwezo wa uzima; kama hawana nuru yo yote ya kutoa, ni kwa sababu hawajaunganishwa na yule aliye Chimbuko la nuru.

Katika zama zote, “Roho wa Kristo ali(ye)kuwa ndani yao” (1 Petro 1:11), amewafanya watu wa Mungu wa kweli kuwa nuru ya watu wa vizazi vyao.Yusufu alikuwa mchukuzi wa nuru kule Misri. Kwa njia ya maisha yake safi, ukarimu wake na upendo wake kwa wazazi wake alimwakilisha Kristo kati ya taifa lile la waabudu sanamu. Waisraeli waliposafiri kutoka Misri kwenda katika Nchi ile ya Ahadi, waaminifu waliokuwa miongoni mwao walikuwa nuru kwa mataifa yaliyowazunguka. Kwa njia yao Mungu alifunuliwa kwa walimwengu. Kutoka kwa Danieli na wenzake kule Babeli, na kutoka kwa Mordekai kule Uajemi, miale ya mwanga mkali iliangaza katika giza lililokuwamo majumbani mwa wafalme wale. Vivyo hivyo wanafunzi wa Kristo wamewekwa kama wachukuzi wa nuru katika safari yao ya kwenda mbinguni; kwa njia yao rehema na fadhili za Baba hudhihirishwa kwa walimwengu waliofunikwa na giza la kuwa na picha mbaya juu ya vile Mungu alivyo. Kwa kuyaona matendo yao mema, wengine wanavutwa kumtukuza Baba aliye kule juu; kwa maana inakuwa dhahiri kwao kwamba yuko Mungu aketiye juu ya kiti cha enzi cha malimwengu ambaye tabia yake inastahili kupewa sifa na kuigwa. Upendo wa Mungu ukiwaka moyoni mwao, amani kama ile ya Kristo ikionekana katika maisha yao, kwa wanadamu wa dunia hii ni kama nafasi waliyopewa ya kuchungulia kidogo tu mbinguni, ili wapate kuuthamini uzuri usio na kifani ulioko kule.

Ni kwa njia hii watu hushawishiwa kuliamini “pendo alilo nalo Mungu kwetu sisi.” 1 Yohana 4:16. Hivyo mioyo iliyokuwa miovu na mipotovu hupata kusafishwa na kuongoka, nao husimamishwa”mbele ya utukufu wake bila mawaa katika furaha kuu.” Yuda 24.

Maneno haya ya Mwokozi, “Ninyi ni nuru ya ulimwengu,” huonesha kwamba yeye amewakabidhi wafuasi wake utume kwa ulimwengu wote. Katika siku zile za Kristo, kujipenda binafsi, na kiburi na chuki isiyo na sababu, mambo hayo yalijenga ukuta wenye nguvu na wenye kimo uliowatenga wale waliokabidhiwa mausia matakatifu ya Mungu na mataifa yale mengine ulimwenguni kote. Lakini Mwokozi alikuwa amekuja kuigeuza kabisa hali hiyo. Maneno waliyoyasikia watu kutoka kinywani mwake yalikuwa tofauti kabisa na yote waliyokuwa wameyasikia kutoka kwa makuhani au waalimu wao. Kristo hukibomoa kile kiambaza kinachowatenga watu, huuondolea mbali ule moyo wa kujipenda binafsi, na ubaguzi unaoyatenga mataifa, naye hutufundisha tuwe na upendo kwa jamaa nzima ya wanadamu. Huwatoa watu kutoka katika vikundi vyao vidogo vya kibinafsi walivyojiundia; na kuvunjilia mbali mipaka ya nchi na na tofauti walizojiwekea wanadamu katika jamii. Haweki tofauti yo yote kati ya majirani na wageni, marafiki na maadui. Anatufundisha sisi kumwangalia kila mtu mwenye shida kama jirani yetu na ulimwengu kama eneo letu la kazi.

Kama vile mishale ya jua ipenyavyo mbali pande zote za dunia, ndivyo Mungu amekusudia ya kuwa nuru ya Injili ienee kwa watu wote duniani. Kama kanisa la Kristo lingekuwa likiendelea kutimiza kusudi la Bwana wetu, nuru ingeenea na kuangaza juu ya wote wakaao gizani na katika nchi ya uvuli wa mauti. Badala ya wao kujikusanya mahali pamoja na kukwepa kuwajibika na kubeba msalaba, washiriki wa kanisa wangetawanyika na kwenda katika nchi zote, wakiacha nuru ya Kristo iangaze nje kutoka ndani yao, wakifanya kazi kama vile yeye alivyofanya kwa ajili ya wokovu wa watu, na hiyo “habari njema ya ufalme” ingepelekwa kwa kasi ulimwenguni kote.

Ni kwa njia hii kusudi la Mungu la kuwaita watu wake tangu zamani za Ibrahimu katika nyanda zile za Mesopotamia hadi siku zetu hizi litakavyotimizwa.Yeye asema, “Nitakubariki,... nawe uwe baraka.” Mwanzo 12:2. Maneno ya Kristo kupitia kwa nabii yule wa Injili, ambayo yamerudiwa tu katika mafundisho yake mlimani, yanatuhusu sisi wa kizazi hiki cha mwisho: “Ondoka, uangaze; kwa kuwa nuru yako imekuja, na utukufu wa Bwana umekuzukia.” Isaya 60:1. Ikiwa moyoni mwako umekuzukia utukufu wa Bwana; ikiwa umeutazama uzuri wake yeye aliye “mashuhuri miongoni mwa elfu kumi,” ambaye “ndiye mzuri sana pia pia;” ikiwa moyo wako umefurahi kwa kuwamo humo utukufu wake, basi, wewe ndiwe unayepelekewa neno hili la Bwana. Je, umesimama pamoja na Kristo juu

ya mlima ule wa kubadilika kwake kiutukufu? Huko chini uwandani wako watu

waliofungwa utumwani na Shetani; wanangoja kusikia neno la imani na maombi ili wapate kuwekwa huru.

Hatutakiwi tu kufikiri sana juu ya utukufu wake Kristo, bali pia juu ya kutangaza sifa zake na ubora wake. Isaya hakuona tu utukufu wa Kristo, ila pia alisema juu yake. Daudi alipowaza mambo ya Mungu, moto uliwaka ndani yake; ndipo akanena kwa ulimi wake. Alipowaza juu ya pendo la ajabu la Mungu, hakuweza kujizuia kusema habari za kile alichokiona kwa macho na kukisikia moyoni mwake. Ni nani kwa imani awezaye kuuona mpango wa ajabu wa ukombozi, yaani, utukufu wa Mwana wa Mungu wa pekee, na asiweze kuongea lo lote juu yake? Ni nani awezaye kutafakari kwa kina upendo usio na kifani uliodhihirishwa juu ya msalaba ule wa Kalvari katika kifo chake Kristo, ili sisi tusiangamie, bali tuwe na uzima wa milele—nani awezaye kuyatazama hayo, kisha akose maneno ya kusema kuutukuza utukufu huo wa Mwokozi?

“Ndani ya hekalu lake wanasema wote, Utukufu.” Zaburi 29:9. Yule mwimbaji mzuri wa Israeli alimsifu kwa kinubi, alisema, “Nitaifikiri fahari ya utukufu wa adhama yako, na matendo yako yote ya ajabu. Watu watayataja matendo yako ya kutisha; nami nitausimulia ukuu wako.” Zaburi 145:5,6.

Yapasa msalaba wa Kalvari uinuliwe juu ya watu, ili kuivuta mioyo yao na kuyakaza mawazo yao kuelekea huko. Ndipo akili ya kiroho itajazwa na nguvu itokayo kwa Mungu. Ndipo kwa kweli nguvu zote zitatumika katika kuifanya kazi ya Bwana. Watenda kazi watauangazia ulimwengu nuru yao, kama wajumbe hai wataiongoa dunia.

Kristo humkubali, naam, tena kwa furaha, kila mjumbe wa kibinadamu anayejitoa kwake. Anauunganisha ubinadamu na uungu, ili aupashe ulimwengu siri kuhusu pendo lake alipokuwa na mwili wa kibinadamu. Ongeeni juu yake, ombeni juu yake, imbeni juu yake; tangazeni kote ujumbe wa utukufu wake, tena songeni mbele kwenda katika nchi za mbali.

Kustahimili maonjo makali, kupokea mibaraka kwa moyo wa shukrani, kuyapinga kiume majaribu, kuzoea kuonesha moyo wa upole, fadhili, huruma na upendo, ndiyo nuru inayong’aa katika tabia na kuwa kinyume cha giza lililo ndani ya moyo uliojaa uchoyo, ambamo nuru ya uzima haijapata kuangaza kamwe.

## SURA YA 3

## SHERIA INAVYOYAHUSU MAMBO YA KIROHO

"Sikuja kutangua, bali kutimiliza."
Mathayo 5:17.

Alikuwa ni Kristo ambaye, katika kishindo kile cha ngurumo na umeme, alitangaza Sheria juu ya Mlima wa Sinai. Utukufu wa Mungu, ambao kuonekana kwake kulikuwa kama moto uwakao, ulikuwa juu ya mlima, na mlima wote ulitetemeka sana mbele zake Bwana. Makutano ya Waisraeli, wakiwa wamelala kifudifudi juu ya nchi, walikuwa wamesikiliza kwa kicho zilipotangazwa amri takatifu za ile Sheria. Ni tofauti iliyoje kuhusu tukio lile juu ya Mlima wa Baraka! Chini ya mbingu zile za kiangazi, bila ya kuwako sauti yo yote ya kuuvuruga utulivu ule isipokuwa tu zile nyimbo za ndege, Yesu aliwafunulia kanuni za ufalme wake. Lakini yule aliyenena na watu siku ile kwa sauti ya upendo, alikuwa akiwafunulia kanuni za ile sheria iliyotangazwa Sinai.

Sheria ilipotolewa, wale Waisraeli, wakiwa wamedhilika kwa ajili ya kukaa siku nyingi utumwani katika nchi ya Misri, walihitaji kuguswa na nguvu na utukufu wake Mungu; lakini yeye alijifunua kwao kama Mungu wa upendo.

"Bwana alitoka Sinai, Akawaondokea ktoka Seiri; Aliangaza katika kilima cha Parani, Akaja Meribath-kadeshi.

Upande wa mkono wake wa kuume Palikuwa na Sheria ya moto-moto kwao.
Hakika awapenda hayo makabila ya watu;
Watakatifu wake wote wamo mkononi mwako;
Nao waliketi miguuni pako;
Watapokea kila mmoja katika maneno yako;" Kumbukumbu la Torati 33:2,3.

Mungu alimfunulia Musa utukufu wake kwa maneno haya ya ajabu ambayo yamehesabiwa kuwa ya thamani kuu: "Bwana, Bwana Mungu, mwingi wa huruma, mwenye fadhili, si mwepesi wa hasira, mwingi wa rehema na kweli; mwenye kuwaonea huruma watu elfu elfu, mwenye kusamehe uovu na makosa na dhambi." Kutoka 34:6,7.

Sheria iliyotolewa kule Sinai ilikuwa tangazo la upendo, yaani, mafunuo ya Sheria ile ya mbinguni hapa dunia ni. Ikatolewa kwa mkono wa Mpatanishi—ikanenwa na yeye ambaye kwa uwezo wake mioyo ya wanadamu yaweza kuafikiana nayo na kufuata kanuni zake. Mungu akawa amelifunua kusudi la Sheria

alipowatangazia Israeli, akisema, “Nanyi mtakuwa watu watakatifu kwangu mimi.” Kutoka 22:31.

Lakini Waisraeli walikuwa hawajatambua hali ya kiroho ya ile Sheria; na mara nyingi kutii kwao kulikuwa kwa kufuata mambo ya kawaida tu, siyo kujitoa kwa moyo na kutawaliwa na upendo. Kadiri Yesu, katika tabia na kazi yake, alivyoonesha mbele ya wanadamu sifa za tabia yake Mungu, aliye mtakatifu, mpaji, na Baba yetu hasa, na kuonesha usivyofaa kabisa utii wa kufuata tu kawaida za dini, ndivyo kadiri ambavyo wakuu wa Wayahudi hawakuweza kuyapokea maneno yake wala kuyaelewa. Wao walidhani kwamba yeye hakuyatilia mkazo sana masharti ya Sheria; na alipowaonesha maneno ya kweli yaliyokuwa asili ya huduma yao waliyopewa na Mungu, wao wakiangalia matendo ya nje tu, wakamshtaki kuwa anataka kuitangua Sheria.

Maneno ya Kristo, ingawa yalisemwa kwa upole, yalinenwa kwa makini na kwa uwezo ulioamsha mioyo ya watu. Walisikiliza kuona kama atarudia-rudia kusema mapokeo yale yasiyo na uhai na mikazo ya waalimu juu ya utii, lakini ikawa kazi bure. “Walishangaa mno kwa mafundisho yake; kwa maana alikuwa akiwafundisha kama mtu mwenye amri, wala si kama waandishi wao.” Mathayo 7:28,29. Mafarisayo waliona tofauti kubwa mno kati ya mafundisho yao na yale ya Kristo. Waliona kwamba utukufu na usafi na uzuri wa ile kweli, pamoja na mvuto wake mpole uingiao mpaka ndani, ulikuwa ukiigusa sana mioyo ya watu wengi. Upendo wa Mwokozi na huruma zake zikaivuta mioyo ya watu kwake. Waalimu wale waliona kwamba mafundisho yake yalikuwa yameubatilisha kabisa mfumo wa mafundisho yao waliyokuwa wamewafundisha watu. Alikuwa akikibomoa kiambaza kile kilichowatenga na wengine ambacho kiliwatia kiburi kingi mno na kuwafanya wajitenge na wengine; nao wakaogopa kwamba, endapo wakimwacha aendelee vile, angeweza kuwavuta watu wote kwenda mbali nao. Kwa hiyo, walimwandama kwa nia ya chuki, wakitumaini kupata sababu ya kuwafanya makutano wamchukie, na hivyo kuliwezesha Baraza Kuu la Wayahudi (Sanhedrin) kumhukumu na kumwua.

Pale mlimani, Yesu alichunguzwa sana na majasusi; naye alipokuwa akizifafanua kanuni za haki, Mafarisayo wakaanzisha minong’ono kwamba mafundisho yake yalikuwa kinyume na maagizo ya Mungu aliyoyatoa katika mlima Sinai. Mwokozi hakusema neno lo lote la kuwatia watu wasiwasi juu ya dini na sheria iliyotolewa na Musa; kwa kuwa mafundisho yale yote ambayo yule kiongozi mkuu wa Waisraeli aliwapa watu wale yalikuwa nuru aliyoipokea kutoka kwa Kristo. Wakati wengi huendelea kusema mioyoni mwao kuwa alikuja kuitangua sheria, Yesu kwa lugha isiyoweza kukosa kueleweka anaonesha mwelekeo wake huu kuhusu hizo amri za Mungu. “Msidhani,” akasema, “nalikuja kuitangua torati au

manabii.”

Muumbaji wa wanadamu, Mtoaji wa torati, ndiye asemaye kwamba si kusudi lake kuyabatilisha maagizo yake. Kila kitu kilicho katika maumbile, kuanzia mwale mdogo sana wa jua hadi kwenye malimwengu yaliyoko huko juu, kiko chini ya sheria. Na utaratibu na ulinganifu wa viumbe na vitu vya dunia hutegemea juu ya kuzitii sheria hizi. Hivyo kuna kanuni kuu za haki zinazoongoza maisha ya viumbe vyote vyenye akili, na usitawi wa malimwengu hutegemea kuzitii kanuni hizi. Kabla ya dunia hii kuumbwa, sheria ya Mungu ilikuwako. Malaika huongozwa na kanuni zake, na ili dunia hii ipate kuafikiana na Mbingu, mwanadamu pia hana budi kuzishika sheria za Mungu. Amri za sheria hii zilijulishwa kwa mwanadamu na Kristo katika Edeni "hapo nyota za asubuhi zilipoimba pamoja, na wana wote wa Mungu walipopiga kelele kwa furaha." Ayubu 38:7. Kazi aliyokuja kufanya Kristo duniani haikuwa kuitangua sheria bali kwa Neema yake kumrejesha mwanadamu katika ut ii wa sheria yake.

Mwanafunzi huyu mpendwa, aliyesikiliza maneno ya Yesu mlimani, baada ya miaka mingi akiandika kwa kuongozwa na Roho Mtakatifu, anasema juu ya sheria hii kuwa ni kanuni ya daima inayotufunga sisi. Yeye anasema kwamba "dhambi ni uvunjaji wa sheria" na kwamba "Kila atendaye dhambi anavunja sheria ya Mungu." 1 Yohana 3:4, AJKK/HN. Anadhihirisha kwamba sheria anayoisema ndiyo ile "amri ya zamani mliyokuwa nayo tangu mwanzo." 1 Yohana 2:7. Anasema juu ya sheria ile iliyokuwako wakati wa uumbaji na ambayo ilitangazwa tena juu ya Mlima Sinai.

Akisema juu ya sheria, Yesu alisema, "Sikuja kutangua, bali kutimiliza." Hapo alilitumia neno hili "kutimiliza" kwa maana ile ile aliyomwambia Yohana Mbatizaji ya kwamba kusudi lake lilikuwa ni "kuitimiza haki yote" (Mathayo 3:15); yaani, kutosheleza matakwa yote ya sheria, kutoa kielelezo cha utii kamili kwa mapenzi yake Mungu.

Utume wake ulikuwa ni "kuitukuza sheria, na kuiadhimisha." Isaya 42:21. Alipaswa kuonesha hali ya kiroho ya ile sheria, kuelezea kanuni zake pana sana, na kufafanua masharti yake yanayotufunga milele.

Mvuto wa tabia takatifu ya Kristo, ambaye tabia ya mwanadamu iliyo nzuri sana na adilifu kabisa huiakisi kwa kiwango hafifu tu; ambaye Sulemani, akiongozwa na Roho, alivuviwa kua ndika juu yake ya kwamba yeye yu "Mashuhuri miongoni mwa elfu kumi,… ndiye mzuri sana pia pia" (Wimbo ulio Bora 5:10-16), ambaye Daudi, alipomwona katika maono, alisema hivi juu yake, "Wewe u mzuri sana kuliko wanadamu" (Zaburi 45:2), Yesu, chapa ya nafsi yake, na mng'ao wa utukufu wake; Mkombozi wetu anayejikana nafsi yake, katika kipindi chote cha safari yake ya kuishi hapa duniani kwa upendo, aliiwakilisha tabia ya upendo

sheria ya Mungu. Katika maisha yake imedhihirishwa ya kwamba upendo ule

utokao kwa Mungu, yaani, zile kanuni za Kikristo, ndizo msingi wa sheria za maadili ya milele.

“Mpaka mbingu na nchi zitakapoondoka,” alisema Yesu, “yodi moja wala nukta moja ya torati haitaondoka, hata yote yatimie.” Kwa utii wake yeye mwenyewe kwa zile sheria, Kristo alishuhudia juu ya asili yake isiyobadilika milele na kuthibitisha kwamba kwa neema yake kila mwana na binti yake Adamu angeweza kuitii kwa ukamilifu. Pale mlimani alitangaza kuwa hata sehemu ndogo sana ya torati haitaondoka mpaka yote yatimie,—mambo yote yanayowahusu wanadamu, yote yahusuyo ule mpango wa ukombozi. Yeye hafundishi kwamba ile sheria itabatilika kwa wakati wo wote ujao, bali yeye anakaza macho yake kupita upeo wa macho ya mwanadamu na kutuhakikishia sisi kwamba mpaka upeo ule utakapofikiwa sheria itaendelea kuwa na mamlaka yake ili asiwepo hata mmoja anayedhani kwamba ilikuwa ni kazi yake kuja kuzifutilia mbali amri za sheria hiyo. Kadiri mbingu na dunia zinavyoendelea kuwako, ndivyo kanuni takatifu za sheria ya Mungu zitakavyodumu. Haki yake, “kama milima ya Mungu” (Zaburi 36:6) itadumu na kuwa chimbuko la baraka, ikivitawanya vijito vyake ili kuiburudisha nchi.

Kwa kuwa sheria ya Bwana ni kamilifu, na kwa ajili hiyo haibadiliki kamwe, haiwezekani kwa wanadamu wenye dhambi, kwa nguvu zao wenyewe, kukifikia kipeo cha matakwa yake. Hiyo ndiyo sababu ya kuja kwake Yesu kuwa Mkombozi wetu. Ilikuwa ni kazi yake kuwapatanisha wanadamu ili wapate kuwa washirika wa tabia ya uungu, yaani, kuwaleta katika hali ya kupatana na kanuni za sheria hiyo ya mbinguni. Tukiacha dhambi zetu na kumkubali Kristo kuwa Mwokozi wetu, sheria hiyo hutukuzwa. Mtume Paulo auliza, “Basi, je! twaibatilisha sheria kwa imani hiyo? Hasha! Kinyume cha hayo twaithibitisha sheria.” Warumi 3:31.

Ahadi ya agano jipya ni hii: “Nitatia sheria zangu mioyoni mwao, na katika nia zao nitaziandika.” Waebrania 10:16. Kawaida za ibada za zamani zilizokuwa kivuli, ambazo zilimwelekea Kristo, Mwana-Kondoo wa Mungu, ambaye huichukua dhambi ya ulimwengu, zilipaswa kukoma wakati wa kufa kwake; lakini kanuni za haki ambazo zimefungamana na Amri Kumi za Mungu, hazibadiliki kamwe kama kilivyo kiti chake cha enzi kidumucho milele. Hakuna amri hata moja iliyotanguka, hakuna yodi moja wala nukta moja iliyobadilika. Kanuni zile zilizojulishwa kwa mwanadamu katika Bustani ya Edeni kuwa ndizo sheria kuu za uzima, zitaendelea kuwako bila kubadilika hata katika Edeni mpya itakayorejeshwa. Edeni itakapong’aa tena kwa maua yake ya kupendeza hapa duniani, Sheria ya Mungu ya upendo wataitii wote walio chini ya jua.

“Ee Bwana, neno lako lasimama imara mbinguni hata milele.” “Maagizo yako yote ni amani. Yamethibitika milele na milele, yamefanywa katika kweli na adili.” “Zamani nimejua kwa shuhuda zako ya kuwa umeziweka zikae milele.” Zaburi 119:89; 111:7,8; 119:152.

“Mtu ye yote atakayevunja Amri Moja Katika hizi Zilizo Ndogo, na Kuwafundisha Watu Hivyo, ataitwa Mdogo Kabisa Katika Ufalme wa Mbinguni”
Mathayo 5:19.

Yaani, hatakuwa na mahali kule. Kwa maana yule anayevunja amri moja kwa makusudi, haitunzi yo yote katika hizo katika roho na kweli. “Maana mtu awaye yote atakayeshika sheria yote, ila akajikwaa katika neno moja, amekosa juu ya yote.” Yakobo 2:10.

Si ukubwa wa tendo la kutomtii Mungu unaolifanya kuwa dhambi; bali ni ukweli wa kwenda kinyume na mapenzi ya Mungu yaliyofunuliwa katika jambo lo lote lililo dogo sana; kwani huko hudhihirisha kwamba kungaliko na ushirika kati ya mtu huyo na dhambi. Moyo umegawanyika katika utumishi wake. Kwa kweli kuna kumkana Mungu, yaani, uasi dhidi ya sheria za serikali yake.

Kama wanadamu wangekuwa huru kuacha kufanya matakwa ya Mungu na kujiwekea kanuni zao wenyewe za uwajibikaji, kungekuwako na kanuni zinazohitilafiana ili kuwapendeza watu wenye mawazo mbalimbali na serikali ingeporwa kutoka katika mikono yake Bwana. Nia ya mwanadamu ingetawala kabisa, na mapenzi makuu na matakatifu ya Mungu—yaani, kusudi lake la upendo kwa viumbe vyake—yangedharauliwa, yasingeheshimiwa.

Wakati wo wote wanadamu wanapochagua kuifuata njia yao wenyewe, wanajiweka katika mashindano na Mungu. Hawatakuwa na sehemu yo yote katika ufalme wa mbinguni, kwa maana wanazipiga vita kanuni halisi za mbinguni. Kwa kutoyajali mapenzi ya Mungu, wanajiweka wenyewe upande wa Shetani, adui wa Mungu na wa wanadamu. Mtu ataishi, si kwa neno moja tu la Mungu, wala si kwa maneno mengi, bali kwa kila neno litokalo katika kinywa cha Mungu. Hatuwezi kuacha kulijali neno lo lote la Mungu, haidhuru lionekane kwetu kuwa ni dogo sana jinsi gani, na kuwa salama. Hakuna amri iwayo yote ya ile sheria ambayo si kwa manufaa na furaha ya mwanadamu, katika maisha haya na katika maisha yale yajayo. Katika kuitii sheria ya Mungu, mwanadamu anazungukwa pande zote na uzio, na kulindwa asipatikane na maovu. Yeye auvunjaye uzio huo uliojengwa na Mungu mahali pamoja tu ameharibu uwezo wake unaomlinda; kwani amefungua njia ambayo kwayo yule adui anaweza kuingia ili kumharibu na kumwangamiza.

Kwa kuthubutu kuacha kuyajali mapenzi ya Mungu katika jambo moja tu, wazazi wetu wale wa kwanza walifungua milango ya mafuriko ya taabu na huzuni juu ya dunia hii. Na kila mtu anayefuata mfano wao atavuna matokeo yale yale. Upendo wa Mungu ndio msingi wa kila amri ya sheria yake, na mtu yule anayeiacha amri anajiletea mwenyewe uchungu na maangamizi.

“Haki Yenu Isipozidi Hiyo Haki ya Waandishi na Mafarisayo, Hamtaingia Kamwe Katika Ufalme wa Mbinguni.” Mathayo 5:20.

Waandishi na Mafarisayo walikuwa hawajamshtaki Kristo tu bali pia wanafunzi wake kuwa ni wenye dhambi kwa kuwa hawakuzijali kawaida za ibada na kanuni za Kiyahudi. Mara kwa mara wanafunzi wake walikuwa wakishikwa na fadhaa na kutaabika moyoni kwa ajili ya kulaumiwa na kushtakiwa na wale ambao walikuwa wamezoea kuwaheshimu kama waalimu wakuu wa dini. Yesu aliifichua hila yao. Alisema kwamba haki ya Mafarisayo ambayo waliithamini mno ilikuwa haifai kitu. Wayahudi walikuwa wamejidai kuwa ni watiifu na wateule wa Mungu; bali Kristo alionesha kuwa dini yao ilikuwa haina imani inayookoa watu. Kujidai kwao kote kuwa wao ni watauwa, pamoja na mavumbuzi yao ya kibinadamu na kawaida zao za dini, na hata kujitapa kwao kuhusu matendo yao ya nje kuhusiana na ile sheria, hayo yote yasingeweza kufaa kuwafanya wawe watakatifu. Hawakuwa safi mioyoni mwao, wala kuwa na tabia njema, wala kuwa kama Kristo katika tabia zao.

Dini inayofuata matendo ya sheria ya nje tu haitoshi kumpatanisha mtu huyo na Mungu. Ugumu na msimamo mkali wa imani ya Mafarisayo, ambao hawakuwa na toba, upole, wala upendo, kilikuwa ni kikwazo kikubwa kwa wenye dhambi. Walikuwa kama chumvi iliyopoteza ladha yake; kwa vile mvuto wao haukuwa na uwezo wa kuuhifadhi ulimwengu usiharibike. Imani ya kweli peke yake ni ile “itendayo kazi kwa upendo” (Wagalatia 5:6) kwa kumtakasa mtu. Hiyo ni kama chachu inayoibadilisha tabia.

Iliwapasa Wayahudi kujua hayo yote kutokana na mafundisho ya manabii. Karne nyingi kabla, kilio cha mtu kwa ajili ya kuhesabiwa haki na Mungu, kilipata sauti na jibu lake katika maneno haya aliyosema nabii Mika, “Nimkaribie Bwana na kitu gani, na kuinama mbele za Mungu aliye juu? Je, nimkaribie na sadaka za kuteketezwa, na ndama za umri wa mwaka mmoja? Je, Bwana atapendezwa na elfu za kondoo waume, au elfu kumi za mito ya mafuta? … Ee mwanadamu amekuonesha yaliyo mema; na Bwana anataka nini kwako, ila kutenda haki, na kupenda rehema, na kwenda kwa unyenyekevu na Mungu wako.” Mika 6:6-8.

Nabii Hosea alikuwa ameonesha jambo ambalo ni asili ya unafiki wa Mafarisayo,

kwa maneno haya, “Israeli ni mzabibu mtupu, anazaa matunda kwa ajili yake

mwenyewe". Hosea 10:1 (KJV). Katika kujidai kwao kwamba walikuwa wakimtumikia Mungu, kwa kweli Wayahudi walizitumikia nafsi zao wenyewe. Haki yao ilikuwa tunda la kujitahidi kwao kushika sheria kwa jinsi walivyoona wenyewe, na kwa manufaa yao wenyewe. Hivyo haik uwa bora kuliko vile walivyokuwa wenyewe. Katika kujitahidi kujifanya wenyewe kuwa watakatifu, walikuwa wakijaribu kutoa kitu safi toka kitu kichafu. Sheria ya Mungu ni takatifu kama Yeye alivyo mtakatifu, ni kamilifu kama Yeye alivyo mkamilifu. Inawaonesha wanadamu haki ya Mungu. Mwanadamu, kwa uwezo wake mwenyewe, hawezi kamwe kuishika sheria hii; kwani mwanadamu, kwa asili yake, ni mpotovu, mwenye kombo, hafanani kabisa na tabia ya Mungu. Matendo ya moyo wenye kujipendeza nafsi wenyewe bila kuwajali wengine ni kama "kitu kilicho kichafu;" na "matendo yetu yote ya haki yamekuwa kama nguo iliyotiwa unajisi." Isaya 64:6.

Maadam sheria ni takatifu, Wayahudi wasingeweza kupata haki kwa kujitahidi kwao wenyewe kuishika sheria. Wanafunzi wa Kristo hawana budi kupata haki inayohitilafiana na haki ya Mafarisayo, endapo wanataka kuingia katika ufalme wa mbinguni. Katika Mwana wake, Mungu aliwapa haki ya sheria iliyo kamilifu. Kama wangefungua mioyo yao kabisa na kumpokea Kristo, ndipo uzima halisi wa Mungu, upendo wake, ungekaa ndani yao, na kuwageuza ili wawe katika mfano wake; na hivyo kwa njia ya kukipokea kipawa cha Mungu cha bure, wangepata ile haki inayotakiwa na sheria ya Mungu. Lakini Mafarisayo walimkataa Kristo; "kwa maana wakiwa hawajui haki ya Mungu, na wakitaka kuithibitisha haki yao wenyewe, hawakujitia chini ya haki ya Mungu." Warumi 10:3.

Yesu akaendelea kuwaonesha wasikilizaji wake maana hasa ya kuzishika amri za Mungu, —ya kwamba ni kuwa na tabia ile ile ya Kristo ndani yao. Maana katika yeye, Mungu alidhihirishwa mbele yao siku zote.

Kila Amwoneaye Ndugu Yake Hasira, Itampasa Hukumu."
Mathayo 5:22.

Kwa kinywa cha Musa, Bwana alikuwa amesema, "Usimchukie ndugu yako moyoni mwako; … Usifanye kisasi, wala kuwa na kinyongo juu ya wana wa watu wako, bali umpende jirani yako kama nafsi yako." Mambo ya Walawi 19:27,18. Kweli alizozifundisha Kristo zilikuwa ni zile zile zilizokuwa zimefundishwa na manabii, lakini maana yake ilikuwa imetiwa giza kutokana na ugumu wa moyo na kupenda dhambi.

Maneno ya Mwokozi yaliwadhihirishia wasikilizaji wake ukweli kwamba wakati walipokuwa wakiwahukumu wengine kuwa ni wakosaji, wao wenyewe walikuwa

wenye dhambi kama wale; kwani walikuwa na moyo wa kutaka kuwadhuru wengine na chuki.

Ng'ambo ya pili ya bahari kutoka mahali walipokusanyika, ilikuwa nchi ya Bashani, mahali pa ukiwa ambapo tangu zamani magenge yake na vilima vyenye misitu vilikuwa maficho ya wabaya wa kila aina wenye kuhalifu sheria. Taarifa za ujambazi na mauaji yaliyotendeka kule zilikuwa zingali mpya katika mawazo ya watu wale, na wengi wao walikuwa na hamaki kuwalaumu wale waovu. Huku wao wenyewe walikuwa wakali na wakaidi; waliwachukia sana Warumi waliowadhulumu, na kuona kwamba wameruhusiwa kuwachukia na kuwadharau wengine wote, hata watu wa taifa lao wenyewe wasiopatana nao katika mambo yao yote. Na kwa haya yote walikuwa wakivunja amri isemayo, "Usiue."

Roho ya chuki na kulipiza kisasi ilianzishwa na Shetani, hata ikamwongoza kumwua Mwana wa Mungu. Ye yote anayekuwa na nia ya kudhuru wengine na ukali, ana moyo ule ule; na matunda yake ni mauti. Katika wazo la kulipiza kisasi tendo baya hujificha, kama mmea unavyojificha katika mbegu. "Kila amchukiaye ndugu yake ni mwuaji: nanyi mnajua ya kuwa mwuaji hana uzima wa milele ukikaa ndani yake." 1 Yohana 3:15.

"Mtu akimfyolea ndugu yake, itampasa baraza." Katika kumtoa Mwanawe kwa ajili ya wokovu wetu, Mungu ameonesha jinsi anavyomthamini sana kila mwanadamu machoni pake, naye hamruhusu mtu awaye yote kumbeua mwenziwe. Twaweza kuona makosa na udhaifu wa wenzetu wanaotuzunguka, lakini Mungu amemhesabu kila mtu kuwa mali yake, —mali yake kwa sababu alimwumba, pia amekuwa mali yake mara ya pili kwa kuwa amemkomboa kwa damu ya Kristo yenye thamani. Wote waliumbwa kwa mfano wake Mungu, na hata watu duni wana haki kustahiwa na kuhurumiwa. Mungu atatuhesabia kuwa tunawajibika kwa kila neno la dharau au la kubeua lisemwalo juu ya mtu awaye yote ambaye Kristo aliutoa uhai wake kwa ajili yake.

"Maana ni nani anayekupambanua na mwingine? Nawe una nini usichokipokea, wajisifia nini kana kwamba hukupokea?" "Wewe u nani unayemhukumu mtumishi wa mwingine? Kwa bwana wake mwenyewe yeye husimama au huanguka." 1 Wakorintho 4:7; Warumi 14:4.

"Na mtu akimwapiza, itampasa jehanum ya moto." Katika Agano la Kale neno hili "mpumbavu" linatumika kuonesha mwenye kuasi, ama mtu anayejitia katika kufanya maovu. Yesu asema kwamba mtu ye yote atakayemhukumu mwenzake kuwa ni mwasi ama kama ni mtu anayemdharau Mungu, hujionesha mwenyewe kuwa amestahili ye ye mwenyewe hukumu hiyo hiyo.

Kristo mwenyewe, “aliposhindana na Ibilisi, na kuhojiana naye kwa ajili ya mwili wa Musa, hakuthubutu kumshtaki kwa kumlaumu.” Yuda 9. Kama angalifanya hivyo, angalijitia upande wa Shetani; kwani mashtaka na lawama ndizo silaha za yule mwovu. Katika Maandiko ameitwa jina lake “mshtaki wa ndugu zetu.” Ufunuo 12:10. Na Yesu asingalitumia silaha yo yote ya Shetani. Alisema tu, “Bwana na akukemee.” Yuda 9.

Mfano wake ni kwa ajili yetu. Kama tumeingizwa katika kushindana na adui za Kristo, inatupasa tusiseme neno lo lote la kurudisha ukali kwa ukali, ama neno linaloonekana kuwa ni neno la lawama. Yeye asimamaye kama mnenaji wa Mungu haimpasi kunena maneno ambayo Mfalme wa mbinguni asingeyatumia katika kushindana na Shetani. Yatupasa kumwachia Mungu kazi ya kuhukumu na kutoa lawama.

Upatane Kwanza na Ndugu Yako.” Mathayo 5:24.

Upendo wa Mungu ni kitu kilicho zaidi ya kukanusha mabaya tu; ni kanuni ijengayo na kutenda kazi, ni chemchemi ya maji ya uzima, ibubujikayo daima kuwaletea mibaraka wengine. Upendo wa Kristo ukiwamo ndani yetu, hatutakuwa na moyo wa kuwachukia wengine tu, bali tutajaribu kwa njia zote kudhihirisha jinsi tuwapendavyo.

Yesu alisema, “Basi ukileta sadaka yako madhabahuni, na huku ukikumbuka ya kuwa nd ugu yako ana neno juu yako, iache sadaka yako mbele ya madhabahu, uende zako, upatane kwanza na ndugu yako, kisha urudi uitoe sadaka yako.” Dhabihu zilionesha imani ya mwenye kutoa kafara kwamba katika Kristo amekuwa mshiriki wa rehema na upendo wa Mungu. Lakini kwa mtu kuonesha imani katika upendo wa Mungu unaosamehe dhambi, na huku yeye mwenyewe akiwa na moyo usio na upendo, kwake ungekuwa ni upuzi mtupu.

Mtu ye yote anayejidai kuwa anamcha Mungu, akimkosea au kumdhuru ndugu mwenziwe, anamweleza huyo nd uguye vibaya namna tabia ya Mungu ilivyo; inampasa kuungama kosa lake, na kukiri kwamba ametenda dhambi, ndipo ataweza kuafikiana na Mungu. Huenda ndugu yetu akawa ametutendea kosa kubwa kuliko sisi tulivyomtendea, lakini hilo halipunguzi uwajibikaji wetu. Tunapomjia Mungu, na huku tunakumbuka kwamba mtu fulani ana neno juu yetu, tumepaswa kuiacha sadaka yetu ya sala, ya shukrani, ya sadaka ya hiari, na kwenda kwake yule ndugu tusiyepatana naye, na kwa unyenyekevu wa moyo tukiri kosa letu na kumwomba msamaha.

Ikiwa tumemdanganya mwenzetu ama kumdhuru kwa njia yo yote, hatuna budi

kumlipa. Ikiwa tumemshuhudia mtu uongo bila kujua, au ikiwa tumekosea katika

kuyaeleza maneno yake jinsi yalivyo hasa, ikiwa tumeharibu sifa yake kwa wengine, inatupasa kwenda kwa wale tulioongea nao juu yake, na kubatilisha yote tuliyoyasema ambayo si ya kweli.

Laiti kama mambo mazito baina ya ndugu yasingaliwekwa wazi mbele ya wengine, bali wao wenyewe wangeyazungumzia kwa kweli na kwa moyo wa upendo wa Kikristo, maovu mengi kama nini yangalizuiwa! Mashina mengi kama nini ya uchungu ambayo watu wengi hutiwa unajisi kwayo, yangeharibiwa mapema, na wafuasi wa Kristo wangezidi kuwa na huruma kama nini na kuungana pamoja katika upendo wake!

“Kila Mtu Atazamaye Mwanamke kwa Kumtamani, Amekwisha Kuzini Naye Moyoni Mwake.” Mathayo 5:28.

Wayahudi walijivuna juu ya uadilifu wao, na kuangalia kwa chuki matendo ya uasherati ya mataifa. Kuwako kwa wakuu wa Rumi, ambao utawala wa dola ile ulikuwa umewaleta Palestina, lilikuwa ni chukizo la kudumu kwa watu, kwani wageni hawa walikuwa wameingiza desturi nyingi za mataifa, tamaa mbaya za mwili na ufisadi. Huko Kapernaumu, maafisa wa Kirumi wakiwa pamoja na hawara zao wafisadi mara kwa mara walipenda kuandamana nao na kwenda matembezini, na mara nyingi kelele za furaha kubwa zilisikika katika utulivu wa ziwani, vyombo vyao vya anasa vilipopita mbio kwa mwendo laini juu ya maji yale matulivu. Watu walitazamia kwamba Yesu angewashutumu watu wale kwa ukali; lakini, walishangaa kama nini kuyasikia maneno yale yaliyofunua maovu ya mioyo yao wenyewe!

Kufikiri maovu kukipendwa na kutunzwa moyoni, ingawa kwa siri sana, alisema Yesu, kunaonesha kuwa dhambi bado ingali inatawala moyoni. Moyo huo ungali bado “katika uchungu kama nyongo, na tena u katika kifungo cha uovu.” Matendo 8:23. Yeye anayependa kufikiri sana juu ya mambo yasiyo safi, anayefurahia kufikiri maovu, na kutazama kwa tamaa, anaweza kuona asili hasa ya maovu anayoyaficha moyoni mwake katika dhambi hiyo iliyo dhahiri, yenye mzigo wake wa aibu na huzuni inayouvunja moyo. Wakati wa jaribu, ambapo mtu huenda anaanguka katika dhambi mbaya sana, huo si chanzo cha maovu yanayofunuliwa, ila huyaendeleza au huyadhihirisha tu yale yaliyokuwa yamefichwa ndani ya moyo wake. “Maana aonavyo nafsini mwake, ndivyo alivyo;” kwani moyoni “ndiko zitokako chemchemi za uzima.” Mithali 23:7; 4:23.

“Mkono Wako wa Kuume Ukikukosesha, Ukate Uutupe Mbali Nawe.”
Mathayo 5:30.

Ili kuzuia ugonjwa usienee mwilini mwote na kuangamiza maisha, mtu angekubali hata kuachana na mkono wake wa kulia. Licha ya kufanya hivyo hata inampasa kukubali kutengana na cho chote ambacho kingeyahatirisha maisha yake ya kiroho.

Kwa njia ya injili, watu ambao wamepoteza heshima yao na kufanywa na Shetani kuwa watumwa hawana budi kukombolewa ili wapate kushiriki katika uhuru wa utukufu wa watoto wa Mungu. Kusudi la Mungu sio tu kukomboa kutoka katika mateso ambayo ni matokeo yasiyoepukika ya dhambi, bali ni kuokoa kutoka katika dhambi yenyewe. Nafsi iliyochafuliwa na kuumbuliwa, inapaswa kutakaswa, kubadilishwa, ili iweze kuvikwa "uzuri wa Bwana, Mungu wetu," i"fananishwe na mfano wa Mwana wake." "Jicho halikuyaona wala sikio halikuyasikia, wala hayakuingia katika moyo wa mwanadamu, mambo ambayo Mungu aliwaandalia wampendao." Zaburi 90:17; Warumi 8:29; 1 Wakorintho 2:9. Umilele peke yake unaweza kudhihirisha hatima tukufu ambayo mwanadamu, aliyerejeshwa katika mfano wa Mungu, anaweza kuifikia.

Ili sisi tuweze kulifikia lengo hili la juu, kile kinachomfanya mtu ajikwae ni lazima kitupiliwe mbali kabisa. Ni kwa njia ya nia yetu dhambi inapata nguvu yake ya kutushika. Kuisalimisha hiyo nia huwakilishwa kama kung'oa jicho na kulitupa mbali au kuukata mkono na kuutupa mbali. Mara nyingi kwetu sisi inaonekana kana kwamba kule kuisalimisha nia yetu kwa Mungu ni sawa na kukubali kuishi maisha yetu kama vilema au viwete. Lakini ni heri, asema Kristo, nafsi yetu iwe kilema, ijeruhiwe, iwe kiwete, endapo kwa njia hiyo wewe unaweza kuingia katika uzima. Kile ambacho wewe unakiona kama maafa ni mlango wa kuingilia katika faida kubwa sana.

Mungu ndiye chemchemi ya uzima, na sisi tunaweza kuwa na uzima tu tunaposhirikiana naye. Tukitengwa mbali na Mungu, uhai wetu unaweza kuendelea kwa kitambo kidogo tu, lakini sisi hatuna uzima ndani yetu. "Bali yeye asiyejizuia nafsi yake amekufa ingawa yu hai." 1 Timotheo 5:6. Ni kwa njia tu ya kuisalimisha nafsi yetu kwa Mungu uwezekano wa Yeye kutupa uzima upo. Ni kwa kuupokea uzima wake kwa njia ya kujisalimisha nafsi zetu, alisema Yesu, uwezekano upo wa kuzishinda dhambi hizi zilizojificha, ambazo nimezielezea. Pengine mnaweza kuzificha mioyoni mwenu na kuzisetiri zisionekane kwa macho ya kibinadamu, lakini, mtasimamaje mbele za Mungu?

Kama ukiing'ang'ania nafsi yako, na kukataa kuisalimisha nia yako kwa Mungu, unachagua kufa. Po pote dhambi inapopatikana, Mungu ni moto ulao. Ukichagua dhambi, na kukataa kutengana nayo, basi, kuwako kwake Mungu, kuiteketezako dhambi, kutakuteketeza wewe pia.

Itahitaji kujitoa mhanga ili kujitoa wenyewe kwa Mungu; lakini ni kujitoa mhanga kwa mambo yaliyo duni zaidi kwa ajili ya yale yaliyo ya juu zaidi, kuacha ya kidunia kwa yale ya kiroho, kuacha yaharibikayo kwa yale yadumuyo milele. Si kusudi la Mungu kuziharibu nia zetu; kwa kuwa ni kwa kuzitumia tu tunaweza kutimiza yale ambayo Yeye angetaka tufanye. Nia yetu haina budi kutolewa kwake ili tuipate tena, ikiisha kusafishwa na kuadilishwa na kuwa katika hali ya kushirikiana na Mungu, hata aweze kututumia kama njia ya kupitishia upendo wake na uwezo wake. Hata hivyo, haidhuru kujisalimisha huko kuonekane kuwa ni kuchungu na kunakoleta maumivu makali jinsi gani kwa moyo wako ulio mkaidi, unaofuata njia zake wenyewe, lakini huko ndiko “kunakufaa wewe.”

Mpaka hapo alipoanguka kifuani pa yule malaika wa agano na kuwa kilema na kupoteza nguvu zake zote, ndipo Yakobo alipoufahamu ushindi wa imani ishindayo na kupokea cheo cha mkuu aliyeshindana na Mungu. Ilikuwa ni wakati ule alipo“chechemea kwa sababu ya paja la mguu wake” (Mwanzo 32:31), vikosi vya vita vya Esau vilipotulia mbele yake, na yule Farao, mrithi mwenye majivuno katika mbari ya kifalme, alipoinama chini na kutamani sana apewe mbaraka wake. Hivyo ndivyo Kapiteni wa wokovu wetu alivyokamilishwa kwa njia ya mateso (Waebrania 2:10), na watoto wa imani “walitiwa nguvu baada ya kuwa dhaifu, walikuwa hodari katika vita, walikimbiza majeshi ya wageni.” Waebrania 11:34. Hivyo “wachechemeao walipata mateka” (Isaya 33:23), aliye dhaifu “atakuwa kama Daudi, nayo nyumba ya Daudi … kama malaika wa Bwana.” Zekaria 12:8.

“Je, ni Halali Mtu Kumwacha Mkewe?” Mathayo 19:3.

Miongoni mwa Wayahudi mtu aliruhusiwa kumwacha mkewe kwa makosa madogo sana yasiyokuwa na maana, na hapo mwanamke alikuwa na nafasi ya kuolewa tena. Tendo hili lilileta maovu mengi sana na dhambi. Katika mahubiri yale mlimani, Yesu alisema dhahiri kwamba kifungo cha ndoa hakiwezi kukatika ila kwa sababu ya uzinzi. Alisema, “Kila mtu amwachaye mkewe, isipokuwa kwa habari ya uasherati, amfanya kuwa mzinzi; na mtu akimwoa yule aliyeachwa, azini.”

Mafarisayo walipomhoji baadaye juu ya uhalali wa talaka, Yesu aliwaelekeza wasikilizaji wake nyuma ilipoanzishwa ndoa wakati wa uumbaji. Akasema, “Musa, kwa sababu ya ugumu wa mioyo yenu, aliwapa ruhusa kuwaacha wake zenu; lakini tangu mwanzo haikuwa hivi.” Mathayo 19:8. Akawaelekeza kwenye siku zile za heri kule Edeni, Mungu alipoona kila kitu alichokifanya kuwa ni “chema sana.” Wakati ule ndipo ndoa na Sabato zilipoanzishwa, taasisi pacha kwa ajili ya utukufu wake Mungu kwa manufaa ya binadamu. Ndipo Mwumbaji

alipowaunganisha katika ndoa mume na mke wa kwanza, alisema: “Mwanamume

atamwacha baba yake na mama yake, naye ataambatana na mkewe: nao watakuwa mwili mmoja” (Mwanzo 2:24); kwa maneno haya alitangaza sheria ya ndoa kwa wanadamu wote mpaka mwisho wa dunia. Kile ambacho Baba wa zamani zote alikitangaza kuwa ni chema, kilikuwa sheria iliyowaletea wanadamu mbaraka mkubwa sana na maendeleo.

Kama vile kilivyo kila kipaji chema cha Mungu alichowakabidhi binadamu kukitunza, ndoa nayo imepotoshwa kwa dhambi; lakini ni kusudi la Injili kuirejeshea hali yake ya usafi na uzuri kama ilivyokuwa mara ya kwanza. Katika Agano la Kale na Agano Jipya kifungo cha ndoa kinawakilisha fungamano la upendo na usafi baina ya Kristo na watu wake, yaani, wale waliokombolewa, ambao amewanunua kwa gharama ya Kalvari. “Usiogope; ... kwa sababu Muumba wako ni mume wako; Bwana wa majeshi ndilo jina lake; na Mtakatifu wa Israeli ndiye Mkombozi wako.” “Rudini, enyi watoto wenye kuasi, asema Bwana; maana mimi ni mume wenu.” Isaya 54:4,5; Yeremia 3:14. Katika Wimbo Ulio Bora twamsikia bibi arusi akisema, “Mpendwa wangu ni wangu, na mimi ni wake.” “Mpendwa wangu… mashuhuri miongoni mwa elfu kumi.” Naye Bwana amwambia mteule wake, “Mpendwa wangu u mzuri pia pia; ndani yako hamna ila.” Wimbo Ulio Bora 2:16; 5:10; 4:7.

Katika nyakati za baadaye, mtume Paulo alipowaandikia Wakristo wa Efeso, alitangaza kwamba Bwana amemweka mume kuwa kichwa cha mke, mlinzi wake, na kifungo cha nyumba, akiwafunga watu wa familia yake ili wawe na umoja, kama vile Kristo alivyo kichwa cha kanisa, naye ni Mwokozi wa mwili wake, yaani, kanisa. Kwa hiyo asema: “Kama vile kanisa limtiivyo Kristo vivyo hivyo wake nao wawatii waume zao katika kila jambo. Enyi waume, wapendeni wake zenu, kama Kristo naye alivyolipenda kanisa, akajitoa kwa ajili yake, ili makusudi alitakase na kulisafisha kwa maji katika neno; apate kujiletea kanisa tukufu, lisilo na ila wala kunyanzi wala lo lote kama hayo; bali liwe takatifu lisilo na mawaa. Vivyo hivyo imewapasa waume nao kuwapenda wake zao kama miili yao wenyewe.” Waefeso 5:24-28.

Neema yake Kristo, na hiyo peke yake, inaweza kuifanya taasisi hii kuwa kama vile Mungu alivyokusudia iwe—yaani, kuwa njia ya kuwabariki na kuwainua wanadamu. Na kwa njia hiyo familia za duniani, katika umoja, amani, na upendo wao, zinaweza kuwa mfano wa familia ile ya mbinguni.

Siku hizi, kama ilivyokuwa katika siku za Kristo, hali ya wanadamu katika ndoa zao ni ya kusikitisha ukiielezea kulingana na kipeo kilichowekwa na mbingu cha utakatifu wa uhusiano huo. Lakini, hata kwa wale ambao wameona uchungu na kukata tamaa badala ya kupata urafiki na furaha nyumbani mwao, Injili ya Kristo

inawapa faraja. Uvumilivu na upole awezao kuwapa Roho wake utawapunguzia

uchungu katika maisha yao. Moyo ule ambao Kristo hukaa ndani yake, utajazwa na kuridhishwa na upendo wake, wala hautaona haja ya kuhurumiwa na wengine. Na kwa njia ya kujitoa nafsi kwa Mungu, hekima yake itaweza kutimiliza mambo yasiyoweza kutimilika kwa hekima ya kibinadamu. Kwa njia ya kuidhihirisha neema yake, mioyo iliyokuwa baridi na kutengana itaweza kuungana na kufungwa pamoja na vifungo imara zaidi na vinavyodumu kuliko vile vya dunia hii, —yaani, vifungo bora mno vya upendo; ambavyo vitastahimili mtihani wa majaribu.

“Usiape Kabisa.” Mathayo 5:34.

Sababu ya amri hii imetolewa: Hatutakiwi kuapa “hata kwa mbingu, kwa maana ndicho kiti cha enzi cha Mungu; wala kwa nchi, kwa maana ndiyo ya kuwekea miguu yake; wala kwa Yerusalemu, kwa maana ndio mji wa Mfalme mkuu. Wala usiape kwa kichwa, maana huwezi kufanya unywele mmoja kuwa mweupe au mweusi.”
Vitu vyote vyatoka kwa Mungu. Hatuna kitu cho chote tusichopewa; na zaidi ya hayo, hatuna kitu cho chote kisichonunuliwa kwa damu ya Kristo. Vyote tulivyo navyo vimekuja kwetu vikiwa vimepigwa muhuri wa msalaba, vimenunuliwa kwa damu ya thamani isiyopimika, kwani damu hiyo ndiyo uzima wa Mungu. Kwa hiyo, hakuna kitu cho chote tunachoweza kudiriki kukidai kana kwamba ni chetu wenyewe, kwa kusudi la kulitimiza neno letu.

Wayahudi walifahamu amri ya tatu kuwa ilikataza watu wasilitumie jina la Mungu vibaya kwa kufuru; lakini walidhani kwamba walikuwa huru kutumia viapo vingine. Kuapa lilikuwa ni jambo la kawaida sana miongoni mwao. Kwa njia ya Musa walikuwa wamekatazwa wasifanye kiapo cha uongo; lakini walikuwa na mbinu nyingi za kukwepa uwajibikaji kwa kiapo walichotoa. Hawakuogopa kusema maneno ya kufuru, wala kuapa uongo, mradi tu waliweza kuficha kwa kutumia ufundi wa kuikwepa sheria.

Yesu aliyashutumu matendo yao, aliwatangazia kwamba desturi zao za kiapo zilikuwa zikikiuka amri ya Mungu. Lakini Mwokozi wetu hakukataza kiapo cha kisheria mbele ya hakimu, ambacho kwacho Mungu huitwa kuwa shahidi kwamba maneno yanayosemwa yote ni kweli tupu. Yesu mwenyewe, alipohukumiwa mbele ya Baraza la Wayahudi (Sanhedrin), hakukataa kushuhudia alipoapishwa. Kuhani mkuu alimwambia, “Nakuapisha kwa Mungu aliye hai, utuambie kama wewe ndiwe Kristo, Mwana wa Mungu.” Yesu alimwambia, “Wewe umesema.” Matha yo 26:63,64. Kama Kristo, katika mahubiri yake pale mlimani, angalikuwa amekataza kiapo cha kisheria mbele ya hakimu, basi, katika hukumu yake angalimkemea yule kuhani mkuu alipomwapisha; na kwa njia hiyo angaliyatia nguvu mafundisho yake, ili wafuasi wake wote wajue la kufanya.

Kuna watu wengi sana wasioogopa kuwadanganya wenzao, lakini wamekwisha kuonywa na kuguswa moyoni na Roho wa Mungu, kwamba ni jambo la kutisha kumwambia Mwumbaji wao uongo. Wanapoapishwa, wanafanywa waone mioyoni mwao kwamba hawashuhudii mbele ya wanadamu tu, ila mbele za Mungu pia; kwamba wakishuhudia uongo, basi, wanamshuhudia Yeye asomaye moyo na kujua yaliyo kweli hasa. Kule kujua habari za hukumu zenye kutisha ambazo zimewapata wengine waliofanya dhambi hii, kuna mvuto wenye nguvu kuwazuia wasiseme uongo.

Lakini kama kuna mtu awaye yote awezaye kushuhudia chini ya kiapo kwa uthabiti, mtu huyo ni Mkristo. Anaishi siku zote kana kwamba yuko mbele zake Mungu, akijua kwamba kila wazo liko wazi mbele za macho yake Yeye aliye na mambo yetu (Waebrania 4:13); na akiapishwa kiapo halali cha kisheria mbele ya hakimu, ni haki yake kumwomba Mungu awe shahidi kwamba kile asemacho ni kweli tupu.

Yesu aliendelea kutoa kanuni ambayo kwayo kuapa kiapo kusingehitajika, kama watu wangeifuata kanuni hiyo. Alifundisha kwamba kusema kweli tupu kumepasa kuwa sharti la maneno yote tusemayo. “Maneno yenu yawe, ndiyo, ndiyo; siyo, siyo; kwa kuwa yazidiyo hayo yatoka kwa yule mwovu.”

Maneno haya yanayashutumu maneno yote yasiyo na maana na matusi yote yanayoelekea kwenye kufuru. Yanashutumu maneno yote ya kumsifu mtu asivyostahili, kuikwepa kweli, kupiga chuku, kutia chumvi nyingi, kupunja katika biashara, mambo ambayo yapo sasa katika jamii na katika ulimwengu wa biashara. Yanatufundisha kwamba mtu ye yote anayejifanya aonekane kinyume cha vile alivyo hasa, ama yule ambaye maneno yake hayaoneshi hisia za kweli zilizo moyoni mwake, hawezi kuitwa mkweli.

Maneno haya ya Kristo kama yangesikiwa, watu wangezuiwa wasitoe maneno mabaya juu ya wengine wala kuwakosoa vibaya; kwa kuwa tunapotoa maoni yetu juu ya matendo na maazimio ya mtu mwingine, ni nani awezaye kuwa na hakika kwamba asemayo ni kweli tupu? Ni mara ngapi majivuno, hasira, chuki ya kibinafsi, huutia doa mvuto uliotolewa! Mtupo wa jicho, neno moja, hata namna neno hilo lisemwavyo, linaweza kujaa uongo ndani yake. Pengine hata mambo ya kweli yanaweza kusemwa kwa namna iwezayo kuleta mvuto wa uongo. Isitoshe, maneno yote “yazidiyo hayo yatoka kwa yule mwovu.”

Kila jambo wafanyalo Wakristo lapaswa kuwa dhahiri kabisa kama ulivyo mwangaza wa jua. Kweli yatoka kwa Mungu; uongo na udanganyifu wa kila aina watoka kwa Shetani; na ye yote kwa njia yo yote ile anayeiacha njia nyofu ya

ukweli hujitia chini ya mamlaka ya yule mwovu. Hata hivyo si jambo jepesi au

rahisi kusema kweli tupu. Hatuwezi kusema kweli tusipoijua hiyo kweli; tena ni mara ngapi maoni tuliyo nayo, mwelekeo wetu kimawazo wa yale tunayoyapendelea, kutokuwa na ujuzi kamili, makosa katika maamuzi yetu, huzuia ufahamu sahihi wa mambo yale tunayopaswa kufanya! Hatuwezi kusema kweli isipokuwa kama nia zetu zinaongozwa daima na Yeye Aliye kweli.

Kwa njia ya mtume Paulo, Kristo atuambia: “Maneno yenu yawe na neema siku zote.” “Neno lo lote lililo ovu lisitoke vinywani mwenu, bali lililo jema la kumfaa mwenye kuhitaji, ili liwape neema wanaosikia.” Wakolosai 4:6; Waefeso 4:29. Katika nuru ya maandiko haya maneno aliyoyatoa Kristo pale mlimani, yanaonekana kana kwamba yanakataza maongezi yote ya upuzi, na ya kipumbavu na yote yasiyo safi. Yanataka maneno yetu yote yawe si ya kweli tu, bali safi pia. Wale ambao wamejifunza kwake Kristo hawatashirikiana na “Matendo yasiyozaa ya giza.” Waefeso 5:11. Katika maongezi yao, kama ilivyo katika maisha yao, watakuwa amini, wanyofu, na wakweli; kwani wanajitayarisha kushirikiana na watakatifu ambao “katika vinywa vyao haukuonekana uongo.” Ufunuo 14:5.

“Msishindane na Mtu Mwovu; Lakini Mtu Akupigaye Shavu la Kuume,
Mgeuzie na la Pili.” Mathayo 5:39.

Matukio yanayochochea chuki kwa Wayahudi yalikuwa yakiendelea kutokea daima kila walipokutana na askari wa Kirumi. Vikosi vya askari hao viliwekwa sehemu mbalimbali katika Yudea yote na kule Galilaya, na kuwapo kwao kuliwakumbusha Wayahudi udhalilishwaji wao kama taifa. Wakiwa na uchungu moyoni walisikia sauti kuu ya parapanda na kuona askari wakijipanga safu penye bendera ya Kirumi na kusujudu kuiheshimu ile alama ya mamlaka ya Rumi. Mara kwa mara kulikuwa na mapambano baina ya Wayahudi na askari hawa, na mambo hayo yalichochea chuki mioyoni mwao. Mara kwa mara, kama afisa wa Kirumi na kikosi chake walitoka kwenye zamu yao kwenda mahali pengine, waliwakamata Wayahudi waliowakuta wakilima mashambani, na kuwalazimisha kuichukua mizigo yao, au kuwashurutisha kufanya kazi nyinginezo zilizohitajiwa. Hivi ndivyo ilivyokuwa kwa mujibu wa sheria na desturi ya Kirumi, na kuyapinga madai kama hayo kungewaletea tu shutuma na kutendewa ukatili. Kila siku ndani kabisa ya mioyo ya watu shauku kuu iliingia ya kutupilia mbali kongwa la utumwa la Kirumi. Hasa miongoni mwa Wagalilaya shupavu na wajeuri roho ya kufanya maasi dhidi ya serikali ile ilikuwa imeenea kote. Kapernaumu, ukiwa ni mji wa mpakani, ulikuwa ngome ya askari walinzi; hata wakati ule Yesu alipokuwa akiwafundisha watu mlimani, waliweza kuwaona askari na kusikia uchungu kwa ajili ya hali duni ya Israeli. Kwa hamu watu walimtazama Kristo, wakitumainia kwamba Yeye ndiye atakayekishusha kiburi cha Warumi.

Yesu aliona huzuni moyoni mwake alipoziangalia nyuso za watu zilizoinuliwa juu mbele yake. Aliona kwamba moyo wa kulipiza kisasi ulikuwa umetia alama nyusoni mwao; akajua kwamba walitamani sana kupata uwezo kusudi kuyavunja mamlaka ya wadhalimu wao. Kwa moyo mzito akawaambia: "Msishindane na mtu mwovu; lakini mtu akupigaye shavu la kuume, mgeuzie na la pili."

Maneno haya yalikuwa ni marudio tu ya mafundisho ya Agano la Kale. Ni kweli kwamba kanuni hii ya "Jicho kwa jicho, jino kwa jino" ilikuwa ni kipengele kimoja katika torati iliyotolewa kwa mkono wa Musa (Walawi 24:20); lakini ilikuwa ni sheria ya serikali. Hakuna hata mmoja aliyeweza kuwa na haki ya kujilipizia kisasi, kwani walikuwa na maneno haya ya Bwana: "Usiseme, mimi nitalipa mabaya." "Usiseme, Nitamtenda kama alivyonitenda mimi." "Usifurahi, adui yako aangukapo." "Adui yako akiwa ana njaa, mpe chakula; tena akiwa ana kiu, mpe maji ya kunywa." Mithali 20:22; 24:29,17; 25:21,22.

Maisha yote ya Yesu hapa duniani yaliidhihirisha kanuni hii. Ilikuwa ni kwa ajili ya kuwaletea adui zake mkate wa uzima ndiyo maana Mwokozi aliyaacha makao yake mbinguni. Ingawa tangu kuzaliwa kwake mpaka alipoingia kaburini alisingiziwa na kuteswa, mambo hayo yalimfanya tu aoneshe moyo wa upendo na msamaha. Kwa njia ya nabii Isaya alisema: "Naliwatolea wapigao mgongo wangu, wang'oao ndevu mashavu yangu; sikuficha uso wangu usipate fedheha na kutemewa mate." "Alionewa, lakini akajinyenyekea, wala hakufunua kinywa chake; kama mwana-kondoo apelekwaye machinjoni, na kama kondoo anyamazavyo mbele yao wakatao manyoya yake; naam, hakufunua kinywa chake." Isaya 50:6; 53:7. Toka msalabani pale Kalvari tunaisikia dua yake aliyowaombea wauaji wake, na ujumbe wa matumaini aliompa yule mwivi aliyekuwa akifa.

Baba alikuwapo pale pamoja na Kristo, akiwa amemzunguka pande zote, na jambo lo lote halikumpata ila lile lililoruhusiwa na Mungu kwa ajili ya kuuletea ulimwengu mibaraka. Hili lilikuwa ndilo chimbuko la faraja yake, na ni letu sisi pia. Anayejazwa Roho wa Kristo hukaa ndani ya Kristo. Pigo linaloelekezwa kwake linaanguka juu ya Mwokozi, ambaye anamzunguka pande zote, akiwa pamoja naye. Lo lote limpatalo yeye linatoka kwa Kristo. Yeye hana haja ya kuupinga uovu, kwa maana Kristo ndiye mlinzi wake. Hakuna cho chote kiwezacho kumgusa isipokuwa kwa kibali chake Bwana, na "mambo yote" anayoruhusu "hufanya kazi pamoja na wale wampendao katika kuwapatia mema." Warumi 8:28.

"Na mtu atakaye kukushtaki na kuitwaa kanzu yako, mwachie na joho pia. Na mtu atakayekulazimisha mwendo wa maili moja, nenda naye mbili." Mathayo

5:40,41.

Badala ya kuwafanyia wenye mamlaka ukaidi, Yesu aliwaambia wanafunzi wake ya kwamba ni afadhali wafanye hata zaidi ya yale waliyotakiwa kufanya. Na, kadiri iwezekanavyo, wafanye kila wajibu uwapasao, hata kama ni zaidi ya sheria ya nchi inavyotaka wafanye. Torati, kama ilivyotolewa kwa mkono wa Musa, iliamuru kuwatendea kwa upole sana maskini. Mtu maskini alipoiweka nguo yake amana au rehani kwa ajili ya deni, mdai wake hakuruhusiwa kuingia nyumbani mwake ili kuitwaa; ilimpasa kungoja barabarani hata yule maskini amletee nje. Na kwa hali iwayo yote, kile kitu kilichowekwa amana kilipaswa kurudishwa kwa mwenyewe kabla ya jua kuchwa. (Kumbukumbu la Torati 24:10-13). Katika siku za Kristo watu hawakuyajali maagizo haya ya kuwa na huruma; lakini Yesu aliwaonesha wanafunzi wake kwamba iliwapasa kuutii uamuzi wa mahakama, hata kama unadai zaidi ya yale yaliyoamriwa katika sheria ya Musa. Hata kama ungedai watoe sehemu ya mavazi yao, walipaswa kukubali. Zaidi ya hayo, wampe mdai wao halali yake, ikibidi kumpa zaidi ya kile mahakama ilichohalalisha kutwaa. "Na mtu atakaye kukushtaki na kuitwaa kanzu yako, mwachie na joho pia." Na wanyapara wa safari wakikulazimisha kwenda nao mwendo wa maili moja, nenda nao mbili.

Yesu aliendelea kusema, "Akuombaye mpe; naye atakaye kukopa kwako, usimpe kisogo." Musa pia alifundisha jambo hilo; "Usifanye moyo wako kuwa mgumu, wala usimfumbie mkono wako nduguyo maskini: lakini mfumbulie mkono wako kwa kweli, umkopeshe kwa kweli yatoshayo haja yake." Kumbukumbu la Torati 15:7,8. Maandiko haya yanaeleza wazi kabisa maana ya maneno ya Mwokozi. Kristo hatufundishi kutoa bila busara kwa wote watuombao msaada wa fedha; bali anasema, "Umkopeshe kwa kweli yatoshayo haja yake;" na hiyo ni afadhali iwe zawadi kuliko kuwa mkopo; kwa maana tumeagizwa "kukopesha [tu]situmaini kupata malipo." Luka 6:35.

"Ajitoaye nafsi yake pamoja na sadaka yake kwa maskini
huwalisha watatu,
Yeye mwenyewe, jirani yake mwenye njaa, na Mimi."

"Wapendeni Adui Zenu." Mathayo 5:44.

Fundisho la Mwokozi aliposema, "Msishindane na mtu mwovu," lilikuwa gumu kwa Wayahudi waliokuwa na moyo wa kulipiza kisasi, nao miongoni mwao walilinung'unikia wao. Lakini baadaye tena Yesu alisema maneno magumu zaidi: "Mmesikia kwamba imenenwa, Umpende jirani yako, na umchukie adui yako." "Lakini nawaambia ninyi mnaosikia, Wapendeni adui zenu, watendeeni mema wale ambao wawachukia ninyi, wabarikieni wale ambao wawalaani ninyi, waombeeni wale ambao wawaonea ninyi;" "ili mpate kuwa wana wa Baba yenu

aliye mbinguni.” Mathayo 5:43-45; Luka 6:27,28.

Hiyo ndiyo maana halisi ya sheria ambayo waalimu wa Kiyahudi walikuwa wameieleza vibaya kuwa haina huruma, tena ina masharti magumu. Walijiona wenyewe kuwa bora kuliko watu wengine wote, na ya kwamba walistahili kupewa upendeleo wa pekee wa Mungu, ati kwa sababu wamezaliwa Waisraeli, lakini Yesu aliwaonesha kwamba moyo wa upendo wenye kusamehe ndio utashuhudia kuwa wao walikuwa wamesukumwa na moyo mwema kuliko ule wa watoza ushuru na wenye dhambi, ambao waliwadharau.

Aliwaelekeza wasikilizaji wake kwa Mtawala wa malimwengu, ili wamjue kwa jina jipya, "Baba yetu." Akataka kuwafundisha jinsi Mungu anavyowaangalia kwa moyo wa upendo na huruma. Anafundisha kwamba Mungu hujishughulisha na kila mtu aliyepotea: "kama vile baba awahurumiavyo watoto wake, ndivyo Bwana anavyowahurumia wamchao." Zaburi 103:13. Dhana kama hiyo juu ya Mungu ilikuwa haijapata kutolewa kamwe kwa walimwengu na dini iwayo yote isipokuwa ile ya Biblia tu. Ukafiri unawafundisha watu kumwangaliaMungu Mkuu kama kitu cha kuleta hofu kuliko upendo—yaani, kama mungu mwenye nia mbaya ya kuwadhuru anayestahili kutulizwa kwa njia ya kafara, badala ya kumwona Yeye kama Baba anayewamwagia watoto wake zawadi ya upendo wake. Hata Waisraeli walikuwa wamepofushwa macho mpaka ha wakuweza kufahamu mafundisho ya thamani ya manabii juu ya Mungu na upendo wake, na Yesu alipowafunulia jambo hili, lilikuwa kama jambo geni kwao.

Wayahudi walishikilia kwamba Mungu anawapenda wale wamtumikiao,—yaani, kwa maoni yao, ni wale waliotimiza matakwa ya waalimu wakuu wa Kiyahudi,— na ya kuwa walimwengu wengine wote Mungu huwachukia na kuwalaani. Lakini, Yesu alisema, Sivyo; walimwengu wote, wabaya kwa wema, wanapendwa na Mungu. Kweli hii mngalikuwa mmejifunza kutokana na viumbe vya asili vyenyewe; "maana yeye huwaangazia jua lake waovu na wema, huwanyeshea mvua wenye haki na wasio haki."

Hakuna uwezo wo wote ndani ya dunia yenyewe unaoiwezesha kutoa mavuno yake kila mwaka, na kuiendesha katika mwendo wake wa kulizunguka jua. Mkono wa Mungu unaziongoza sayari na kuziweka mahali pao katika mwendo wao ulioratibiwa kupitia katika mbingu. Ni kwa uwezo wa Mungu, wakati wa baridi na hari, kupanda na kuvuna, mchana na usiku hufuatana kwa utaratibu wake. Kwa neno lake mimea inapata kusitawi, na kutoa majani na maua yake. Kila kitu chema tunachokipata, mwangaza wa jua na kunyesha kwa mvua, kila kipande cha chakula, na kila dakika ya uhai wetu, ni kipawa cha upendo wa Mungu.

Tulipokuwa tungali hatuna upendo wala hatupendeki kwa tabia zetu, "tukichukiza na kuchukiana," Baba yetu aliye mbinguni alituhurumia. "Lakini

wema wake Mwokozi wetu Mungu, na upendo wake kwa wanadamu,

ulipofunuliwa, alituokoa; si kwa sababu ya matendo ya haki tuliyoyatenda sisi, bali kwa rehema yake.” Tito 3:3-5. Vivyo hivyo, tukiupokea upendo wake, utatufanya kuwa wenye upendo na huruma, siyo tu kwa watu wanaotupendeza, bali kwa wakosaji wakubwa pia, wenye kutenda mabaya, na wenye kufanya dhambi.

Watoto wa Mungu ndio wale wanaoshiriki tabia yake. Kuwa na cheo hapa duniani, wala kuwa wa ukoo ulio bora, wala kuwa mtu wa taifa maalum, wala kuwa mkuu wa mambo ya dini, hayo siyo mambo yanayoweza kuthibitisha kwamba tu watu wa nyumba ya Mungu; ila ni upendo, yaani, upendo kwa wanadamu wote. Hata wenye dhambi, ambao hawajamfungia kabisa Roho wa Mungu mioyoni mwao, wanaweza kuvutwa na huruma; ingawa wanaweza kuchukia wakichukiwa, pia wataonesha upendo kama wakipendwa. Lakini kutoa upendo penye chuki hakuwezekani ila kwa Roho wa Mungu. Kuwahurumia wasio na shukrani na waovu, kutenda mema bila kutumaini kupata kitu tena, ndiyo alama ya watu wa nyumba ya Mfalme aliye mbinguni, na dalili ya kweli ambayo kwayo watoto wa Mungu hudhihirisha hali bora waliyo nayo.

“Basi Mtakuwa Ninyi Wakamilifu, Kama Baba Yenu wa Mbinguni Alivyo Mkamilifu.”
Mathayo 5:48.

Neno hili “basi” laonesha hitimisho la maneno yaliyotangulia. Yesu alikuwa amewaeleza wasikilizaji wake juu ya rehema ya Mungu na upendo wake usiopimika, kwa hiyo, akawaamuru wawe wakamilifu. Kwa sababu Baba yenu aliye mbinguni “ni mwema kwa wasiomshukuru, na waovu,” (Luka 6:35), kwa kuwa Yeye alijidhili kusudi kutuinua sisi, basi, Yesu asema, mnaweza kufanana naye katika tabia zenu, kusimama bila mawaa mbele ya watu na mbele za malaika.

Masharti ya kupata uzima wa milele, chini ya neema, ni kama yalivyokuwa zamani kule Edeni,—kuwa na haki kamilifu, kupatana na Mungu, kufuata kabisa kanuni za sheria yake. Kipeo cha tabia kilichotakiwa katika Agano la Kale, ndicho kinachooneshwa katika Agano Jipya. Hiki si kipeo tusichoweza kukifikia. Katika kila amri na agizo la Mungu kuna ahadi yake. Mungu yu tayari kutuwezesha kufanana naye, tena atatimiza kusudi lake hili kwa wote wasiomwasi kwa nia ya ukaidi, na kuyapinga mapenzi yake na hivyo kuifanya neema yake isifanye kazi
Mungu ametupenda kwa upendo mkuu usiosemekana; na kwa kadiri tunavyofahamu mapana na marefu na kimo na kina cha upendo huu upitao akili zote, ndivyo mioyo yetu itakavyoamshwa kumpenda Mungu. Kwa vile tunavyovutwa kwake Kristo kwa ajili ya uzuri wake, na kujua jinsi

alivyotudhihirishia upendo wake tulipokuwa tungali wenye dhambi, moyo mgumu

hutiishwa na mwenye dhambi huongoka moyo na kuwa mwana wa Mungu. Mungu hatumii nguvu kumlazimisha mtu; hutumia upendo tu kuiondoa dhambi moyoni. Kwa njia ya upendo hugeuza majivuno kuwa unyenyekevu, uadui na kutoamini kuwa upendo na imani.

Wayahudi walikuwa wametaabika wakijaribu kufikia ukamilifu kwa kujitahidi wenyewe, na walikuwa wameshindwa. Kristo alikuwa tayari amekwisha kuwaambia ya kwamba kwa haki yao wenyewe wasingeweza kamwe kuingia katika ufalme wa mbinguni. Sasa awaonesha namna ya haki watakayokuwa nayo wote watakaoingia mbinguni. Katika mahubiri yote mlimani, alieleza matunda ya haki ile, na sasa kwa sentensi moja anawaonesha asili yake na hali yake jinsi ilivyo: “Mwe wakamilifu kama Mungu alivyo mkamilifu.” Sheria ni mfano halisi wa tabia ya Mungu. Tazameni ndani ya Baba yenu aliye mbinguni mwone kikamilifu hizo kanuni ambazo ni msingi wa serikali yake.

Mungu ni upendo. Kama mishale ya nuru inavyotoka juani, nd ivyo upendo na nuru na furaha vinavyotoka kwake kwenda kwa viumbe vyake vyote. Ni tabia yake kutoa. Maisha yake hasa ni bubujiko la upendo usiojifikiria nafsi yake wenyewe.

“Utukufu wake ni kuwatakia mema watoto wake; Furaha yake, ni Ubaba wake wenye huruma.”

Anatuambia sisi tuwe wakamilifu kama yeye alivyo mkamilifu, kwa namna ile ile moja. Tunatakiwa tuwe asili ya nuru na baraka kwa jamaa zetu, kama vile Mungu alivyo kwa malimwengu. Sisi wenyewe hatuna cho chote, lakini nuru ya upendo wake inatuanga zia, nasi yatupasa kuitoa na kuitupa nuru ile kwa wengine. “”Katika wema wake tulioazimwa,” twaweza kuwa wakamilifu katika mazingira yetu, kama vile Mungu alivyo mkamilifu katika mazingira yake.

Yesu alisema, Mtakuwa wakamilifu kama Baba yenu alivyo mkamilifu. Ikiwa ninyi ni watoto wa Mungu, basi, ninyi ni washiriki wa tabia yake, nanyi hamna budi kufanana naye. Kila mtoto huishi kwa uhai wa baba yake. Kama ninyi ni watoto wa Mungu,—mliozaliwa kwa Roho wake,—mnaishi kwa uzima wa Mungu. Katika Kristo “unakaa utimilifu wote wa Mungu, kwa jinsi ya kimwili” (Wakolosai 2:9), na uhai wa Yesu unadhihirishwa “katika miili yetu ipatikanayo na mauti” (2 Wakorintho 4:11). Uhai ule ukiwa ndani yenu utafanyiza tabia ile ile na kuonesha matendo yale yale kama ulivyofanya ndani yake. Hivyo mtapatana na kila agizo la sheria yake; kwani “sheria ya Bwana ni kamilifu, huiburudisha nafsi.” Zaburi 19:7. Kwa njia ya upendo “maagizo ya torati” yata“timizw(a) ndani yetu sisi, tusioenenda kwa kufuata mambo ya mwili, bali mambo ya Roho.” Warumi 8:4.

## SURA YA 4

## SABABU YA KWELI KATIKA HUDUMA

“Angalieni msifanye wema wenu machoni pa watu, kusudi mtazamwe na wao.” Mathayo 6:1.

MANENO ya Kristo mlimani yalidhihirisha mambo yale yaliyokuwa mafunzo ya kimya ya maisha yake, lakini watu waliyoshindwa kuyafahamu. Hawakuweza kuelewa jinsi ambavyo, yeye akiwa na uwezo mkuu kama ule, aliacha kuutumia kujipatia mambo yale ambayo wao walidhani ni bora sana. Moyo wao, makusudi yao, na njia zao zilikuwa kinyume kabisa na zake. Ingawa walijidai kuwa walikuwa na wivu sana kuona kuwa sheria ile inaheshimiwa, kusudi lao hasa lilikuwa kujipatia heshima wenyewe; na Kristo alitaka kuwadhihirishia kwamba mwenye kujipenda mwenyewe ni mvunja sheria.

Lakini kanuni zile zilizopendwa sana na Mafarisayo ni zile zinazoonesha tabia ya wanadamu wa vizazi vyote. Roho ile ya Ufarisayo ndiyo tabia ya kibinadamu; na kama Mwokozi alivyoonesha tofauti kati ya roho yake mwenyewe na njia zake na zile za waalimu, ndivyo mafundisho yake kwa ulinganifu yanavyo wahusu watu wa zama zote.

Katika siku za Kristo Mafarisayo walikuwa wakijaribu daima kujipatia kibali kwa Mungu kwa njia ya matendo, ili wapate heshima ya kidunia na kufanikiwa, mambo ambayo waliyahesabu kuwa ijara ya matendo mema. Huku kwa majivuno wakionesha utoaji wao wa sadaka mbele ya watu ili kuyavuta macho yao wawatazame, na hivyo kujipatia sifa kuwa wao ni watauwa.

Yesu alikemea majivuno yao, alisema kwamba Mungu haitambui huduma kama ile na ya kwamba kusifiwa mno na watu isivyostahili na kupewa heshima walikotaka sana, kulikuwa ndiyo ijara pekee ambayo wangeipokea.

“Bali wewe utoapo sadaka,” akasema, “hata mkono wako wa kushoto usijue ufanyalo mkono wako wa kuume; sadaka yako iwe kwa siri; na Baba yako aonaye sirini atakujazi.”

Kwa maneno haya Yesu hakufundisha ya kuwa kila tendo la fadhili lazima liwe la siri. Mtume Paulo, alipoandika akiongozwa na Roho Mtakatifu, hakuficha neno la kujinyima na ukarimu wa Wakristo wa Makedonia; bali alieleza juu ya neema za Kristo alizowakirimia, na hivyo wengine waliingiwa na moyo wa namna ile. Pia aliwaandikia watu wa kanisa la Korintho, na kusema, “Bidii yenu imewatia moyo

wengi wao." 2 Wakorintho 9:2.

Maneno yenyewe aliyoyasema Kristo huidhihirisha maana yake,—ya kuwa kusudi la kutoa sadaka na kusaidia maskini lisiwe kujipatia wenyewe sifa na heshima kutoka kwa watu. Mwenye kuishi maisha ya utauwa na kufanana na Kristo hataki kujivuna wala kujitamba. Wale watakao kusifiwa na wengine na kusifiwa isivyostahili, huku wakipendezwa moyoni kwa ajili ya maneno hayo, ni Wakristo wa jina tu.

Kwa matendo yao mema, wafuasi wa Kristo hawatajiletea wenyewe utukufu, bali watamtukuza yeye aliyewawezesha kuyatenda kwa neema yake na uweza wake. Kila tendo jema linafanywa kwa njia ya Roho Mtakatifu, na Roho Mtakatifu hutolewa kusudi kumtukuza Mtoaji, si mpokeaji. Nuru ya Kristo ikiangaza moyoni, mdomo utajaa sifa na shukrani kwa Mungu. Maombi yako, namna unavyofanya wajibu wako, sadaka zako, kujinyima kwako,—mambo haya hayatakuwa jambo kubwa fikarani mwako wala katika mazungumzo yako. Yesu ndiye atakayetukuzwa, nafsi yako itakuwa ikifichwa, na Kristo atadhihirishwa katika yote.

Inatupasa kutoa kwa moyo, si kwa kuyaonesha matendo yetu mema, ila kwa ajili ya kuwahurumia na kuwapenda wale wanaoteseka. Kuwa na nia ya kweli, na huruma moyoni, ndio msukumo anaouthamini Mungu. Yule aliye na upendo wa kweli, anayemcha Mungu kwa moyo wake wote, ndiye Mungu amhesabuye kuwa mwenye thamani kubwa kuliko dhahabu ya ofiri.

Tusifikiri juu ya kupata ijara, bali tufikiri jinsi tunavyoweza kuwahudumia wengine; lakini wema unaofanywa kwa moyo huo hautakosa kupata ijara yake. “Baba yako aonaye sirini atakujazi.” Ingawa ni kweli kwamba Mungu mwenyewe ndiye Thawabu kuu, mwenye kuzikumbatia thawabu nyingine zote, mtu aweza kumpokea na kumfurahia tu, wakati anapofanana naye kwa tabia. Ni wale wafananao tu ndio wawezao kupendana na kufurahiana. Ni wakati ule tunapojitoa wenyewe kwa Mungu ili kuwahudumia wanadamu, anapojitoa kwetu sisi.

Hakuna awezaye kumwachia Mungu nafasi moyoni mwake na maishani mwake kuwa njia ya kuwapitishia wengine baraka zake, pasipo kupokea thawabu kubwa yeye mwenyewe. Vilima na mabonde vinavyopitisha maji ya mito kwenda baharini havipati hasara kwa sababu hii. Kile vinachotoa vinalipwa mara mia. Kwani kijito kile kinachoimba kinapokwenda zake huacha nyuma thawabu yake ya mimea mingi na mazao mengi. Majani kwenye kingo zake ni chanikiwiti, miti ina majani ya kijani, na maua ni mengi zaidi. Ardhi inapokuwa tupu na ya kikahawia kutokana na joto kali linalounguza la kiangazi, mstari wa mimea mingi huonesha mipaka ya mto; na nchi ile tambarare iliyopokea hazina zilizotoka

mlimani kwenda baharini inapendeza na kuonekana nzuri, huo ni ushuhuda wa

*One-Soul Audience Ministry*

malipo ambayo Mungu huwapa wote wanaojitoa kuwa njia ya kuwapitishia wengine neema yake.

Hii ndiyo baraka ya wale wanaowahurumia maskini. Nabii Isaya asema: “Je, siyo kuwagawia wenye njaa chakula chako, na kuwaleta maskini waliotupwa nje nyumbani kwako? Umwonapo mtu aliye uchi, mvike nguo; wala usijifiche na mtu mwenye damu moja nawe? Ndipo nuru yako itakapopambazuka kama asubuhi, na afya yako itatokea mara;... Naye Bwana atakuongoza daima, ataishibisha nafsi yako mahali pasipokuwa na maji,... kama bustani iliyotiwa maji, na kama chemchemi ambayo maji yake hayapungui.” Isaya 58:7-11.

Tendo la fadhili linapata baraka mara mbili. Yeye anayetoa msaada kwa maskini huwaletea wengine baraka, na wakati uo huo yeye mwenyewe hupata baraka kwa kiwango kikubwa zaidi. Neema ya Kristo moyoni mwake hukuza tabia iliyo kinyume na uchoyo;—tabia itakayofanya maisha yake yawe adilifu, bora na yenye manufaa. Matendo ya fadhili yanayofanywa kwa siri yataifunga mioyo pamoja, na yataivuta karibu zaidi kwa moyo wake Yeye aliye asili ya kila tendo jema. Matendo madogo madogo ya kuwajali wengine, matendo yanayofanywa kwa upendo na kwa kujinyima yaonekanayo kimya kimya katika maisha kama harufu nzuri itokayo katika ua—mambo haya yanaleta mibaraka mingi na furaha kubwa katika maisha. Na mwishowe itaonekana kwamba kujinyima kwa ajili ya kuwafanyia wengine mema na kuwafurahisha, hata kama ni matendo madogo madogo yasiyosifiwa hapa duniani, huko mbinguni yanahesabiwa kuwa dalili ya umoja wetu na Yeye, aliye Mfalme wa utukufu, ambaye alikuwa tajiri, lakini akawa maskini kwa ajili yetu.

Matendo ya ukarimu huenda yakawa yamefanywa kwa siri, lakini matokeo yake juu ya tabia ya mtendaji hayawezi kufichwa. Sisi kama wafuasi wa Kristo, tukimtumikia kwa moyo wote, moyo wetu utashirikiana kwa karibu zaidi na Mungu, na Roho wa Mungu, akiugusa mo yo wetu, atafanya mwafaka mtakatifu uwemo moyoni kuitikia mguso huo wa Mungu.

Yeye awaongezeaye talanta wale waliovitumia vizuri vipawa walivyopewa, anapendezwa kuikubali huduma ya watu wake waaminio katika yule Mpendwa, ambaye kwa neema na nguvu zake wametenda kazi hizo. Wale waliojitahidi kuikuza na kuikamilisha tabia yao ya Kikristo kwa kutumia akili zao katika kutenda matendo mema, katika ulimwengu ujao, watavuna kile walichopanda. Kazi iliyoanzwa hapa duniani itafikia utimilifu wake katika maisha yale ya juu zaidi na matakatifu zaidi yatakayoendelea milele na milele.

“Tena Usalipo, Usiwe Kama Wanafiki.”

Mathayo 6:5.

Mafarisayo walikuwa na saa zilizowekwa kwa ajili ya kusali; na saa fulani ilipofika basi walisimama po pote walipokuwapo,—pengine njiani ama sokoni, kati ya masongamano ya watu waendao haraka,—na hapo walipaaza sauti na kusema sala zao za kawaida. Ibada ya namna ile iliyotolewa kwa majivuno tu, Yesu aliigombeza kwa ukali. Hata hivyo, Yesu hakukataza sala hadharani; kwani hata Yeye mwenyewe alisali pamoja na wanafunzi wake, na mbele za makutano. Lakini atufundisha ili sala zetu za faraghani zisitangazwe. Katika sala ya faraghani maombi yetu hayapaswi kusikiwa na mtu ye yote, ila Mungu asikiaye dua zetu. Sikio lo lote halipaswi kupokea mzigo wa dua kama hizo.

"Bali wewe usalipo, ingia katika chumba chako cha ndani." Uwe na mahali pa sala faraghani. Yesu alikuwa na mahali alipopaweka kwa maongezi na Mungu, nasi pia inatupasa kufanya hivyo. Tunahitaji kujitenga mara kwa mara na kwenda mahali pa faragha, ijapokuwa pasiwe mahali pazuri, tuwepo peke yetu pamoja na Mungu.

"Usali mbele za Baba yako aliye sirini." Kwa jina la Yesu tunaweza kuja mbele za Mungu kwa matumaini kama ya mtoto. Mtu ye yote hahitajiwi kuwa mpatanishi. Kwa njia ya Yesu twaweza kumfunulia Mungu mioyo yetu kama tufanyavyo kwa mtu atujuaye na atupendaye.

Tukiwa mahali pa kuombea faraghani, ambapo hapana macho yanayotuona ila ya Mungu tu, wala hakuna sikio liwezalo kutusikia ila la Mungu tu, hapo tunaweza kumweleza waziwazi Baba mwenye huruma zisizo na kiasi, tamaa na shauku zetu zilizojificha sana mioyoni mwetu, na katika utulivu na unyamavu wa moyo, sauti ile isiyokosa kujibu haja ya binadamu, itasema nasi katika mioyo yetu.

"Bwana ni mwingi wa rehema, mwenye huruma." Yakobo 5:11. Anangoja kwa moyo wa upendo usiochoka ili apate kusikia maungamo ya wale wapotovu na kuyakubali majuto yao. Hutazamia shukrani kutoka kwetu, kama vile mama mzazi amtazamiavyo mtoto wake mpendwa kumchekea na kumwonesha kwamba amemjua. Mungu ataka tufahamu jinsi anavyotupenda na kutuhurumia kwa moyo wake wote. Anatuita tumwendee na taabu zetu naye atatusaidia; tumpelekee huzuni zetu, naye atatufariji kwa upendo wake; tumpelekee majeraha yetu, naye atatuponya; tumpelekee udhaifu wetu, naye atatuwezesha kwa uwezo wake; tumwendee jinsi tulivyo bila kitu, naye atatujaza.

Hakuna hata mtu mmoja ambaye amekwenda kwake na kukatishwa tamaa kwa kutokupata msaada aliotumainia. "Wakamwelekea macho wakatiwa nuru: wala nyuso zao hazitaona ha ya." Zaburi 34:5.

Wale wanaomtafuta Mungu faraghani, na kumweleza Bwana haja zao, na kumwomba msaada wake, hawatamsihi bure bila kupata. “Baba yako aonaye sirini, atakujazi.” Kama tukimfanya Kristo kuwa mwenzetu kila siku, tutaona kuwa tumezungukwa na mamlaka za ulimwengu usioonekana; na kwa kumwangalia Yesu tutabadilishwa na kufanana naye. Kwa kuangalia tunabadilishwa. Tabia yetu inalainishwa, inaadilishwa na kuwa bora kwa ajili ya ufalme wa mbinguni. Matokeo ya hakika ya kuongea na kufanya urafiki na Bwana wetu yatakuwa kuzidishiwa utauwa, usafi, na nguvu. Tutazidi kuwa na ujuvi katika maombi. Tunapokea elimu ya Mungu, nayo inadhihirishwa katika maisha yenye bidii na uangalifu.

Mtu anayemgeukia Mungu ili apate msaada, riziki, na uwezo wake, kwa nj ia ya kuomba kila siku kwa moyo wa bidii—atanuia mambo ya juu yaliyo bora, atakuwa na ufahamu safi wa ile kweli na wajibu wake; katika matendo yake atakuwa na makusudi yaliyo bora, atakuwa daima mwenye njaa na kiu ya haki. Kwa kudumisha uhusiano wetu na Mungu, tutawezeshwa kuwatolea wengine nuru, na amani, na utulivu tulio nao mioyoni mwetu, kwa njia ya kushirikiana nao. Nguvu zipatikanazo kwa kumwomba Mungu, pamoja na kufanya bidii kuzizoeza roho zetu kuwa na uzingativu na uangalifu, humtayarisha mtu kwa kazi na wajibu wake wa kila siku, na kuutuliza moyo na kuulinda katika amani katika hali yo yote.

Tukimkaribia Mungu, atatia vinywani mwetu neno lake ili tupate kumshuhudia, hata sifa kwa ajili ya jina lake. Atatufundisha sehemu ya wimbo waimbao malaika, hata kumshukuru Baba yetu aliye mbinguni. Kwa kila tendo la maisha yetu, itadhihirishwa nuru na upendo wa Mwokozi akaaye moyoni. Taabu za nje haziwezi kuathiri maisha ya mtu aishiye kwa imani ya Mwana wa Mungu.

“Nanyi Katika Kusali Msipayuke Payuke Kama watu wa Mataifa.” Mathayo 6:7.

Watu wa mataifa wanayaangalia maombi yao kuwa ndani yake yenyewe yanayo sifa inayostahiki kuwalipia fidia ya dhambi zao. Kwa hiyo kadiri sala inavyokuwa ndefu, ndivyo stahili yao inavyozidi kuwa kubwa. Kama wangeweza kuwa watakatifu kwa kujitahidi kwao, basi wangekuwa na jambo la kushangilia, na sababu ya kujisifu. Dhana hii ya sala ni utendaji wa kanuni ya kulipa sadaka ili kulipa wenyewe fidia ya dhambi zao, huu ndio msingi wa dini zote za uongo. Mafarisayo walikuwa wameitumia dhana hii ya kipagani ya sala, na kwa vyo vyote vile ipo hata siku hizi, hata kati ya watu wanaojidai kuwa ni Wakristo. Kurudia-rudia kusema maneno yaliyotungwa kidesturi, wakati moyo haumhitaji Mungu, ni tabia ile ile ya “kupayuka-payuka” waliyo nayo watu wa Mataifa.

Sala si fidia ya dhambi; haina wema wo wote wala sifa ndani yake yenyewe. Maneno ya ufasaha tunayoweza kuyatumia katika kusali hayawezi kulinganishwa na haja moja takatifu. Maombi ya ufasaha sana ni maneno yasiyo na maana kama hayaoneshi hisia za kweli zilizomo moyoni. Lakini maombi yatokayo katika moyo mwaminifu yanayoeleza mahitaji ya kawaida yaliyomo moyoni, kama vile ambavyo tungaliweza kumwomba rafiki wa hapa duniani atusaidie, tukitumaini kwamba tutatimiziwa haja yetu—hayo ndiyo maombi ya imani. Mungu hataki kupokea maneno yetu ya kawaida ya kumsifu; ila kilio kisichosemekana kitokacho katika moyo uliopondeka na kuvunjika kwa ajili ya dhambi na udhaifu wake, hupanda juu na kumfikia Baba mwenye rehema.

"Tena Mfungapo, Msiwe Kama Wanafiki." Mathayo 6:16.

Kufunga kunakoamriwa katika neno la Mungu ni zaidi ya kufunga kwa mtindo tu. Hakuhusiani na kukataa tu chakula, kujivika nguo za magunia, na kujimwagia majivu kichwani. Yeye afungaye kwa kuwa amehuzunishwa moyoni kwa ajili ya dhambi zake, hataki kabisa kujionesha kwa wengine.

Kusudi la kufunga ambako Mungu anatutaka sisi tufunge si kuutesa mwili kwa ajili ya dhambi za moyo, bali ni kutusaidia kufahamu hali ya dhambi jinsi ilivyo mbaya mno, ili tujidhili mioyoni mwetu mbele za Mungu na kupokea neema yake inayotupatia msamaha. Aliwaamuru Waisraeli hivi: "Rarueni mioyo yenu, wala si mavazi yenu, mkamrudie Bwana, Mungu wetu." Yoeli 2:13.

Haitatufaa kitu kufanya kitubio au kujisifu kwamba kwa matendo yetu wenyewe tutastahili kupewa haki au kununua urithi na kuwa miongoni mwa watakatifu. Kristo alipoulizwa swali hili, "Tufanyeje ili tupate kuzitenda kazi za Mungu?" alijibu, "Hii ndiyo kazi ya Mungu, mmwamini yeye aliyetumwa na yeye." Yohana 6:28,29. Toba ni kuipa kisogo nafsi yetu na kwenda kwa Kristo; na tunapompokea Kristo ili kwa njia ya imani yeye aweze kuishi maisha yake ndani yetu, matendo mema yatadhihirishwa.

Yesu alisema, "Wewe ufungapo, jipake mafuta kichwani, unawe uso; ili usionekane na watu kuwa unafunga, ila na Baba yako aliye sirini." Lo lote lifanywalo kwa utukufu wa Mungu lifanywe kwa furaha na ukunjufu, si kwa huzuni na moyo mzito. Hakuna uzito wa moyo wo wote katika dini ya Yesu. EndapoWakristo, kwa mwonekano wao wa kuwa na huzuni na masikitiko, hudokeza kwa watu kuwa wamekata tamaa kwa kuwa hawakupata kwa Bwana kile walichotarajia kupata, watakuwa wanaiwakilisha vibaya tabia yake na kuweka hoja kinzani kinywani mwa adui zake. Ingawa kwa maneno yao wanaweza kudai kuwa Mungu ni Baba yao, lakini kwa ajili ya huzuni na mioyo yao mizito

huonekana kwa walimwengu kuwa wao ni yatima.

*One-Soul Audience Ministry*

Kristo ataka sisi tuwadhihirishie wengine kuwa kazi yake ni nzuri inaupendeza moyo, kama ilivyo hasa. Kujinyima kwetu na taabu za moyoni zifunuliwe tu kwa Mwokozi wetu mwenye huruma. Iache mizigo yako chini ya msalaba, nenda zako ukifurahia upendo wake yeye aliyekupenda wewe kwanza. Huenda wanadamu wasiweze kujua kamwe juu ya kazi ile inayoendelea kwa siri baina ya mtu na Mungu, lakini matokeo ya kazi ya Roho Mtakatifu aifanyayo moyoni yatatadhihirika kwa wote; kwani "Baba yako aonaye sirini atakujazi."

"Msijiwekee Hazina Duniani." Mathayo 6:19.

Hazina iwekwayo duniani haitadumu; wevi huvunja nyumba na kuiba; nondo na kutu zinaiharibu; moto na dhoruba zinafutilia mbali mali zenu. Na "hazina yako ilipo, ndipo utakapokuwapo na moyo wako." Hazina iliyowekwa duniani inachota mawazo yote yasipate kutafakari mambo ya mbinguni.

Kupenda mali kulikuwa ni tamaa iliyotawala katika zama zile za Wayahudi. Kuipenda dunia kulikuwa badala ya Mungu na dini moyoni mwao. Hivyo ndivyo ilivyo hata siku hizi. Tamaa ya mali na uchoyo huleta mvuto juu ya maisha yao unaowafanya waonekane kana kwamba wamelogwa na kupagawa na kuleta matokeo ya kuharibu tabia njema na kuchafua ubinadamu walio nao watu hao mpaka wanazama katika uharibifu. (1Timotheo 6:9). Kumtumikia Shetani huleta hali ya kuwa na mashaka mengi, mahangaiko na kazi ya taabu; na hazina ile ambayo wanadamu hushughulika sana kujilimbikizia hapa duniani ni ya kitambo tu.

Yesu alisema, "Msijiwekee hazina duniani, nondo na kutu viharibupo, na wevi huvunja na kuiba; bali jiwekeeni hazina mbinguni, kusikoharibika kitu kwa nondo wala kutu, wala wevi hawavunji wala hawaibi; kwa kuwa hazina yako ilipo, ndipo utakapokuwapo na moyo wako."

Agizo ni hili "Jiwekeeni hazina mbinguni." Ni kwa faida yako kujipatia utajiri wa mbinguni. Huo tu, katika vitu vyote ulivyo navyo, ndio wako kabisa. Hazina iwekwayo mbinguni haiwezi kuharibika. Moto wala dhoruba haviwezi kuifutilia mbali; mwivi hawezi kuichukua, nondo wala kutu haiwezi kuiharibu; kwa kuwa iko mkononi mwa Mungu.

Hazina hii, ambayo Kristo ameona kwamba thamani yake haipimiki ndiyo "utajiri wa utukufu wa urithi wake katika watakatifu." Waefeso 1:18. Wafuasi wa Kristo wana itwa vito vyake vya thamani, hazina yake ya thamani na ya pekee. Asema, "Watakuwa kama vito vya taji." "Nitafanya wanadamu kuadimika (kuwa wa thamani) kuliko dhahabu safi, na watu kuliko dhahabu ya ofiri." Zekaria

9:16; Isaya 13:12. Kristo huwatazama watu wake wakiwa katika usafi na

ukamilifu wao kuwa ndio ujira wa mateso yake yote, kujidhili kwake, na upendo wake; huwaona pia kama ni utimilifu wa utukufu wake; Kristo ndiye Mkuu ambaye utukufu wote watoka kwake.

Nasi tumeruhusiwa kuungana naye katika kazi kubwa ya wokovu, na kushirikiana naye katika utajiri aliojipatia kwa ajili ya kufa kwake na mateso yaliyompata. Mtume Paulo alipowaandikia Wakristo wa Thesalonike, alisema: "Maana tumaini letu, au furaha yetu, au taji ya kujionea fahari, ni nini? Je! si ninyi, mbele za Bwana wetu Yesu, wakati wa kuja kwake? Maana ninyi ndinyi utukufu wetu, na furaha yetu." 1 Wathesalonike 2:19,20. Hii ndiyo ile hazina ambayo Kristo hutuamuru tuishughulikie kuipata. Tabia njema ndiyo mavuno makubwa ya maisha ya binadamu. Kila neno na kila tendo ambalo, kwa neema ya Kristo, linaelekeza mawazo ya mtu mbinguni na kila jitihada ya kujenga tabia kama ile ya Kristo, huko ndiko kujiwekea hazina mbinguni.

Hazina ilipo, ndipo utakapokuwapo na moyo. Katika kila jitihada ya kuwanufaisha wengine, tunanufaishwa na sisi wenyewe. Yeye atoaye pesa zake au muda wake kwa ajili ya kuieneza Injili, hana budi kuyatia mapenzi yake na maombi yake katika kazi ile, na kuwaombea wale watakaosikia habari za Injili; anavutwa kuwapenda wengine, pia anaamshwa moyoni mwake kujitoa zaidi kwa Mungu, ili awezeshwe kuwatendea mema mengi sana.

Na katika siku ile ya mwisho, mali yote ya dunia itakapoharibika, yeye aliyejiwekea hazina mbinguni ataiona ile aliyoichuma kutokana na maisha yake. Kama tutakuwa tumeyazingatia maneno ya Kristo, basi, tutakapokusanyika kule mbele ya kiti cha enzi, kikubwa, cheupe, tutawaona watu ambao wameokolewa kwa ajili ya kazi yetu; tutasikia jinsi mtu fulani alivyowaokoa wengine, na wale walivyowaleta wengine tena—mkutano mkubwa wa watu ambao wamejaliwa kufika mahali kule kwenye raha kwa ajili ya kazi yetu, kule wataweka chini, miguuni pa Yesu, taji zao wapate kumsifu milele hata milele. Mtenda kazi wa Kristo atafurahi kama nini akiwaona wateule hawa wanaoshiriki utukufu wa Mwokozi! Mbinguni patakuwa mahali pa furaha kama nini kwa waaminifu waliojibidisha katika kazi ya kuziokoa roho za watu!

"Basi mkiwa mmefufuliwa pamoja na Kristo, yatafuteni yaliyo juu, Kristo aliko, ameketi mkono wa kuume wa Mungu." Wakolosai 3:1.

"Jicho Lako Likiwa Safi, Mwili Wako Wote Utakuwa na Nuru." Mathayo 6:22.

Kuwa na nia moja tu, kumcha Mungu kwa moyo wote, hiyo ndiyo hali iliyooneshwa kwa maneno haya ya Mwokozi. Kusudi na liwe safi na lisiyumbe

katika kuijua ile kweli na kuitii kwa hali iwayo yote, ndipo utaangazwa moyoni

*One-Soul Audience Ministry*

kwa nuru itokayo juu. Utauwa wa kweli huanza wakati ule maridhiano yote na dhambi yanapokoma kabisa. Ndipo lugha ya moyo wako itakuwa ni ile ya mtume Paulo: “Natenda neno moja tu; nikiyasahau yaliyo nyuma, nikiyachuchumilia yaliyo mbele; nakaza mwendo, niifikilie mede ya thawabu ya mwito mkuu wa Mungu katika Kristo Yesu.” “Naam, zaidi ya hayo, nayahesabu mambo yote kuwa hasara kwa ajili ya uzuri usio na kiasi wa kumjua Kristo Yesu, Bwana wangu; ambaye kwa ajili yake nimepata hasara ya mambo yote nikiyahesabu kuwa kama mavi ili nimpate Kristo.” Wafilipi 3:13,14,8.

Lakini jicho lako likipofushwa kwa ajili ya kujipenda wewe mwenyewe, basi, ni giza tupu. “Jicho lako likiwa bovu, mwili wako wote utakuwa na giza.” Lilikuwa ni giza la namna hii lililowatia Wayahudi moyo wa ukaidi usioweza kuwa na imani, likifanya uwezekano usiwepo kwao kufahamu na kupendezwa na tabia na kazi yake Yeye aliyekuja kuwaokoa kutoka katika dhambi zao.

Kushindwa na majaribu huanza wakati ule unapouacha moyo wako kusitasita, yaani, kule kutokuwa thabiti kwako katika kumtumaini Mungu. Tusipochagua kujitoa kabisa kwa Mungu, tutakuwa tumo gizani. Tunapokaa bila kujitoa tunaacha mlango wazi ambao kwa huo Shetani anaweza kuingia na kutupoteza kwa majaribu yake. Ajua kwamba akiweza kupofusha macho yetu, hata jicho letu la imani lisiweze kumwona Mungu, basi, hakitakuwako kizuizi cho chote dhidi ya dhambi.

Tamaa mbaya ikishinda moyoni, inaonesha kuwa umedanganywa na Shetani. Kila mara mtu anapotimiza ile tamaa mbaya anazidi kumchukia Mungu moyoni mwake. Katika kufuata njia aliyoichagua Shetani, tunazungukwa na vivuli vya uovu, na kila hatua tunayokwenda inatuingiza katika giza nene zaidi na kuzidisha upofu wa moyo wetu.

Sheria ile ile inatumika katika ulimwengu wa kiroho kama inavyotumika katika ulimwengu wa asili. Yeye anayedumu kukaa gizani, mwishowe atapofuka macho. Giza nene kuliko lile la usiku wa manane limemfungia ndani; na kwake mwanga mkali sana wa adhuhuri hauwezi kumletea nuru yo yote. Yeye “yu katika giza, tena anakwenda katika giza, wala hajui aendako, kwa sababu giza imempofusha macho.” 1 Yohana 2:11. Kwa kuendelea kwa ushupavu kupenda maovu moyoni, kutojali kwa makusudi mazima kusihi kwa Mungu mwenye upendo, mwenye dhambi anapoteza upendo wa kutenda mema, kumtaka Mungu, yaani, anapoteza uwezo ule ule hasa wa kupokea nuru kutoka mbinguni. Mwaliko wa neema bado umejaa upendo, nuru inang’aa sana kama ilivyomzukia mwanzoni moyoni mwake; lakini sauti hiyo inaanguka katika masik io ya kiziwi, nuru inayaangazia macho yaliyopofuka.

Mtu awaye yote haachwi kabisa na Mungu, yaani, haachwi afuate njia zake mwenyewe, kadiri tumaini linavyozidi kuwapo la wokovu wake. “Mwanadamu humwacha Mungu, si Mungu kumwacha yeye.” Baba yetu aliye mb inguni huendelea kutufuata na kutuita na kutuonya na kutuahidi huruma zake, mpaka imebainika kwamba kuzidi kutupa nafasi nyingi na upendeleo ni bure kabisa. Kwa kumpinga Roho wa Mungu leo, mtu anatayarisha njia ya kuipinga nuru kwa mara ya pili inapomjia kwa nguvu nyingi zaidi. Hivyo anaendelea toka hatua moja ya kupinga kwenda nyingine, mpaka hatimaye nuru itashindwa kumgusa, naye atakoma kupokea kwa kiwango cho chote mvuto wa Roho wa Mungu. Ndipo hata “ile nuru iliyomo ndani yako” inageuka na kuwa giza. Kweli ile tuijuayo hasa inakuwa imepotoka kiasi cha kuzidisha upofu wa moyo wetu.

“Hakuna Mtu Awezaye Kutumikia Mabwana Wawili.”
Mathayo 6:24.

Kristo hasemi kwamba mtu hatataka kuwatumikia au hatawatumikia mabwana wawili, bali asema kwamba mtu hawezi. Mambo yanayomhusu Mungu na mambo yanayohusiana na mali hayawezi kupatana wala kushirikiana. Pale ambapo dhamiri ya Mkristo inamwonya kuacha kufanya jambo fulani, kujikana nafsi, kusimama, ndipo pale pale ambapo mtu wa kidunia anavuka mpaka, anatimiza tamaa zake mwenyewe. Upande mmoja wa mpaka huo yupo mfuasi wa Kristo anayejikana nafsi; upande mwingine ni mtu wa kidunia apendaye kujifurahisha kwa anasa za dunia, apendaye kufuata mitindo ya walimwengu, ajiingizaye katika mambo ya kipuzi na kupendelea kufanya anasa zilizokatazwa. Upande ule wa mpaka Mkristo hawezi kwenda.

Hakuna mtu awezaye kusimama katikati asikae upande huu wala upande huu; hakuna kundi la watu lisimamalo katikati, ambalo halimpendi Mungu wala halimtumikii adui yule wa haki. Kristo hana budi kuishi ndani ya wajumbe wake wa kibinadamu, na kufanya kazi akitumia akili zao, na kutenda akitumia nguvu zao. Mapenzi yao sharti yatawaliwe na mapenzi yake; ni lazima wafanye kazi pamoja na Roho wake.Ndipo wanakuwa si wao tena walio hai, bali ni Kristo aliye hai ndani yao. Mtu asiyejitoa kabisa kwa Mungu, yuko chini ya mamlaka mengine, anasikiliza sauti nyingine, ambayo mashauri yake yanahitilafiana kabisa na yale ya Mungu. Kutoa huduma nusu nusu humweka mjumbe wa kibinadamu upande wa yule adui kuwa rafiki wa majeshi yale ya giza. Watu wanaojidai kuwa ni askari wa Kristo, na huku wanafanya urafiki na jamii ya Shetani na kumsaidia wakiwa upande wake, wanajidhihirisha kuwa ni maadui wa Kristo. Wanazisaliti amana takatifu walizokabidhiwa. Watu hao huwa kama kiungo kati ya Shetani na askari wa kweli wa Kristo, na kwa njia ya watu hao adui hufanya kazi daima kuirubuni mioyo ya askari wa Kristo.

Ngome ya ufisadi yenye nguvu kuliko zote katika ulimwengu wetu siyo maisha maovu sana ya mwenye dhambi aliyetupwa, ama mhuni aliyepoteza heshima yake miongoni mwa watu; bali ni maisha ya yule anayeonekana kuwa mnyofu, mwenye heshima, mwenye tabia nzuri, lakini ambaye ndani yake dhambi moja inatunzwa, ufisadi mmoja unaendekezwa. Mfano kama huo, kwa mtu yule anayejitahidi sirini kupigana na jaribu fulani kubwa sana, huku akitetemeka ukingoni kabisa mwa genge refu, ni mmojawapo wenye nguvu nyingi sana kumshawishi atende dhambi. Mtu ambaye amejaliwa kufahamu mawazo ya hali ya juu kuhusu maisha na kweli na heshima inayotakiwa, lakini kwa makusudi anaihalifu amri moja ya sheria takatifu ya Mungu, amepotosha vipawa vyema vya Mungu na kuvifanya viwe kishawishi cha kuwavuta wengine dhambini. Akili isiyo kifani, talanta, moyo wa huruma, hata na matendo ya ukarimu na fadhili, yaweza kutumiwa na Shetani kuwa chambo cha kuwashawishi wengine kwenda na kuanguka kwenye genge la maangamizi katika maisha haya na maisha yale yajayo.

“Msiipende dunia, wala mambo yaliyomo katika dunia. Mtu akiipenda dunia kumpenda Baba hakumo ndani yake. Maana kila kilichomo duniani, yaani tamaa ya mwili, na tamaa ya macho, na kiburi cha uzima, havitokani na Baba, bali vyatokana na dunia.” 1 Yohana 2:15,16.

Msisumbukie Maisha Yenu.” Mathayo 6:25.

Yeye aliyekupa uzima ajua jinsi unavyohitaji chakula ili kuyadumisha maisha. Yeye aliyeumba mwili afahamu jinsi unavyohitaji mavazi. Je, yeye aliyetoa kipawa kikubwa hatatoa pia kile kinachohitajika ili kukikamilisha?

Yesu aliwaonesha wasikilizaji wake ndege wa angani walioimba nyimbo tamu bila kusumbuka moyoni, kwa kuwa “hawapandi, wala hawavuni;” lakini Baba mkuu awaruzuku. Naye auliza, “Ninyi je! si bora kupita hao?”

“Hakuna shomoro aangukaye chini bila yeye kumjali, Hakuna mtu ainamaye chini bila Yesu kujua;
Kwa maana yeye yu pamoja nasi kila mahali,
Naye huona kila chozi chungu linalobubujika.
Naye kamwe, kamwe, kamwe
Hatamwacha mtu anayemtumaini yeye daima.”

Mbavuni mwa vilima na mashambani palikuwa na maua mengi yenye kung’aa, na Yesu, asubuhi ile yenye umande mpya, aliyaelekezea kidole na kusema, “Fikirini maua ya mashamba, jinsi yameavyo.” Kwa akili zao wanadamu waweza kufanya

taswira ya maua na rangi zao, lakini ni nani awezaye kuyafanyiza maua au majani

yapate kumea? Kila ua lililo kando ya njia liko pale kwa nguvu ile ile iliyoziweka dunia za nyota kule juu. Viumbe vyote vyapata uzima mmoja utokao kwa Mungu mwenyewe. Maua ya mashamba yamevikwa kwa mkono wake uzuri ulio bora kuliko ule wa mavazi ya fahari ya wafalme wa dunia. "Basi, ikiwa Mungu huyavika hivi majani ya kondeni, yaliyopo leo, na kesho hutupwa kalibuni, Je! hatazidi sana kuwavika ninyi, enyi wa imani haba?" Yeye aliyeyaumba maua, na kumpa shomoro wimbo wake, ndiye asemaye, "Fikirini maua," na tena, "Waangalieni ndege wa angani." Kwa kuutazama uzuri wa viumbe vya asili utaweza kuifahamu hekima ya Mungu zaidi ya wanavyoifahamu wataalamu. Juu ya majani ya ua yenye rangi, Mungu ameandika ujumbe kwa ajili yako, ameandika katika lugha ambayo moyo wako unaweza tu kuisoma unapoacha kujifunza mafundisho ya kutomtumainia yeye na kujipenda binafsi na kuwa na masumbufu yanayokula wewe. Kwa nini Mungu amekupa wewe ndege waimbao na maua mazuri, je, si kwa kusudi la kukujulisha upendo wa Baba yetu unaobubujika kutoka moyoni mwake, ambao ungeiangazia njia yako ya maisha na kukuletea furaha? Yale yote ambayo yangehitajika kwa maisha yako yangekuwa yako pasipo hayo maua na ndege, lakini Mungu hakuridhika kukupa kile ambacho kingetosheleza tu riziki ya maisha. Amejaza uzuri uwezao kuuona duniani na angani na katika mbingu ili kukupasha wewe juu ya wazo lake la upendo alilo nalo kwako wewe. Uzuri wa vitu vyote alivyoviumba ni kama kianga kidogo tu kitokacho kwenye mng'ao wa utukufu wake mkuu. Ikiwa ametumia akili zake nyingi hivi kuvifanya viumbe vya ulimwengu huu, kwa ajili ya kukupa wewe raha na furaha, je, waweza kuwa na mashaka kuwa hatakupa kila mbaraka unaouhitaji?

"Fikirini maua ya mashamba." Kila ua linalofunua majani yake kuelekea kwenye mwanga wa jua huzitii kanuni kuu zile zile zilizowekwa na Mungu kuziongo za nyota, na maisha yake huwa mepesi, mazuri, na matamu kama nini! Kwa njia ya maua, Mungu anataka kuyavuta mawazo yetu kuelekea kwenye uzuri wa tabia inayofanana na ile ya Kristo. Yeye aliyeyapa maua uzuri kama huo, anataka zaidi sana kwamba moyo uvikwe uzuri wa tabia yake Kristo.

Fikirini, Yesu asema, jinsi maua ya mashamba yameavyo; jinsi kutoka katika ardhi baridi, ya giza, au kutoka katika matope chini ya mto, mimea inavyojitokeza katika uzuri wake na kuwa na harufu nzuri. Nani angeota kwamba uwezekano wa uzuri uko kwa shina la ovyo ovyo la kikahawia la yungiyungi? Lakini uzima wa Mungu, uliojificha ndani yake, unapojitokeza kwa amri yake juu ya mvua na mwanga wa jua, wanadamu wanashangaa sana kuona uzuri wake na kupendeza kwake. Hivyo ndivyo uzima wa Mungu utakavyofunuliwa katika maisha ya kila mwanadamu anayejitia chini ya uongozi wa neema ya Mungu, itolewayo bure kama mvua na mwanga wa jua, na kuleta mbaraka kwa wote. Neno la Mungu ndilo liyaumbayo maua, pia neno lilo hilo ndilo litakalofanya kazi ndani yako

kuzaa matunda ya Roho wake.

Sheria ya Mungu ni sheria ya upendo. Amekuzungushia vitu vizuri kusudi kukufundisha kwamba umewekwa hapa duniani si kwa kuiangalia nafsi yako tu, kulima na kujenga, kufanya kazi ya taabu na kusokota nyuzi; bali upo hapa kuyafanya maisha yawe machangamfu na ya furaha na mazuri kwa upendo wa Kristo—kama maua, uwaletee wengine furaha katika maisha yao kwa huduma yako ya upendo.

Akina baba na mama, acheni watoto wenu wajifunze habari za maua. Nendeni nao makondeni na mashambani na chini ya miti yenye majani mengi, wafundisheni kusoma katika viumbe vya asili ujumbe wa upendo wa Mungu. Hebu mawazo yao juu yake yafungamanishwe na ndege na ua na mti. Zielekezeni fikara za watoto ili, kwa kila kitu kizuri cha kupendeza wanachokiona, wapate kuona jinsi Mungu awapendavyo. Isifie kwao dini yenu kwa uzuri wake. Sheria ya wema na iwe ulimini mwenu.

Wafundisheni watoto kwamba kwa sababu ya upendo mkuu wa Mungu tabia zao zinaweza kubadilika na kufanana na yake. Wafundisheni kuwa Mungu ataka wawe na maisha mazuri, kama uzuri ule wa maua. Wafundisheni, wanapochuma maua yenye harufu nzuri, kwamba yeye aliyeyafanya maua hayo ni mzuri kuliko hayo. Kwa njia hiyo vikonyo vya mioyo yao vitajizungusha kumzunguka yeye. Yeye ambaye “ndiye mzuri sana pia,” kwao atakuwa rafiki wanayemfahamu daima, na maisha yao yatabadilika na kufanana na usafi wa maisha yake.

“Utafuteni Kwanza Ufalme Wake.” Mathayo 6:33.

Watu walioyasikia maneno haya ya Kristo, bado walikuwa na hamu wakitazamia kusikia tangazo fulani juu ya ufalme wake duniani. Yesu alipokuwa akiwafunulia mambo ya mbinguni, jambo ambalo walilifikiri sana lilikuwa ni hili: Kushirikiana naye kutazidishaje mafanikio yetu hapa duniani? Yesu aliwaonesha kwamba kule kuyasumbukia sana mambo ya kidunia kuliwafanya wafanane na mataifa waliokuwa kandokando yao, na kuishi kana kwamba hakuna Mungu anayevishughulikia sana viumbe vyake.

“Hayo yote,” Yesu alisema, “ndiyo watafutayo mataifa ya duniani.” “Baba yenu wa mbinguni anajua ya kuwa mnahitaji hayo yote. Bali utafuteni kwanza ufalme wake, na haki yake; na hayo yote mtazidishiwa.” Luka 12:30; Mathayo 6:32,33. Nimekuja kuwafunulia ninyi ufalme wa upendo na haki na amani. Ifungueni mioyo yenu kuupokea ufalme huu, na mioyoni mwenu kutenda kazi yake liwe jambo kubwa sana. Ingawa ni ufalme wa kiroho, msiogope kuwa mtakosa kupata riziki zenu kwa maisha haya. Yeye aliye na mamlaka yote mbinguni na duniani atawapeni mahitaji yenu.

Yesu hatupi uhuru wa kutouona umuhimu wa kuwa na juhudi, bali atufundisha kwamba yatupasa kumweka Yeye kuwa wa kwanza, na wa mwisho na aliye bora kuliko wote katika kila jambo. Tusifanye shughuli iwayo yote, tusitafute kazi yo yote itupendezayo, tusitafute anasa yo yote ambayo ingezuia utendaji wa haki yake katika tabia yetu na maisha yetu. Lo lote tufanyalo, tulifanye kwa moyo, kama kwa Bwana.

Yesu, alipokuwa hapa duniani, aliyatukuza maisha katika nyanja zake zote kwa kuuweka utukufu wa Mungu mbele ya wanadamu, na kwa kukitiisha kila kitu chini ya mapenzi ya Baba yake. Tukiuiga mfano wake, ahadi yake kwetu ni kwamba mambo yote yanayohitajika katika maisha haya tuta"zidishiwa." Umaskini au utajiri, ugonjwa au afya, ujinga au hekima—hali hizi zote zinaruzukiwa katika ahadi ya neema yake.

Mikono ya milele ya Mungu humkumbatia yule anayemgeukia yeye ili kupata msaada wake, ingawa ni mdhaifu mno. Vitu vya thamani vilivyo vilimani vitatoweka; lakini yeye aishiye kwa ajili ya Mungu atakaa pamoja naye. "Dunia inapita, pamoja na tamaa zake, bali yeye afanya ye mapenzi ya Mungu adumu hata milele." 1 Yohana 2:17. Jiji lile la Mungu litafungua malango yake kumpokea yule aliyejifunza alipokuwa hapa duniani kumtegemea Mungu kwa uongozi wake na hekima, kwa faraja na tumaini, kati ya hasara na mateso. Huyo atakaribishwa na malaika kwa nyimbo za shangwe, na matunda ya mti wa uzima yatakuwa yake. "Maana milima itaondoka, na vilima vitaondolewa; bali wema wangu hautaondoka kwako, wala agano langu la amani halitaondolewa; asema Bwana akurehemuye." Isaya 54:10.

"Basi Msisumbukie ya Kesho;... Yatosha Kwa Siku Maovu Yake." Mathayo 6:34.

Kama wewe umejitoa kuwa wa Mungu, kufanya kazi yake, basi, huna haja ya kusumbukia ya kesho. Yeye, ambaye wewe u mtumishi wake, ajua mwisho tangu mwanzo. Mambo ya kesho, ambayo yamefichwa machoni pako, ni wazi machoni pake Mwenyezi Mungu.

Tunapojichukulia mikononi mwetu uongozi wa mambo yale yatupasayo kufanya, na kutegemea hekima yetu wenyewe kwa mafanikio, tunachukua mzigo tusiopewa na Mungu, na kujaribu kuuhimili pasipo msaada wake. Tunajitwalia wenyewe madaraka yanayomhusu Mungu, na hivyo kweli tunajiweka mahali pake. Kweli tunaweza kuhangaika, na kutazamia hatari na hasara; kwa kuwa bila shaka mambo hayo yatatujia. Lakini kama tunasadiki kabisa ya kuwa Mungu anatupenda na ameazimia kutufanyia mema, tutaacha kuwa na wasiwasi juu ya mambo ya wakati ujao. Tutamtumainia Mungu kama vile mtoto anavyomtumainia

mzazi anayempenda. Ndipo masumbuko na mahangaiko yetu yatatoweka; kwa sababu mapenzi yetu yamemezwa na mapenzi ya Mungu.

Kristo hajatoa ahadi yo yote kwetu ya kutupa leo msaada wa kuihimili mizigo ya kesho. Yeye amesema, “Neema yangu yakutosha” (2 Wakorintho 12:9); lakini, kama vile mana ilivyotolewa kule jangwani, ndivyo na neema yake inavyotolewa siku kwa siku kukidhi ma hitaji ya siku hiyo. Kama makutano ya Israeli katika maisha yao ya kusafiri, twaweza kupata kila asubuhi mkate utokao mbinguni kutosha kuturidhisha kwa siku hiyo. Siku moja tu ndiyo yetu, na kwa siku hiyo inatupasa kuishi kwa ajili ya Mungu.

Kwa siku moja hiyo inatupasa kuweka makusudi yetu yote na mipango yetu yote mkononi mwake Kristo, tukimtwika yeye fadhaa zetu zote, kwa maana yeye hujishughulisha sana kwa mambo yetu, na kumkumbuka Mungu katika huduma yetu. “Maana nayajua mawazo ninayowawazia ninyi, asema Bwana, ni mawazo ya amani, wala si ya mabaya, kuwapa ninyi tumaini siku zenu za mwisho.” “Bwana Mungu,... asema hivi, kwa kurudi na kustarehe mtaokolewa; nguvu zenu zitakuwa katika kutulia na kutumaini.” Yeremia 29:11; Isaya 30:15.

Kama ukimtafuta Bwana na kuongoka kila siku; kama kwa uchaguzi wako mwenyewe wa kiroho utakuwa huru na mwenye furaha katika Mungu; kama kwa furaha unaukubali kwa moyo wako mwito wake na unakuja ukiwa umevaa nira ya Kristo,—nira ya utii na utumishi,—manung’uniko yako yote yatatulizwa, shida zako zote zitaondolewa, na matatizo yote yanayokufadhaisha, ambayo yanakukabili wewe sasa, yatafumbuliwa.

# SURA YA 5

# SALA YA BWANA

"Basi Ninyi Salini Hivi." Mathayo 6:9.

SALA ya Bwana ilitolewa na Mwokozi wetu mara mbili; mara ya kwanza kwa makutano katika mahubiri Mlimani, tena baada ya miezi kadhaa kwa wanafunzi peke yao. Kwa muda mfupi wanafunzi hawakuwa pamoja na Bwana; na waliporudi walimkuta akiwa amezama katika kuongea na Mungu. Akionekana kana kwamba hajui kwamba walikuwa pale, akaendelea kuomba kwa sauti. Uso wa Mwokozi uliangazwa kwa nuru ya mbinguni. Alionekana kama yuko mbele zake yule Asiyeonekana; na maneno yake yalikuwa na nguvu iliyo hai, kama ya mtu aliyeongea na Mungu.

Mioyo ya wanafunzi wake waliokuwa wakisikiliza iliguswa sana. Walikuwa wameona mara nyingi jinsi alivyotumia saa nyingi peke yake akiongea na Babaye. Alizitumia siku zake kuwahudumia makutano waliomzunguka na kumsonga, na kufichua hila za waalimu wao wakuu za mafundisho yao ya uongo, na kazi yake hiyo isiyokoma ilimwacha akiwa amechoka chakari, hata mama yake na ndugu zake, pamoja na wanafunzi wake, waliogopa kwamba atayakatisha maisha yake. Lakini aliporudi kutoka katika saa zake za kusali, zilizokuja mwisho wa siku yake yenye kazi ngumu, waliona jinsi uso wake ulivyokuwa na utulivu, tena alionekana kwamba yu katika hali ya kuburudika. Baada ya kutumia saa nyingi mbele za Mungu na kuongea naye, alitoka kila siku asubuhi kuwapelekea wanadamu nuru ya mbinguni. Wanafunzi wake katika fikara zao walikuwa wameunganisha nyakati zake za kusali na zile nguvu za maneno yake na kazi zake. Basi, walipozisikia dua zake, mioyo yao iliingiwa na kicho na kunyenyekezwa. Alipomaliza kuomba, ilikuwa ni kutokana na haja kubwa waliyokuwa nayo mioyoni mwao walipomaka, na kusema, "Bwana, tufundishe sisi kusali." Luka 11:1.

Yesu hawapi namna mpya ya sala. Ile aliyowafundisha zamani anairudia, kana kwamba angesema hivi: Yawapasa mfahamu ile niliyokwisha kuwapeni zamani. Ina maana yenye kina ambayo ninyi bado hamjaielewa.

Walakini, Mwokozi hatuwekei mipaka kutumia maneno yale yale tu. Lakini, kama alivyoshiriki hali ya kibinadamu, alitoa mawazo yake juu ya sala iliyo kamili—maneno rahisi mno yawezayo kutumiwa na mtoto mdogo, lakini yanayojumuisha mambo yote ambayo maana yake haiwezi kamwe kufahamika kikamilifu na watu wenye akili nyingi sana. Tunafundishwa kuja kwa Mungu tukimheshimu kwa shukrani zetu, tukimjulisha mahitaji yetu, tukiziungama dhambi zetu, na kudai rehema yake kulingana na ahadi yake.

“Msalipo, Semeni, Baba Yetu.” Luka 11:2.

Yesu atufundisha tumwite Baba yake Baba yetu. Yeye haoni haya kutuita sisi ndugu zake. (Waebrania 2:11). Moyo wa Mwokozi u tayari sana, una shauku kuu kutukaribisha sisi kama watu wa familia ya Mungu, hata katika maneno yale ya kwanza kabisa tunayopaswa kutumia kumwendea Mungu anatupa uthibitisho wa uhusiano wetu na Mungu, yaani, “Baba yetu.”

Hapa ni tangazo la ile kweli ya ajabu, ni jambo la kututia moyo na kutufariji sana, kwamba Mungu atupenda sisi kama vile ampendavyo Mwanawe. Hivyo ndivyo alivyosema Yesu katika sala yake ya mwisho alipowaombea wanafunzi wake. “Ukawapenda wao kama ulivyonipenda mimi.” Yohana 17:23.

Dunia hii ambayo Shetani amedai kuwa ni yake tena ameitawala kwa udhalimu na ukatili, Mwana wa Mungu, kwa ushindi wake mmoja mkubwa, ameizingira kwa upendo wake, na kuiunganisha tena na kiti cha enzi cha Yehova. Makerubi na Maserafi, na majeshi yasiyohesabika ya dunia zile zisizoanguka dhambini, waliimba nyimbo za shangwe kumsifu Mungu na Mwana-Kondoo ushindi ule ulipothibitishwa. Walifurahi kwa kuwa ilifunguliwa njia ya wokovu kwa wanadamu waliokuwa wameanguka dhambini, na kwa kuwa dunia hii ingekombolewa kutoka katika laana ya dhambi. Basi, je, si wangefurahi zaidi sana wale ambao ni walengwa wa upendo wa ajabu sana kama huo!

Twawezaje kuwa na wasiwasi na mashaka moyoni, na kujiona kuwa sisi ni yatima? Ilikuwa ni kwa ajili ya wale waliokuwa wameihalifu sheria Yesu alitwaa asili ya binadamu; akawa kama sisi, ili tupate kuwa na amani ya milele na matumaini. Tunaye Mwombezi mbinguni, na mtu ye yote anayemkubali kuwa Mwokozi wake, haachwi yatima kuchukua mwenyewe mzigo wa dhambi zake.

“Wapenzi, sasa tu wana wa Mungu.” “Kama tu watoto, basi, tu warithi; warithi wa Mungu, warithio pamoja na Kristo; naam, tukiteswa pamoja naye ili tupate na kutukuzwa pamoja naye.” “Wala haijadhihirika bado tutakavyokuwa; lakini twajua ya kuwa atakapodhihirishwa, tutafanana naye; kwa maana tutamwona kama alivyo.” 1 Yohana 3:2; Warumi 8:17.

Hatua ya kwanza kabisa katika kumkaribia Mungu ni kuujua na kuuamini upendo alio nao kwetu sisi (1 Yohana 4:16); kwa maana ni kwa njia ya kuvutwa na upendo wake sisi tunaongozwa kuja kwake.

Katika kuufahamu upendo wa Mungu tutaongozwa kujihini na kuachana na ubinafsi. Tunapomwita Mungu Baba yetu, tunatambua ya kuwa watoto wake

wote ndio ndugu zetu. Sisi sote ni sehemu ya mtandao mkubwa wa binadamu,

wote tu watu wa familia moja. Katika dua zetu twapaswa kuwaingiza jirani zetu pamoja na sisi wenyewe. Hakuna aombaye ipasavyo ambaye hujiombea apewe baraka yeye mwenyewe tu.

Yesu alisema kwamba Mungu, asiye na mwanzo wala mwisho, huwapa ninyi upendeleo wa kumkaribia kwa jina la Baba. Fahamuni basi, maana yake yote. Hakuna mzazi wa kibinadamu ambaye amemsihi mwana wake mpotevu kwa bidii nyingi sana kama vile Yeye aliyewaumba ninyi anavyomsihi mhalifu wa sheria yake. Hakuna moyo wa kibinadamu wenye huruma na upendo, ambao umepata kumfuatilia yule asiyetaka kutubu na kutoa mwito wa upendo kama huo. Mungu yumo ndani ya kila nyumba; husikia kila neno linenwalo, husikiliza maombi yote yatolewayo, huonja huzuni na mambo ya kukatisha tamaa yampatayo kila mtu, huyaona mambo anayotendewa baba, mama, ndugu, rafiki, na jirani. Anajali na kutupatia mahitaji yetu, na pendo lake na rehema zake na neema yake daima huja kwetu kukidhi mahitaji yetu.

Lakini mkimwita Mungu Baba yenu, basi mwakubali kwamba ninyi ni watoto wake, mtakaoongozwa na hekima yake, na kumtii katika mambo yote, mkijua hakika kwamba upendo wake haubadiliki. Mtaukubali mpango wake kwa maisha yenu. Kama watoto wa Mungu, mtaishikilia heshima yake, tabia yake, familia yake, kazi yake, kama mambo yapendezayo sana katika moyo wenu. Itakuwa furaha yenu kuutambua na kuuheshimu uhusiano wenu na Baba yenu na kila mtu wa familia yake. Mtafurahia kufanya tendo lo lote, hata liwe duni jinsi gani, litakalomtukuza Yeye, au kuwanufaisha ndugu zenu.

“Uliye mbinguni.” Yeye ambaye Kristo atuagiza kumwangalia kama “Baba yetu,” “yuko mbinguni; alitakalo lote amelitenda.” Katika ulinzi wake twaweza kuwa na utulivu wa moyo, na kusema, “Siku ya hofu yangu nitakutumaini Wewe.” Zaburi 115:3; 56:3.

“Jina Lako Litukuzwe.” Mathayo 6:9.

Ili kulitukuza jina la Bwana inatakiwa kwamba maneno yote tunayotumia kwa kumnena Mwenyezi Mungu yasemwe kwa heshima na kicho. “Jina lake ni takatifu la kuogopwa.” Zaburi 111:9. Haitupasi kamwe kwa njia yo yote ile kuvitaja bure vyeo au majina ya Mungu. Katika kusali tunakuja mbele zake Yeye Aliye juu; na yatupasa kuja mbele zake kwa kicho kitakatifu. Malaika hufunika nyuso zao mbele zake. Makerubi na maserafi wanaong’aa na watakatifu hukikaribia kiti chake cha enzi kwa heshima kuu. Basi, si zaidi sana sisi, wanadamu tunaokufa, wenye dhambi, inatupasa tuje mbele zake Bwana, Muumbaji wetu, kwa kicho!

Lakini kulitukuza jina la Bwana kuna maana zaidi ya hiyo. Kama walivyofanya Wayahudi katika siku za Kristo, hata sisi pia pengine twaweza kumtolea Mungu heshima nyingi sana kwa nje, na huku tukilinajisi jina lake daima. “Jina la Bwana” ni “mwingi wa huruma, mwenye fadhili, si mwepesi wa hasira, mwingi wa rehema na kweli;... mwenye kusamehe uovu na makosa na dhambi.” Kutoka 34:5-7. Imeandikwa hivi juu ya kanisa la Kristo: “Na jina lake atakaloitwa ni hili, Bwana ni haki yetu.” Yeremia 33:16. Jina hili linawekwa juu ya kila mfuasi wa Kristo. Hilo ndilo urithi wa mwana wa Mungu. Familia yake huitwa kwa jina la Baba yao. Wakati ule Israeli walipokuwa katika mahangaiko makubwa na dhiki kubwa, nabii Yeremia aliomba, “Wewe, Bwana u katikati yetu, nasi tunaitwa kwa jina lako; usituache.” Yeremia 14:9.

Jina hili linatukuzwa na malaika wa mbinguni, na wakazi wa dunia zile zisizoanguka dhambini. Unaposali hivi, “Jina lako litukuzwe,” unaomba kwamba litukuzwe hapa duniani, yaani, litukuzwe ndani yako wewe. Mungu amekukiri mbele ya wanadamu na mbele ya malaika kuwa wewe ni mtoto wake; omba kwamba usiliaibishe “jina lile zuri mliloitwa” nalo. Yakobo 2:7. Mungu anawatuma duniani kama wajumbe wake. Katika kila tendo la maisha yenu hamna budi kulidhihirisha jina la Mungu. Dua hili linawataka ninyi mwe na tabia yake. Hamwezi kulitukuza jina lake, yaani, hamwezi kumwakilisha kwa walimwengu, isipokuwa kama kwa maisha na tabia yenu mnayawakilisha maisha halisi na tabia ya Mungu. Hilo mnaweza tu kufanya kwa kuipokea neema na haki ya Kristo.

“Ufalme Wako Uje.” Mathayo 6:10.

Mungu ndiye Baba yetu atupendaye na kututunza kama watoto wake; pia Yeye ndiye Mfalme mkuu wa malimwengu yote. Mambo yahusuyo ufalme wake ndiyo tunayopaswa kuyapenda kwa moyo wote, tena tunapaswa kufanya kazi kuuendeleza ufalme huo.

Wanafunzi wa Kristo walitazamia kuja kwa ufalme wake wa utukufu wakati ule; lakini kwa kuwapa sala hii Yesu aliwafundisha kwamba ufalme wake usingeweza kusimamishwa katika siku zile. Walitakiwa kuomba ili uje kama tukio la baadaye. Lakini pia dua hiyo ilikuwa ni ahadi kwao. Ijapokuwa wasingeweza kuuona ufalme ule ukija katika siku zao, ule ukweli kwamba Yesu aliwafanya waombe kwa ajili yake ni ushahidi kwamba kwa wakati wake Mungu ni hakika utakuja.

Ufalme wa neema ya Mungu unaendelea kusimamishwa sasa, siku kwa siku mioyo iliyokuwa imejaa dhambi na maasi inaweka chini ya mamlaka ya upendo wake. Lakini kusimamishwa kikamilifu kwa ufalme wake wa utukufu hakutafanyika

mpaka hapo Kristo atakapokuja mara ya pili duniani. “Na ufalme, na mamlaka,

na ukuu wa ufalme, chini ya mbingu zote, watapewa watu wa watakatifru wake Aliye juu." Danieli 7:27. Wataurithi ufalme waliowekewa tayari "tangu kuumbwa ulimwengu." Mathayo 25:34. Ndipo Kristo atakapotwaa mamlaka yake kuu, naye atamiliki.

Malango ya mbinguni yatainuliwa tena, na pamoja na malaika zake watakatifu elfu kumi mara elfu kumi na elfu mara elfu, Mwokozi wetu atatokea kama Mfalme wa wafalme na Bwana wa mabwana. Yehova Imanueli "atakuwa Mfalme juu ya nchi yo te; siku hiyo Bwana atakuwa mmoja na jina lake moja." "Maskani ya Mungu" yatakuwa "pamoja na wanadamu, naye atafanya maskani yake pamoja nao, nao watakuwa watu wake. Naye Mungu mwenyewe atakuwa pamoja nao." Zekaria 14:9; Ufunuo 21:3.

Lakini kabla ya kuja kwake, Yesu alisema kwamba "Habari njema ya ufalme itahubiriwa katika ulimwengu wote, kuwa ushuhuda kwa mataifa yote." Mathayo 24:14. Ufalme wake hautakuja mpaka habari njema za neema yake zimepelekwa duniani kote. Kwa hiyo, tunapojitoa kwa Mungu, na kuwaleta watu wengine kwake, tunahimiza kuja kwa ufalme wake. Wale tu wanaojitoa kufanya kazi yake, na kusema, "Mimi hapa; nitume mimi" (Isaya 6:8), ili wawafumbue vipofu macho yao, na kuwageuza watu "waiache giza na kuielekea nuru, waziache na nguvu za Shetani na kumwelekea Mungu, ili wapate msamaha wa dhambi zao, "na urithi miongoni mwao waliotakaswa" (Matendo 26:18)—hao tu ndio waombao kwa unyofu, wakisema, "Ufalme wako uje."

Mapenzi Yako Yatimizwe, Hapa Duniani Kama Huko Mbinguni." Mathayo 6:10.

Mapenzi ya Mungu yameelezwa katika maagizo ya sheria yake takatifu, tena kanuni za sheria hiyo ndizo kanuni za mbinguni. Malaika wa mbinguni hawakifikii kipeo cha juu sana cha maarifa kuliko kile cha kuyajua mapenzi ya Mungu, na kufanya mapenzi yake ndiyo huduma iliyo bora kuliko zote iwezayo kuzishughulisha nguvu zao.

Lakini huduma ya mbinguni haitolewi katika roho ya kutimiza sheria. Shetani alipoasi sheria ya Yehova, wazo la kwamba kulikuwako na sheria likawajia wale malaika karibu kama kitu fulani kilichowazindua akili zao kwa jambo lile walilokuwa hawajapata kulifikiria. Katika huduma yao malaika si kama watumwa, bali ni kama wana. Upo umoja kamili kati yao na Muumbaji wao. Utii si kazi ngumu kwao isiyopendeza. Kumpenda Mungu kunaifanya hud uma yao kuwa ya furaha. Hivyo ndani ya kila moyo akaamo Kristo, tumaini la utukufu, maneno haya yanatoa mwangwi wake tena na tena, "Kufanya mapenzi yako, Ee Mungu wangu, ndiyo furaha yangu; naam, sheria yako imo moyoni mwangu."

Zaburi 40:8.

Dua hii, “Mapenzi yako yatimizwe, hapa duniani kama huko mbinguni,” ni ombi kwamba utawala wa uovu ukome hapa duniani, kwamba dhambi ipate kuharibiwa milele, na ufalme wa haki upate kusimamishwa. Ndipo hapa duniani kama huko mbinguni itatimizwa “kila haja ya wema na kila kazi ya imani kwa nguvu” (2 Wathesalonike 1:11).

“Utupe leo Riziki Yetu.” Mathayo 6:11.

Nusu ya kwanza ya sala ambayo Yesu ametufundisha ni juu ya jina na ufalme na mapenzi ya Mungu—kwamba jina lake litukuzwe, ufalme wake upate kuimarishwa, na mapenzi yake yatimizwe. Ukisha kuweka kazi ya Mungu kuwa kitu cha kwanza moyoni mwako, ndipo unaweza kuomba kwa matumaini kwamba utapewa mahitaji yako. Ikiwa umejikana nafsi yako na kujitoa mwenyewe kwa Kristo, basi sasa wewe ni mtu wa familia ya Mungu, na vyo vyote vilivyomo nyumbani mwa Baba ni vyako. Hazina zote za Mungu zimefunuliwa kwako, za dunia ya sasa, na za ile ijayo. Huduma ya malaika, kipawa cha Roho wake, kazi za watumishi wake—hayo yote ni kwa ajili yako. Dunia, na vyote vilivyomo ndani yake, ni yako kwa kadiri inavyoweza kukuletea mema. Hata uadui wa wabaya utaonekana kwako kuwa ni mbaraka unaokungoza na kukuadilisha uwe tayari kuingia mbinguni. Ikiwa “ninyi ni wa Kristo,” basi “vyote ni vyenu.” 1 Wakorintho 3:23,21.

Lakini, wewe u kama mtoto ambaye bado hajapewa mamlaka juu ya urithi wake. Mungu hakukabidhi urithi wako wa thamani kubwa, Shetani kwa hila zake asije akakudanganya kama alivyofanya kwa watu wale wawili wa kwanza kule bustanini Edeni. Kristo ndiye anayeushika salama kwa ajili yako, mbali na pale awezapo kufika huyo mharabu. Kama mtoto, siku kwa siku utapokea kile kinachohitajika kwa siku hiyo. Yakupasa kuomba kila siku, “Utupe leo riziki yetu.” Usifadhaike moyoni usipopata ya kutosha kwa ajili ya kesho. Unalo tumaini la ahadi yake hii, “Mtakula chakula chenu na kushiba, na kuketi katika nchi yenu salama.” Mambo ya Walawi 26:5. Daudi asema, “Nalikuwa kijana nami sasa ni mzee, lakini sijamwona mwenye haki ameachwa, wala mzao wake akiomba chakula.” Zaburi 37:3,25. Mungu yule aliyewatuma kunguru wamlishe Eliya kule kwenye kijito cha Kerithi, hatakosa kumjali hata mmoja wa watoto wake waaminifu wanaojinyima. Imeandikwa hivi juu yake aendaye kwa haki: “Atapewa chakula chake; maji yake hayatakoma.” “Hawataaibika wakati wa ubaya: na siku za njaa watashiba.” “Yeye asiyemwachilia Mwana wake mwenyewe, bali alimtoa kwa ajili yetu sisi sote, atakosaje kutukirimia na mambo yote pamoja naye?” Isaya 33:16; Zaburi 37:19; Warumi 8:32. Yeye aliyepunguza masumbuko na mashaka ya mamaye mjane, na kumsaidia kuwaruzuku wale wa nyumbani mwake kule Nazareti, humhurumia kila mama anayetaabika kuwapatia

riziki watoto wake. Yeye aliyewahurumia makutano kwa sababu “walikuwa

wamechoka na kutawanyika" (Mathayo 9:36), angali anawahurumia maskini wanaosumbuka. Mkono wake umenyoshwa kwao kuwabariki; na katika sala ile ile aliyowapa wanafunzi wake, anatufundisha sisi pia kuwakumbuka maskini.

Tukiomba, "Utupe leo riziki yetu," tunaomba kwa ajili ya wengine na kwa ajili yetu wenyewe. Pia tunakiri kwamba cho chote tupewacho na Mungu si chetu sisi wenyewe tu. Mungu anatupa akitudhamini, kusudi tuwalishe wenye njaa. Katika wema wake amewaandalia maskini riziki zao. Zaburi 68:10. Naye asema hivi: "Ufanyapo chakula cha mchana au cha jioni, usiwaite rafiki zako, wala jamaa zako wenye mali ... Bali ufanyapo karamu waite maskini, vilema, viwete, vipofu, nawe utakuwa heri, kwa kuwa hao hawana cha kukulipa; kwa maana utalipwa katika ufufuo wa wenye haki." Luka 14:12-14.

"Na Mungu aweza kuwajaza kila neema kwa wingi, ili ninyi, mkiwa na riziki za kila namna sikuzote, mpate kuzidi sana katika kila tendo jema." "Apandaye haba atavuna haba; apandaye kwa ukarimu atavuna kwa ukarimu." 2 Wakorintho 9:8,6.

Katika kuomba riziki yetu ya kila siku, hatuombi tu chakula cha kuusaidia mwili wetu, bali chakula kile cha kiroho kitakachoilisha nafsi yetu hata kutupatia uzima wa milele. Yesu atwagiza, "Msikitendee kazi chakula chenye kuharibika, bali chakula kidumucho hata uzima wa milele." Yohana 6:27. Asema, "Mimi ndimi chakula chenye uzima kilichoshuka kutoka mbinguni; mtu akila chakula hiki, ataishi milele." Fungu la 51. Mwokozi wetu ndiye mkate wa uzima, na ni kwa njia ya kuutazama upendo wake, na kuupokea mioyoni mwetu, tunakula mkate ule uliotoka mbinguni.

Tunampokea Kristo kwa njia ya Neno lake, na Roho Mtakatifu ametolewa kusudi atufunulie Neno la Mungu tupate kulifahamu na kuhakikishiwa kweli zake mioyoni mwetu. Yatupasa kuomba siku kwa siku kwamba tunapolisoma Neno lake, Mungu amtume Roho wake kutufunulia sisi kweli yake itakayotutia nguvu mioyoni mwetu kukabili mahitaji ya siku hiyo.

Katika kutufundisha kuomba kila siku yale tunayohitaji—yaani, mibaraka ya kimwili na ya kiroho pia,—Mungu analo kusudi analotaka kulitekeleza litakalotuletea mema. Ataka tutambue jinsi tunavyomtegemea yeye katika kututunza sisi daima, kwa maana ataka kutuvuta kwake mwenyewe ili tuongee naye. Katika maongezi yetu haya na Kristo, kwa njia ya maombi na kuzichunguza kweli kuu na za thamani za Neno lake, sisi kama watu wenye njaa tutashibishwa; kama wenye kiu tutaburudishwa kwenye chemchemi ya maji ya uzima.

"Utusamehe Dhambi Zetu, Kwa Kuwa Sisi Nasi Tunamsamehe Kila Tumwiaye." Luka 11:4.

Yesu atufundisha kwamba sisi tunaweza tu kupata msamaha wa Mungu kwa kadiri ile ile tunavyowasamehe wengine. Ni pendo la Mungu lituvutalo kwake, na pendo hilo haliwezi kuigusa mioyo yetu bila kuamsha upendo wetu kwa ndugu zetu.

Baada ya kumaliza sala ya Bwana, Yesu alizidi kusema hivi: "Kwa maana mkiwasamehe watu makosa yao, na Baba yenu wa mbinguni atawasamehe ninyi. Bali msipowasamehe watu makosa yao, wala Baba yenu hatawasamehe ninyi makosa yenu." Yeye asiyekubali kuwasamehe wengine, amejikatilia mbali njia ile ya pekee ambayo kwayo aweza kupata rehema kwa Mungu. Tusifikiri kwamba wale waliotufanyia mabaya yanayotuumiza wasipoungama makosa yao, basi tuna haki kuwanyima msamaha wetu. Bila shaka, kwa upande wao yawapasa kunyenyekea mioyoni mwao wakitubu na kuyaungama makosa yao; lakini yatupasa kuwa na moyo wa huruma kwa wale waliotukosea, wakiungama au hata wasipoyaungama makosa yao. Ingawa wanaweza kuwa wametutia uchungu mwingi sana, tusikaribishe manung'uniko moyoni mwetu wala tusisikitike kwa ajili ya machungu waliyotutendea; bali kama vile sisi tunavyotumainia kusamehewa makosa yetu dhidi ya Mungu, ndivyo itupasavyo nasi kuwasamehe wote waliotutendea mabaya.

Lakini msamaha una maana pana zaidi ya ile inayodhaniwa na wengi. Mungu anapotoa ahadi yake kuwa "atamsamehe kabisa" mtu mbaya anayemrudia, anaongeza maneno haya, kana kwamba maana ya ahadi hiyo inapita ufahamu wetu wote tuwezao kuwa nao, anasema: "Maana mawazo yangu si mawazo yenu, wala njia zenu si njia zangu; asema Bwana. Kwa maana kama vile mbingu zilivyo juu sana kuliko nchi, kadhalika njia za ngu zi juu sana kuliko njia zenu, na mawazo yangu kuliko mawazo yenu." Isaya 55:7-9. Msamaha wa Mungu si kama tendo la hakimu tu ambalo kwalo atufanya huru tusihukumiwe. Si msamaha tu kwa ajili ya dhambi, bali ni kuongoa kutoka katika dhambi. Ni bubujiko la upendo ukomboao linalougeuza moyo kabisa. Daudi alifahamu msamaha jinsi ulivyo hasa aliposali hivi, "Ee Mungu, uniumbie moyo safi, uifanye upya roho iliyotulia ndani yangu." Tena asema, "Kama mashariki ilivyo mbali na magharibi, ndivyo alivyoweka dhambi zetu mbali nasi." Zaburi 51:10; 103:12.

Mungu ndani ya Kristo, alijitoa mwenyewe kwa ajili ya dhambi zetu. Alipata mateso ya kifo kile cha kikatili pale msalabani, akauchukua mzigo wa dhambi kwa ajili yetu, "mwenye haki kwa ajili yao wasio haki," apate kutudhihirishia upendo wake, na kutuvuta kwake. Naye asema hivi: "Tena iweni wafadhili ninyi kwa ninyi, wenye huruma, mkasameheane kama na Mungu katika Kristo

alivyowasamehe ninyi.” Waefeso 4:32. Mwache Kristo, aliye Uzima wa Mungu,

akae ndani yako, na kwa njia yako apate kudhihirisha upendo ule utokao mbinguni utakaotia tumaini na kuleta amani itokayo mbinguni katika moyo uliolemewa na dhambi. Tunapomjia Mungu, hili ndilo sharti tunalokabiliana nalo tunapoingia nyumbani mwake, ya kwamba, tunapopata rehema yake, tujitoe wenyewe kwake ili tupate kuwadhihirishia wengine neema yake.

Jambo moja la muhimu kwetu ili tupate kupokea na kutoa upendo wa Mungu unaosamehe ni kulijua na kuliamini pendo lile alilo nalo kwetu. Shetani anatumia njia zote za udanganyifu kama awezavyo, apate kutuzuia tusilifahamu pendo lile. Atajaribu kutuongoza ili tufikiri kwamba makosa yetu na dhambi zetu zimekuwa nzito sana hata Bwana hawezi kuzijali sala zetu, tena hawezi kutubariki na kutuokoa. Ndani yetu wenyewe hatuwezi kuona cho chote ila udhaifu tu, hakuna kitu cha kutupatia sifa kwa Mungu, na Shetani anatuambia kwamba hatuna matumaini tena; hatuwezi kufanya lo lote kurekebisha mapungufu ya tabia zetu. Tunapojaribu kumwendea Mungu, adui ananong'ona na kutuambia, "Ni kazi bure kwako kuomba; je, hivi hukufanya jambo lile baya? Je, hujatenda dhambi dhidi ya Mungu, na kuihalifu dhamiri yako?" Lakini, twaweza kumwambia yule adui ya kuwa "damu yake Yesu Mwana wake, yatusafisha dhambi zote." 1 Yohana 1:7. Tunapoona kwamba tumefanya dhambi, na hatuwezi kuomba, huo ndio wakati hasa wa kusali. Twaweza kuona haya, na kushushwa moyo; lakini ni lazima tuombe, na kuamini. "Ni neno la kuaminiwa, tena lastahili kukubalika kabisa, ya kwamba Kristo Yesu alikuja ulimwenguni awaokoe wenye dhambi; ambao wa kwanza wao ni mimi." 1 Timotheo 1:15. Msamaha, yaani, kupatanishwa na Mungu, huja kwetu, si kama ijara kwa matendo yetu, hautolewi kwa sababu ya sifa njema walizo nazo wanadamu wenye dhambi, bali ni kipawa kwetu, kinachotolewa kwa msingi wa haki ya Kristo isiyo na waa.

Tusijaribu kupunguza hatia yetu kwa kutoa udhuru juu ya dhambi. Hatuna budi kukubali jinsi Mungu anavyoikadiria dhambi, na hilo ni jambo zito kweli. Ni Kalvari tu iwezayo kufunua ubaya mkubwa wa kutisha wa dhambi. Kama sisi wenyewe tungelazimika kubeba mzigo wa dhambi zetu, ungetuseta kabisa. Lakini Yeye asiye na dhambi amekuwa badala yetu; ingawa yeye hakustahili, ameyachukua maovu yetu. "Tukiziungama dhambi zetu," Mungu "ni mwaminifu na wa haki hata atuondolee dhambi zetu, na kutusafisha na udhalimu wote." 1 Yohana 1:9. Ni ukweli wa ajabu huo!—yeye ni mwenye haki kwa sheria yake mwenyewe, tena ni mwenye kuwahesabia haki wote wamwaminio Yesu. "Ni nani aliye Mungu kama wewe, mwenye kusamehe uovu, na kuliachilia kosa la watu wa urithi wake waliosalia? hashiki hasira yake milele, kwa maana yeye hufurahia rehema." Mika 7:18.

"Usitutie Majaribuni, Lakini Utuokoe Na Yule Mwovu."

Mathayo 6:13.

Majaribu ni ushawishi wa kufanya dhambi, na huo hautoki kwa Mungu, bali unatoka kwa Shetani, na kwenye uovu uliomo mioyoni mwetu wenyewe. “Mungu hawezi kujaribiwa na maovu, wala yeye mwenyewe hamjaribu mtu.” Yakobo 1:13.

Shetani anataka kututia majaribuni, ili uovu wa tabia zetu udhihirishwe mbele ya wanadamu na mbele ya malaika, apate kudai kuwa sisi ni watu wake. Katika mfano wa unabii wa Zekaria, Shetani anaonekana akisimama mkono wa kuume wa Malaika wa Bwana, akimshtaki Yoshua, kuhani mkuu, aliyevaa mavazi machafu, naye Shetani anaipinga kazi ambayo Malaika wa Mungu anataka kumfanyia Yoshua. Hii huonesha nia aliyo nayo Shetani dhidi ya kila mtu ambaye Kristo ataka kumvuta kwake. Yule adui hutuongoza tufanye dhambi, ndipo hutushtaki mbele ya wale wa mbinguni kuwa hatustahili upendo wa Mungu. Lakini “Bwana akamwambia Shetani, Bwana na akukemee, Ewe Shetani; naam, Bwana, aliyechagua Yerusalemu, na akukemee; je! hiki si kinga kilichotolewa motoni?” Kisha akamwambia Yoshua: “Tazama, nimekuondolea uovu wako, nami nitakuvika mavazi ya thamani nyingi.” Zekaria 3:1-4.

Kwa pendo lake kuu, Mungu anataka kukuza ndani yetu matunda ya thamani ya Roho wake. Anatuacha tupate migogoro, mateso na shida, si kama laana, bali kama mbaraka mkuu kuliko yote katika maisha yetu. Kila jaribu tunalolishinda, kila taabu tunayoivumilia, hutuletea uzoefu mpya maishani mwetu, na kutusogeza mbele katika kazi ya ujenzi wa tabia zetu. Mtu yule ambaye hushinda majaribu kwa nguvu itokayo juu, huwadhihirishia walimwengu na wote mbinguni jinsi neema ya Kristo ilivyo na nguvu.

Lakini wakati hatupaswi kuwa na hofu kwa ajili ya taabu, japo iwe kali, tungeomba kwamba Mungu asituache twende mahali ambapo tutavutwa mbali na tamaa za mioyo yetu miovu. Katika kusali sala hiyo aliyotupa Kristo, tunajitoa wenyewe kuongozwa na Mungu, tunamwomba atuongoze katika njia zilizo salama. Hatuwezi kusali sala hii kwa moyo mnyofu, na huku tukaazimu kwenda katika njia zetu tulizozichagua wenyewe. Tutausubiri mkono wake utuongoze; tutaisikiliza sauti yake, ikisema, “Njia ni hii, ifuateni.” Isaya 30:21.

Si salama kwetu kusitasita na kutafakari juu ya faida itakayopatikana tukiyatii mashauri ya Shetani. Dhambi humaanisha aibu na maangamizi kwa kila mtu ajifurahishaye katika hiyo; lakini kwa tabia yake inapofusha macho na kudanganya, tena inatushawishi kwa kutuletea mambo yanayovutia sana. Tukithubutu kwenda upande wa Shetani, hatuna ahadi yo yote ya kulindwa dhidi ya uwezo wake. Kwa kadiri ya uwezo ulio ndani yetu, imetupasa kufunga kila njia ambayo kwayo huyo mjaribu anaweza kupata njia ya kuingia ndani yetu.

Sala hii, “Usitutie majaribuni,” ni ahadi kwa yenyewe. Tukijiweka mikononi mwa Mungu, tunayo ahadi hii “hatawaacha mjaribiwe kupita mwezavyo; lakini pamoja na lile jaribu atafanya na mlango wa kutokea, ili mweze kustahimili.” 1 Wakorintho 10:13.

Kuna kitu kimoja tu kinachoweza kutulinda na maovu—nacho ni Kristo akikaa mioyoni mwetu kwa njia ya imani katika haki yake. Ni kwa sababu ubinafsi umo mioyoni mwetu ndiyo maana majaribu yanatushinda. Lakini tunapouona upendo mkuu wa Mungu, ubinafsi unaonekana kwetu katika hali yake ya kuchukiza sana na mbaya sana, nasi tunatamani uondolewe kabisa kutoka moyoni mwetu. Roho Mtakatifu anapomtukuza Kristo, mioyo yetu inalainishwa na kutiishwa, majaribu yanapoteza nguvu zake, na neema ya Kristo inazigeuza tabia zetu.

Kristo hatamtupa kamwe mtu ambaye amemfia. Huenda mtu huyo akamwacha Kristo, na kushindwa na majaribu; lakini Kristo kamwe hawezi kumpa kisogo mtu huyo aliyemlipia fidia kwa kutoa uhai wake mwenyewe. Laiti kama macho yetu ya kiroho yangeweza kutiwa nguvu, tungewaona watu walivyolemewa na taabu na mizigo ya huzuni zao, wakiwa wamekandamizwa, kama mkokoteni uliojazwa miganda, wakiwa tayari kufa kwa kukata tamaa. Tungewaona malaika wakiruka kasi kwenda kuwasaidia wale wanaojaribiwa, ambao wanasimama kana kwamba wako ukingoni mwa jabali refu, tayari kuanguka kule chini. Malaika toka mbinguni huyarudisha nyuma kwa nguvu majeshi ya uovu yanayowazunguka watu hawa, na kuwaongoza kuikita miguu yao juu ya msingi ulio imara. Vita vinavyopiganwa baina ya majeshi hayo mawili ni vita halisi kama vile vinavyopiganwa baina ya majeshi ya dunia hii, na juu ya hoja ya pambano hili la kiroho hatima yetu ya milele inategemea.

Kwetu sisi, kama kwa Petro, neno hili lanenwa, “Tazama, Shetani amewataka ninyi apate kuwapepeta kama vile ngano; lakini nimekuombea wewe ili imani yako isitindike.” Luka 22:31,32. Tumshukuru Mungu, hatujaachwa peke yetu. Yeye aliye“upenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele” (Yohana 3:16), hatatuacha peke yetu katika kupigana na yule adui wa Mungu na wa wanadamu. “Tazama,” yeye asema, “nimewapa amri ya kukanyaga nyoka na nge, na nguvu zote za yule adui, wala hakuna kitu kitakachowadhuru.” Luka 10:19.

Ishi kwa kuungana na Kristo aliye hai, naye atakushika sana kwa mkono wake usioweza kamwe kukuachia. Lifahamu na kuliamini pendo lile alilo nalo Mungu kwetu, nawe utakuwa salama; pendo hilo ni ngome isiyoweza kuvunjwa na madanganyo yote wala mashambulio yote ya Shetani. “Jina la Bwana ni ngome imara; mwenye haki huikimbilia, akawa salama.” Mithali 18:10.

“Kwa Kuwa Ufalme ni Wako, Na Nguvu, na Utukufu.” Mathayo 6:13.

Sentensi hii ya mwisho kama ile ya kwanza ya Sala ya Bwana, hutuelekeza kwa Baba yetu aliye juu ya uwezo wote na mamlaka yote na juu ya kila jina linalotajwa. Mwokozi aliiona miaka iliyokuwa mbele ya wanafunzi wake, si kama wao walivyowaza kuwa wataishi katika mwanga wa utajiri wa ulimwengu huu na heshima yake, bali yeye aliiona ikiwa ya giza na dhoruba kali inayotokana na chuki za wanadamu na ghadhabu ya Shetani. Katikati ya vita za taifa lile na maangamizi yake, hatua za wanafunzi zingekabiliwa na hatari nyingi, na mara nyingi mioyo yao ingelemewa kwa hofu. Iliwapasa kuiona Yerusalemu ikiharibiwa vibaya, hekalu likifagiliwa mbali, ibada yake ikikomeshwa milele, na Waisraeli wakitawanyika katika nchi zote, kama meli zilizoharibika ufukoni mwa jangwa. Yesu alisema: “Nanyi mtasikia habari za vita na matetesi ya vita.” “Kwa maana taifa litaondoka kupigana na taifa, na ufalme kupigana na ufalme; kutakuwa na njaa, na matetemeko ya nchi mahali mahali. Hayo yote ndiyo mwanzo wa utungu.” Mathayo 24:6-8. Licha ya hayo, haikuwapasa wafuasi wa Kristo kuogopa kwamba tumaini lao lilikuwa limepotea, wala kufikiri kwamba Mungu alikuwa ameiacha dunia. Uweza na utukufu ni wake yeye ambaye makusudi yake makuu bado yangeendelea kusonga mbele bila ya kipingamizi cho chote mpaka yatakapotimizwa kabisa. Katika sala hii iliyoonesha mahitaji yao ya kila siku, wanafunzi wa Kristo walielekezwa kuangalia juu zaidi ya ile nguvu na utawala wote wa uovu, kwa Bwana Mungu wao, ambaye ufalme wake unatawala yote, na ambaye ni Baba yao na Rafiki yao wa milele.

Kuangamizwa kwa Yerusalemu kulikuwa mfano wa kuangamizwa kwa dunia siku ya mwisho. Unabii ule uliokuwa ukitimizwa kwa sehemu katika kuangamizwa kwa Yerusalemu, unazihusu zaidi sana siku za mwisho. Sasa tunasimama ukingoni mwa matukio makubwa na ya kutisha. Hatari kubwa iko mbele yetu, ambayo ulimwengu huu haujapata kamwe kuishuhudia. Na tamu kwetu, kama kwa wale wanafunzi wa kwanza, yaja ahadi isemayo kwamba ufalme wa Mungu unatawala juu ya yote. Programu ya matukio yajayo imo mikononi mwa Muumbaji wetu. Mfalme wa mbinguni anajua hatima ya mataifa, pamoja na mambo yanayolihusu kanisa lake, hayo yako chini ya uangalizi wake. Mwalimu toka mbinguni anasema kwa kila mjumbe katika kuikamilisha mipango yake, kama alivyomwambia Koreshi, “Nitakufunga mshipi ijapokuwa hukunijua.” Isaya 45:5.

Katika njozi ya nabii Ezekieli, palionekana mkono chini ya mabawa ya makerubi. Maana yake ni kuwafundisha watenda kazi wake kuwa uwezo wa Mungu ndio unaowafanikisha. Wale ambao Mungu huwatumia kama wajumbe wake wasijione kwamba kazi yake inawategemea wao. Wanadamu wenye maisha mafupi hawaachwi kuubeba mzigo wa kazi hii. Yeye asiyesinzia, ambaye daima yu kazini

kwa kuyatimiza makusudi yake, ataendesha kazi yake mwenyewe. Atayazuia

makusudi ya wabaya, na kuyachafua mashauri ya wale wanaofanya shauri baya juu ya watu wake. Yeye aliye Mfalme, Bwana wa majeshi, anaketi katikati ya makerubi, naye bado anawalinda watoto wake katikati ya mapigano na machafuko ya mataifa. Yeye atawalaye mbinguni ndiye Mwokozi wetu. Hulipima kila jaribu, huiangalia tanuru ya moto ambao hauna budi kumpima kila mmoja. Ngome za wafalme zitakapoangushwa, mishale ya ghadhabu itakapochoma mioyo ya adui zake, watu wake watakuwa salama mikononi mwake.

"Ee Bwana, ukuu ni wako, na uwezo, na utukufu, na kushinda, na enzi; maana vitu vyote vilivyo mbinguni na duniani ni vyako;... na mkononi mwako mna uwezo na nguvu; tena mkononi mwako mna kuwatukuza na kuwawezesha wote." 1 Mambo ya Nyakati 29:11,12.

Mungu ninakuja kwako, Nguvu na nirejezewe,
Naitwa na neno lako, Dhambi na nisamehewe,
Nije miguuni pako, Kwako na nibarikiwe,
Asubuhi. Hivi leo.

Nakukaribia Wewe, Hata nifike mbinguni,
Daima nifurahiwe, Sina tamu duniani,
Lazima nisizuiwe, Kama pako miguuni,
Na dunia. Bwana wangu.

## SURA YA 6

# SIYO KUHUKUMU BALI KUFANYA

“Msihukumu, ili msihukumiwe.” Mathayo 7:1.

Jitihada ya kujipatia wokovu kwa matendo mema ya mtu mwenyewe huwaongoza wanadamu katika kuzidisha masharti ya kibinadamu yawe kizuio cha dhambi. Maana, wakiona wanashindwa kuishika sheria, basi, wanaweka masharti na kanuni zao wenyewe ili kujilazimisha kuitii sheria. Haya yote huiondoa nia kutoka kwa Mungu na kuielekeza kwa mtu ili aifikirie nafsi yake mwenyewe. Upendo wake unatoweka moyoni, na pia upendo wake kwa wanadamu wenzake unatoweka. Mfumo uliobuniwa na wanadamu, pamoja na masharti yake mengi sana, unawafanya wale wanaoutetea kuwahukumu wote wanaopungua kufikia kiwango kilichowekwa na binadamu. Roho ya ubinafsi na ukosoaji finyu, hufisha hisia za uadilifu na ukarimu, na kuwafanya wanadamu kuwa mahakimu wanaojipenda binafsi na wapelelezi wa mambo madogo ya wengine.

Mafarisayo walikuwa katika kundi hili. Walipotoka katika ibada zao, hawakujidhili mioyoni mwao kwa udhaifu waliokuwa nao, wala hawakuwa na shukrani kwa Mungu kwa upendeleo mkubwa aliowapa. Walitoka wakiwa wamejaa kiburi, na neno lao kuu lilikuwa hili: “Mimi mwenyewe, hisia zangu, ujuzi wangu, njia zangu mwenyewe.” Kipeo walichokifikia kikawa ndicho kipimo ambacho kwacho waliwapima wengine, na kuwahukumu. Wakiwa wamevaa mavazi ya kujitukuza wenyewe, walipanda juu ya kiti cha hukumu kuwakosoa na kuwahukumu wengine.

Hata akina yahe kwa sehemu kubwa walikuwa na roho ile ile, wakijiingiza wenyewe kufanya kazi ya dhamiri na kuhukumiana wao kwa wao juu ya mambo yaliyokuwa kati ya mwanadamu na Mungu. Ilikuwa ni kwa ajili ya roho hii na matendo yao ndiyo maana Yesu alisema, “Msihukumu, ili msihukumiwe.” Maana yake, usijiweke mwenyewe kuwa kipimo cha kuwapimia wengine. Kauli zako, na mawazo yako juu ya wajibu, maelezo yako juu ya neno la Mungu, yasiwekwe kuwa kipimo cha kuwakadiria wengine na moyoni mwako kuwalaumu wakikosa kukifikia kipeo chako. Usiwakosoe wengine na kuyakisia makusudi yao bila kuyahakikisha, na kuwahukumu.

“Basi ninyi msihukumu neno kabla ya wakati wake, hata ajapo Bwana; ambaye atayamulikisha yaliyositirika ya giza, na kuyadhihirisha mashauri ya mioyo.” 1 Wakorintho 4:5. Sisi hatuwezi kuyasoma yaliyomo moyoni. Kwa kuwa sisi wenyewe tu wenye makosa, hatustahili kuwahukumu wengine. Wanadamu

wanaweza kuhukumu kwa kulitazama umbo la nje tu. Yeye peke yake ajuaye

mambo ya moyoni, ambaye ni mwenye hisani na huruma, ndiye atakayekata shauri juu ya kila mtu.

“Kwa hiyo, wewe mtu uwaye yote uhukumuye, huna udhuru; kwa maana katika hayo umhukumuyo mwingine wajihukumu mwenyewe kuwa na hatia; kwa maana wewe uhukumuye unafanya yale yale.” Warumi 2:1. Hivyo wenye kuwalaumu na kuwakosoa wengine, hujitangaza wenyewe kwamba wana hatia wenyewe; kwa maana hufanya mambo yale yale. Katika kuwahukumu wengine, hukata hukumu yao wenyewe; na Mungu asema kwamba hukumu hii ni ya haki.Anakubali hukumu wanayojikatia wenyewe.

“Nyayo hizi nzito, bado ziko matopeni,
Zaenda huku zikiseta maua pasipo kukoma; Mikono hii migumu, ambayo tuna maana nzuri nayo
Twaitupa kwa nguvu ndani ya moyo wa rafiki.”

“Mbona Wakitazama Kibanzi Kilicho Ndani ya Jicho la Ndugu Yako?” Mathayo 7:3.

Neno hili, “Wewe uhukumuye unafanya yale yale,” halitoshi kuonesha ukubwa wa dhambi ya mtu yule anayethubutu kumlaumu na kumhukumu nduguye jinsi ilivyo. Yesu alisema, “Mbona wakitazama kibanzi kilicho ndani ya jicho la ndugu yako, na boriti iliyo ndani ya jicho lako mwenyewe huiangalii?”

Maneno yake yanamweleza mtu yule aliye mwepesi kuyaona makosa ya wengine. Anapodhani kwamba amepata kosa katika tabia ama katika mwenendo wa mtu fulani, anafanya bidii inayozid i kiasi kujaribu kumwonesha kosa lake; lakini Yesu anatangaza kwamba tabia iyo hiyo hasa inayokuzwa kwa kufanya kazi hii isiyo ya Kikristo, ukiilinganisha na kosa linalolaumiwa, ni kama boriti ikilinganishwa na kibanzi. Ni kukosa moyo wa uvumilivu na upendo kunakomwongoza mtu kuhesabu kitu kidogo sana kuwa kikubwa mno. Wale ambao katika mioyo yao wenyewe hawajawahi kuwa na majuto kwa ajili ya dhambi wala hawajajitoa kabisa kuwa wa Kristo, katika maisha yao hawawezi kudhihirisha mvuto ule ulainishao wa upendo wa Mwokozi. Wanaiwakilisha vibaya roho ya upole na heshima inayoletwa na injili, na kuwaumiza watu wa thamani, ambao Kristo alikufa kwa ajili yao. Kulingana na mfano anaoutumia Mwokozi wetu, aliye na moyo wa kuwalaumu wengine yu mwenye kosa kubwa kuliko yule anayemshtaki; kwa maana yeye siyo tu anafanya kosa lile lile, bali anaongeza juu yake makosa ya kujivuna na kuwa na moyo wa kuwalaumu wengine.

Kristo ndiye kipimo halisi cha tabia; na yule ajiwekaye mwenyewe kuwa kipimo cha wengine, anajiweka mahali pa Kristo. Na kwa kuwa Baba “amempa Mwana

hukumu yote" (Yohana 5:22), ye yote anayethubutu kuhukumu nia na makusudi

ya wengine anajinyakulia tena mamlaka yamhusuyo Mwana wa Mungu peke yake. Mahakimu hao na wakosoaji hao wanaojiweka wenyewe wanajiweka upande wa Mpinga Kristo, “ajiinuaye nafsi yake juu ya kila kiitwacho Mungu ama kuabudiwa; hata yeye mwenyewe kuketi katika hekalu la Mungu; akijionesha nafsi yake kana kwamba yeye ndiye Mungu.” 2 Wathesalonike 2:4.

Dhambi iletayo matokeo machungu sana ni moyo usio na upendo, unaolaumu, na usiosamehe, ambao tabia yake inafanana na Ufarisayo. Maisha ya dini yasipokuwa na upendo, Yesu hayumo humo; nuru ya kuwako kwake haimo humo. Kushughulika sana na shughuli fulani au kuwa na bidii nyingi bila Kristo hakuwezi kujazia mapungufu. Pengine twaweza kuwa wepesi katika kuona makosa ya wengine; lakini kila apendaye kuwa na roho hiyo, Yesu humwambia, “Mnafiki wewe, itoe kwanza ile boriti katika jicho lako mwenyewe; ndipo utakapoona vema kukitoa kile kibanzi katika jicho la ndugu yako.” Yeye aliye na hatia ya kutenda baya ndiye mwepesi kushuku kosa kwa mtu mwingine. Katika kumhukumu mwingine anajaribu kufunika ama kutoa udhuru kwa ubaya ulio moyoni mwake. Ilikuwa ni kwa njia ya kutenda dhambi wanadamu walipata ujuzi wa uovu; watu wale wawili wa kwanza mara tu walipokwisha kufanya dhambi walianza kulaumiana; na hivyo ndivyo tabia ya asili ya binadamu itakavyofanya bila kukwepa isipotawaliwa na neema yake Kristo.

Wanadamu wakiendekeza roho hii ya kuwalaumu wengine, hawatosheki kuonesha tu jambo lile wanalodhani kuwa ndilo kosa la ndugu yao. Wasipoweza kumfanya atende lile wanalofikiri angepaswa kufanya kwa njia ya upole, basi, wanatumia nguvu. Kwa kadiri ya uwezo walio nao watawashurutisha wengine kufanya matakwa yao wanayodhani ni sahihi. Hivyo ndivyo walivyofanya Wayahudi katika siku za Kristo; na ndivyo pia lilivyopata kufanya kanisa wakati wo wote ule lilipopoteza neema ya Kristo. Lijikutapo lenyewe kuwa halina nguvu ya upendo, limepata kunyosha mkono wake kuushika mkono wenye nguvu wa dola ili ishinikize mafundisho yake na kusimamia utekelezaji wa amri zake. Hapa ndipo ilipo siri ya amri zote za kidini zilizotungiwa sheria na serikali za dunia, tena hii ndiyo siri ya mateso yote kuanzia siku zile za Habili mpaka zamani hizi. Kristo hawashurutishi watu, bali anawavuta kwake. Shurutisho pekee analolitumia ni upendo wake unaobidisha. Kanisa lianzapo kutegemea nguvu za mamlaka ya kidunia, ni dhahiri kwamba halina uwezo wa Kristo kabisa—yaani, halina upendo wa Mungu unaobidisha.

Lakini shida inakuwa kwa mtu mmoja mmoja katika kanisa, na ni hapo tiba ni lazima ifanyike. Yesu anamwagiza mwenye kumshtaki nduguye aitoe kwanza boriti katika jicho lake, aache kuwa na moyo wa kuwalaumu bure watu wengine, aungame na kuziacha dhambi zake, kabla ya kujaribu kuwasahihisha wengine.

matunda mazuri.” Luka 6:43. Moyo wa kulaumu unaouendekeza ni matunda mabaya, na huonesha kuwa mti huo ni mbaya. Ni kazi bure kwenu kujijengea haki yenu wenyewe. Mnachohitaji ni badiliko la moyo. Hamna budi kuwa na uzoefu huu kabla hamjaweza kufaa kuwasahihisha wengine; “maana, kinywa cha mtu huyanena yaujazayo moyo wake.” Mathayo 12:34.

Shida inapokuja katika maisha ya mtu awaye yote, nawe unajaribu kumpa ushauri au onyo, maneno yako yatakuwa na uzito tu kulingana na mvuto wako wa kutenda mema uliojipatia kwa mfano wako na roho yako. Yakupasa kuwa mwema kabla hujaweza kutenda mema. Huwezi kuwa na mvuto utakaowabadilisha wengine mpaka moyo wako uwe umenyenyekezwa na kutakaswa na kuwa na huruma kwa neema yake Kristo. Badiliko hili linapofanyika ndani yako, ndipo itakuwa kawaida kwako kuishi maisha ya kuwaletea wengine mibaraka kama ilivyo kwa mti wa waridi kutoa maua yake yanayonukia vizuri sana au kwa mzabibu kuzaa vichala vyake vya rangi ya zambarau.

Kristo akiwa ndani yako, “tumaini la utukufu,” hutakuwa na nia ya kuwaangalia wengine, na kuyafunua makosa yao. Badala ya kutaka kuwashtaki na kuwalaumu, utakusud ia kuwasaidia, kuwabariki, na kuwaokoa. Katika kushughulika na wale walio na makosa, utazingatia agizo lisemalo, Ukijiangalia “nafsi yako usije ukajaribiwa wewe mwenyewe.” Wagalatia 6:1. Utakumbuka mara nyingi jinsi wewe mwenyewe ulivyofanya makosa, na jinsi ilivyokuwa vigumu kwako kuipata tena njia ya haki baada ya kuiacha,. Hutamsukuma ndugu yako kuingia katika giza nene zaidi, bali kwa moyo uliojaa huruma utamwambia juu ya hatari inayomkabili.

Yeye autazamaye mara kwa mara msalaba wa Kalvari, na kukumbuka kuwa ni dhambi zake zilizomweka pale Mwokozi, hatajaribu kamwe kukadiria kiwango cha dhambi zake kwa kuzilinganisha na zile za wengine. Hataketi juu ya kiti cha hukumu kumshtaki mwingine. Wale wanaotembea katika uvuli wa msalaba wa Kalvari hawatakuwa na moyo wa kuwalaumu wengine wala wa kujitukuza wenyewe.

Mpaka hapo utakapojisikia ya kuwa ungeweza kupoteza heshima yako mwenyewe, na hata kutoa uhai wako ili kumwokoa ndugu anayekosa, utakuwa umeondoa boriti iliyo ndani ya jicho lako na kuweza kuwa tayari kumsaidia ndugu yako. Ndipo waweza kumkaribia na kumgusa moyo wake. Hakuna aliyerejeshwa kutoka makosani kwa kukemewa na kulaumiwa; bali wengi kwa njia hiyo wamefukuzwa mbali na Kristo, na wamefanywa waifunge mioyo yao wasisikie mvuto wa Roho Mtakatifu. Moyo wa upendo, tabia ya upole inayovutia kwa watu, huweza kuwaokoa wakosaji na kufunika wingi wa dhambi zao. Kuonekana kwa

Kristo katika tabia yako kutakuwa na uwezo wa kuwabadilisha tabia wale wote

unaokutana nao. Mwache Kristo aonekane ndani yako kila siku, naye ataidhihirisha kupitia kwako nguvu ile iumbayo ya neno lake—yaani, ile nguvu inayofanya kazi yake kwa upole, kwa ushawishi, lakini iliyo na mvuto wenye nguvu kuwaumba upya watu wengine katika uzuri wa Bwana Mungu wetu.

"Msiwape Mbwa Kilicho Kitakatifu." Mathayo 7:6.

Hapa Yesu asema habari za watu wasiotaka kuwekwa huru mbali na utumwa wa dhambi. Kwa ajili ya kujizoeza kufanya mabaya na maovu, hali yao na tabia zao zimepotoka hata wanashikamana na uovu, hawataki kutengwa mbali nao. Watenda kazi wa Kristo wasikubali kuzuiwa na wale wanaoshindana tu na Injili na kuifanyia dhihaka.

Lakini Mwokozi kamwe hakumwacha hata mtu mmoja, ingawa ni mwenye dhambi sana, ambaye alikubali kuzipokea zile kweli za thamani za mbinguni. Maneno yake yalikuwa mwanzo wa maisha mapya kwa watoza ushuru na makahaba. Mariamu Magdalene, ambaye alimtoa pepo saba, alikuwa mtu wa mwisho kaburini pa Mwokozi, pia alikuwa mtu wa kwanza kumwamkia asubuhi ile ya ufufuo wake. Alikuwa ni yule Sauli wa Tarso, mmoja wa maadui wakuu sana wa Injili, aliyegeuka na kuwa Paulo, mtenda kazi mwaminifu wa Kristo. Chini ya mwonekano wa chuki na dharau, hata chini ya uhalifu na ufisadi, anaweza kujificha mtu ambaye neema ya Kristo itamwokoa apate kung'aa kama johari katika taji ya Mkombozi.

"Ombeni, Nanyi Mtapewa; Tafuteni, Nanyi Mtaona; Bisheni, Nanyi Mtafunguliwa."
Mathayo 7:7.

Bwana anaikariri ahadi yake mara tatu, ili mtu awaye yote asiwe na nafasi ya kutoamini, ama kutofahamu, ama kueleza vibaya maana ya maneno yake. Atamani sana kwamba wale wamtafutao Mungu wamwamini Yeye awezaye kutenda mambo yote. Kwa hiyo, anaongeza kusema, "Kwa maana kila aombaye hupokea; naye atafutaye huona; naye abishaye atafunguliwa."

Bwana hataji masharti yo yote ila kwamba wewe uzitamani rehema zake, utake shauri lake, na kutamani sana pendo lake. "Omba." Kule kuomba kunadhihirisha kuwa unaitambua haja yako; na ukiomba kwa imani, utapata. Bwana ametoa ahadi katika neno lake, nalo haliwezi kukosa kutimizwa. Kama ukimjia kwa majuto ya kweli, hupaswi kujisikia ya kuwa wewe ni mfidhuli unapomwomba lile aliloahidi. Uombapo mibaraka unayohitaji, ili uikamilishe tabia yako iwe kama ile ya Kristo, Bwana anakuhakikishia wewe ya kwamba unaomba sawasawa na

ahadi itakayothibitishwa kuwa ya kweli.Kujisikia na kufahamu jinsi ulivyo

mwenye dhambi ni sababu ya kutosha ifaayo kuomba rehema na huruma zake. Sharti la kumjia Mungu si kwamba wewe uwe mtakatifu, bali kwamba utake akutakase dhambi zako zote na kukusafisha uovu wote. Hoja ambayo twaweza kuileta kwake sasa na daima ni ile inayohusu haja yetu kuu, yaani, ile hali yetu ya kutokuwa na uwezo kabisa, ambayo inamfanya yeye na uweza wake ukomboao kuwa wa lazima.

"Tafuta." Tusitake mbaraka wake tu, bali tumtake Yeye mwenyewe. "Mjue sana Mungu, ili uwe na amani." Ayubu 22:21. Tafuta, nawe utaona. Mungu anakutafuta wewe, na ile shauku yenyewe unayoisikia ya kuja kwake ni Roho wake akuvutaye. Heri ukubali mvuto wake huo. Kristo anawaombea wajaribiwao, wakosao, na wasioamini. Ataka kuwainua wawe katika hali ya urafiki naye. "Ukimtafuta, ataonekana nawe." 1 Mambo ya Nyakati 28:9.

"Bisha." Tunamjia Mungu kwa maana tumealikwa rasmi, naye hutungojea tufike kwake. Wanafunzi waliomfuata Yesu mara ya kwanza hawakuridhika na maongezi machache naye huko njiani; walisema, "Rabi,... unakaa wapi? ... Wakaenda, wakaona akaapo, wakakaa kwake siku ile." Yohana 1:38,39. Hivyo pia nasi twaweza kumkaribia Mungu na kuongea naye. "Aketiye mahali pa siri pake Aliye juu atakaa katika uvuli wake Mwenyezi." Zaburi 91:1. Wale watakao mbaraka wa Mungu basi, wabishe mlango wa rehema zake na kungoja wakiwa na tumaini na kusema, kwa maana wewe, Ee Bwana, umesema, "Kila aombaye hupokea; naye atafutaye huona; naye abishaye atafunguliwa."

Yesu aliwaangalia wale waliokusanyika kuyasikia maneno yake, naye alitamani sana kwamba watu wale wengi wapate kufahamu rehema na upendo wa Mungu. Kama kielelezo cha hitaji lao na jinsi Mungu alivyo tayari kuwapa, aliwaeleza juu ya mtoto amwombaye mzazi wake wa kidunia chakula. Alisema, "Kuna mtu yupi kwenu, ambaye, mwanawe akimwomba mkate, atampa jiwe?" Anagusia upendo wenye huruma ambao ni silika ya mzazi kwa mtoto wake na kisha anasema, "Basi ikiwa ninyi, mlio waovu, mnajua kuwapa watoto wenu vipawa vyema, je! si zaidi sana Baba yenu aliye mbinguni atawapa mema wao wamwombao?" Hakuna mtu awaye yote mwenye moyo kama wa baba ambaye angemwacha mwanawe aliye na njaa anayemwomba mkate. Je, watu wangemfikiria ya kuwa angeweza kumchezea mtoto wake, yaani, kumtamanisha bure kwa kuinua juu matumaini yake ya kupata, halafu kumkatisha tu tamaa? Je, angemwahidi kumpa chakula kizuri chenye virutubisho, kisha ampe jiwe? Basi, mtu awaye yote angewezaje kukosa kumheshimu Mungu na kufikiri kwamba Yeye asingejibu maombi ya watoto wake?

Basi ikiwa ninyi wanadamu, mlio waovu, "mnajua kuwapa watoto wenu vipawa

vyema, je! Baba aliye mbinguni hatazidi sana kuwapa Roho Mtakatifu hao

wamwombao?" Luka 11:13. Roho Mtakatifu, anayemwakilisha Yeye, ndiye kipawa kikubwa kuliko vyote. "Vitu vyema" vyote vimo ndani yake. Muumbaji mwenyewe hawezi kutupa kitu cho chote kilicho kikubwa au bora kuliko hiki. Tunapomsihi Bwana atuhurumie katika shida yetu, na kutuongoza kwa Roho wake Mtakatifu, kamwe hatatuacha bila kusikia sala yetu. Uwezekano upo hata kwa mzazi kugeuka na kwenda zake mbali na mtoto wake mwenye njaa, bali Mungu hawezi kamwe kukikataa kilio kitokacho katika moyo wenye haja na shauku kubwa. Ni kwa huruma ilioje ameuelezea upendo wake! Kwa wale ambao katika siku za shida wanajisikia kwamba Mungu hawajali, huu ndio ujumbe utokao moyoni mwa Baba: "Sayuni alisema, Yehova ameniacha, Bwana amenisahau. Je! mwanamke aweza kumsahau mtoto wake anyonyaye, hata asimhurumie mwana wa tumbo lake? Naam, hawa waweza kusahau, lakini mimi sitakusahau wewe. Tazama, nimekuchora katika vitanga vya mikono yangu." Isaya 49:14-16.

Katika kila ahadi ya neno la Mungu tunalo jambo la kuomba, tukiweka mbele zake neno lake aliloahidi kama dhamana yetu. Hata tuwe tunahitaji mbaraka gani wa kiroho, ni haki yetu kuudai mbaraka huo kwa jina la Yesu. Twaweza kumwambia Bwana, kwa unyofu kama ule wa mtoto, hitaji letu kama lilivyo hasa. Twaweza kumweleza mambo yetu ya kimwili, kumwomba mkate na mavazi pamoja na mkate ule wa uzima na vazi la haki ya Kristo. Baba yako aliye mbinguni anajua kwamba unayahitaji hayo yote, nawe unakaribishwa kumwomba yeye kuhusiana na mambo hayo. Ni kwa njia ya jina la Yesu kila fadhili inapokewa. Mungu ataliheshimu jina lile na "atawajazeni kila mnachokihitaji kwa kadiri ya utajiri wake." Wafilipi 4:19.

Lakini usisahau kwamba ukimjia Mungu kama Baba yako, unakubali kwamba wewe ni mtoto wake. Siyo tu kwamba wewe uzitumainie fadhili zake, bali katika mambo yote uyatii mapenzi yake, ukijua kwamba upendo wake haubadiliki. Unajitoa kwake kufanya kazi yake. Wale ambao Yesu alikuwa amewaagiza watafute kwanza ufalme wa Mungu na haki yake, ndio aliowapa ahadi hii, "Ombeni, nanyi mtapata." Yohana 16:24.

Vipawa vyake Yeye aliye na mamlaka yote mbinguni na duniani vimewekwa akiba kwa ajili ya watoto wa Mungu. Ni vipawa vya thamani sana kiasi kwamba tunavipata kwa njia ya kafara ya damu ya Mkombozi wetu; vipawa vinavyoitosheleza shauku kubwa sana ya moyo wetu; vipawa hivi vitadumu milele; wote watakaomjia Mungu kama watoto wadogo watavipokea vipawa hivi na kuvifurahia. Zitumie ahadi za Mungu kama ni zako mwenyewe, zidai mbele zake kama ni maneno yake mwenyewe, nawe utapokea utimilifu wa furaha.

"Basi Yo Yote Myatakayo Mtendewe na Watu, Nanyi Watendeeni Vivyo Hivyo."

Mathayo 7:12.

Kwa kutege mea ahadi ya pendo la Mungu alionalo kwetu, Yesu anatuamuru tupendane sisi kwa sisi, kwa kuifuata kanuni hiyo moja inayojumuisha yote na kugusia mahusiano yote ya ushirikiano wa kibinadamu.

Wayahudi walijali sana kile ambacho wangepata; mzigo wa wasiwasi wao ulikuwa juu ya kile walichodhani ni stahili yao kuhusu mamlaka na heshima na huduma. Lakini, Kristo anatufundisha kwamba mahangaiko yetu yasingekuwa juu ya, Tutapata kiasi gani? bali juu ya, Kiasi gani tunaweza kutoa? Kipimo cha uwajibikaji wetu kwa wengine kinapatikana katika yale ambayo sisi wenyewe tunaona kuwa ni wajibu wao kututendea sisi.

Katika kushirikiana na wengine, jitie mahali pao. Ingia katika hisia zao, shida zao, kukata tamaa kwao, furaha zao, na huzuni zao. Ujifanye mmoja wao, na ha lafu watendee kama vile ambavyo wewe ungependa wakutendee kama ungebadilishana nao hali ile waliyo nayo. Hii ndiyo kanuni halisi ya haki. Hayo ndiyo maelezo mengine ya amri hii, “Mpende jirani yako kama nafsi yako.” Mathayo 22:39. Pia ndicho kiini cha mafundisho ya manabii. Ni kanuni ya mbinguni, na itakuzwa ndani ya wote wanaoandaliwa kufika huko kushiriki urafiki wa watakatifu.

Usia ule—Watendee wengine kama unavyotaka wakutendee wewe—ndiyo kanuni ya uungwana wa kweli, na kielelezo chake halisi huonekana katika maisha na tabia ya Yesu. Ni nuru iliyoje hiyo ya upole na uzuri iliyoangaza katika maisha ya kila siku ya Mwokozi wetu! Mambo ya kupendeza kama nini yaliyotokana na kuwako kwake! Roho ile ile itaonekana ndani ya watoto wake. Wale wakaao na Kristo watazungukwa na mvuto mtakatifu. Mavazi yao meupe ya usafi wa maisha yatanukia manukato matamu kutoka katika bustani ya Bwana. Nuru yake itaonekana nyusoni pao, nao wataimulikia njia miguu inayojikwaa na iliyochoka. Mtu ye yote anayefahamu tabia kamilifu ilivyo hatakosa kudhihirisha huruma na upole wa Kristo maishani mwake. Mvuto wa neema ni kuulainisha moyo, kuziadilisha na kuzitakasa hisia, kumpa mtu uzuri na adabu yenye chimbuko lake mbinguni.

Lakini usia huu—Watendee wengine kama unavyotaka wakutendee wewe—bado una maana yenye kina zaidi. Kila mtu aliyefanywa kuwa wakili wa neema mbalimbali za Mungu, ameitwa kuwaletea nuru wale wasiomjua Mungu na walio gizani, kama vile yeye ambavyo angekuwa mahali pao angetaka wamfanyie. Mtume Paulo alisema, “Nawiwa na Wayunani na wasio Wayunani, nawiwa na wenye hekima na wasio na hekima.” Warumi 1:14. Kwa yote uliyoyajua juu ya pendo la Mungu, kwa vyote ulivyopewa kuhusiana na vipawa vyema vya neema yake zaidi ya yule aliye mjinga na aliye na hali mbaya hapa duniani, ndivyo

unavyowiwa na mtu yule ili umgawie vipawa hivyo.

Vivyo hivyo kwa vipawa na mibaraka ya maisha haya; unawiwa na wenzako kwa vile vyote ulivyo navyo zaidi yao; kwa kadiri ambayo umejaliwa zaidi yao ndivyo unavyowiwa nao. Hivi tunao utajiri au hata anasa za maisha haya, basi, tunao wajibu mzito sana kuwatunza wagonjwa, wajane na yatima kama vile ambavyo sisi tungetumaini kusaidiwa nao endapo hali yetu ingegeuzwa kuwa kama yao.

Usia huu, kwa maana yake halisi, unafundisha kweli ile ile iliyofundishwa mahali pengine katika Mahubiri ya Mlimani, ya kwamba "kipimo kile mpimiacho, ndicho mtakachopimiwa." Lile tuwatendealo wengine, kama ni jema au baya, litaturudia tena sisi wenyewe, na kutuletea baraka au laana. Cho chote tutoacho, tutakipokea tena. Mibaraka ya kidunia tunayowatolea wengine, mara nyingi inaweza inarudishwa kwetu kama tulivyoitoa. Tutoacho kinaturudia sisi wakati wa shida, mara nyingi huturudia mara nne kwa kipimo cha fedha za ufalme wake. Lakini, zaidi ya hayo, vipaji vyote vinarudishwa, hata katika maisha haya, kwa kujazwa pendo lake kikamilifu, ambalo ni utukufu wote wa mbinguni na hazina yake. Na maovu tuliyowatendea nayo yanarudi tena. Kila mtu ambaye amethubutu kuwalaumu wengine na kuwakatisha tamaa, hana budi kupitishwa yeye mwenyewe katika njia ile ile ambayo aliwapitisha wengine; atapata uchungu walioupata kwa vile yeye hakuwa na huruma wala upole kwao.

Pendo la Mungu alilo nalo kwetu ndilo lililoagiza hivyo. Ataka atuongoze tupate kuchukizwa na ugumu wa mioyo yetu, na kumfungulia Yesu mioyo yetu akae humo. Na hivyo, kutoka katika kitu kibaya, chema kinatokea, na kile kilichoonekana kuwa ni laana hugeuka na kuwa mbaraka.

Kipimo cha usia ule mwema—Watendee wengine kama unavyotaka wakutendee wewe—ndicho kipimo halisi cha Ukristo; cho chote kinachopungua katika kipimo hiki ni udanganyifu. Dini ile inayowaongoza watu kuwaona binadamu kuwa wana thamani ndogo tu, ambao Kristo aliwahesabu kuwa wana thamani kubwa hata akajitoa nafsi yake kwa ajili yao; dini ile ambayo inatuongoza tusijali mahitaji ya binadamu, mateso yao, au haki zao, ni dini ya uongo. Kama tunadharau madai ya maskini, na wateswao, na wenye dhambi, twajidhihirisha kuwa tu wasaliti wa Kristo. Ni kwa sababu watu wanajiita tu kwa jina la Kristo, wakati katika maisha yao wanakataa kuwa na tabia yake, ndiyo maana Ukristo una nguvu kidogo sana ulimwenguni. Watu wanalikufuru jina la Bwana kwa sababu ya mambo hayo.

Kuhusu kanisa lile la mitume, katika siku zile angavu utukufu wa Kristo aliyefufuka ulipoangaza juu yao, imeandikwa kwamba hakuna mtu ye yote aliyesema, "kuwa kitu cho chote alicho nacho ni mali yake mwenyewe." "Wala hapakuwa na mtu mmoja miongoni mwao mwenye mahitaji." "Na mitume wakatoa ushuhuda wa kufufuka kwake Yesu kwa nguvu nyingi, na neema nyingi

ikawa juu ya wote.” “Na siku zote kwa moyo mmoja walidumu ndani ya hekalu,

wakimega mkate nyumba kwa nyumba, na kushiriki chakula chao kwa furaha na kwa moyo mweupe, wakimsifu Mungu, na kuwapendeza watu wote. Bwana akalizidisha kanisa kila siku kwa wale waliokuwa wakiokolewa.” Matendo 4:32,34,33; 2:46,47.

Tafuta mbinguni na duniani, hakuna kweli nyingine inayodhihirishwa kuwa ina nguvu zaidi ya ile inayooneshwa kwa matendo ya huruma yatendwayo kwa wale wanaohitaji huruma yetu na msaada wetu. Hii ndiyo kweli jinsi ilivyo katika Kristo. Wale wanaolitaja jina la Kristo watakapozifuata kanuni za usia huu, ndipo Injili itakapokuwa na nguvu kama ile iliyokuwa nayo katika siku zile za mitume.

“Mlango ni Mwembamba, na Njia Imesonga Iendayo Uzimani.” Mathayo 7:14.

Katika siku za Kristo watu wa nchi ya Palestina walikaa katika miji yenye maboma, ambayo mingi yao ilijengwa juu ya vilima na milima. Milango, ambayo ilifungwa jua lilipozama, ilifikiwa kwa njia zenye mwinuko mkali na miamba, na msafiri aliyesafiri kurudi nyumbani mwisho wa siku mara nyingi alilazimika kukaza mwendo akiwa na hamu ya kuharakisha kupanda mwinuko mgumu ili kuufikia mlango kabla giza halijaanza kuingia. Mwenye kuchelewa alifungiwa nje. Ile njia nyembamba, iendayo juu nyumbani kwenye pumziko, ilimpatia Yesu mfano wenye nguvu wa njia ya Kikristo. “Njia hii niliyoiweka mbele yenu,” alisema, “ni nyembamba. Ni vigumu kuingia kupitia mlango huu; maana usia huu wa kuwatendea wengine mema huwafungia nje wote wenye kiburi na wenye kupenda mambo yawapendezayo wao tu. Ni kweli iko njia pana; lakini mwisho wake ni maangamizi. Endapo wewe utapanda njia ile ya maisha ya kiroho, basi yakupasa kupanda daima; kwa maana ni njia inayopanda juu. Yakupasa kwenda pamoja na wachache; kwa maana watu wengi sana watachagua kwenda katika njia ile ya mtelemko.

Katika njia ile iendayo mautini waweza kwenda wanadamu wote, pamoja na tabia zao za kupenda anasa za dunia, kujipenda binafsi, majivuno yao, na ufisadi wao wote. Ina nafasi inayoruhusu maoni na mafundisho ya dini ya kila mtu; nafasi ipo kwa kila mtu kufuata tamaa zake mwenyewe, na kufanya yote ambayo mapenzi yake yanamwamuru kufanya. Ili kuifuata njia iendayo mautini, hakuna haja ya kuitafuta njia hiyo; kwani mlango wake ni mpana, na njia ni pana, na kwa kawaida miguu hugeuka na kwenda katika njia ile ambayo mwisho wake ni mauti.

Lakini njia ile iendayo uzimani imesonga, na mlango wake ni mwembamba. Ukiing’ang’ania sana dhambi yo yote inayokuzinga, utaona kuwa njia hiyo ni nyembamba hata huwezi kuingia. Ikiwa unataka kuifuata njia ya Bwana, huna

budi kuacha njia zako mwenyewe, mapenzi yako, mazoea na matendo yako yote

mabaya. Yeye anayetaka kumtumikia Kristo hawezi kuyafuata mawaidha ya kidunia wala kutimiza kipimo cha kidunia. Njia iendayo mbinguni ni nyembamba hata hapana nafasi kwa wenye vyeo na matajiri kwenda humo kwa fahari, ni nyembamba mno hata kwa wale wanaocheza mchezo wa kujitakia makuu wenyewe, mwinuko wake ni mkali mno na unaparuza hata wale wapendao anasa wanashindwa kupanda. Taabu, uvumilivu, kujinyima, shutuma, umaskini, mapingamizi ya wenye dhambi dhidi ya nafsi yake—haya yote yalikuwa fungu lake Kristo, pia yapasa kuwa fungu letu, kama tunataka kuingia Paradiso ya Mungu.

Hata hivyo usidhani kwamba njia ipandayo juu ndiyo ngumu na njia ile ya mtelemko ni rahisi. Katika njia yote iendayo mautini kuna maumivu na adhabu, kuna huzuni na kukata tamaa kwa kutopata yaliyotazamiwa, kuna maonyo yanayokataza kuendelea katika njia hiyo. Kwa upendo wake Mungu ameviweka vizuizi ili iwe vigumu kwa wale wasiojali na wakaidi kujiangamiza wenyewe. Ni kweli kwamba njia ya Shetani inaonekana kuwa ni ya kuvutia, lakini huo ni udanganyifu mtupu; katika njia ya maovu kuna majuto makali na mashaka yanayowala. Pengine tunaweza kufikiri kwamba ni vizuri kuiga kiburi na kutaka makuu ya dunia hii; lakini mwisho wake ni maumivu na huzuni tu. Mipango yetu wenyewe inaweza kutupa matarajio yanayotutia hamasa na kutupa matumaini ya kupata raha, lakini tutagundua kwamba furaha yetu ina uharibifu, na maisha yetu yametiwa uchungu kwa matumaini yetu yaliyojengwa juu ya nafsi zetu wenyewe. Katika njia ile ya mtelemko mlango wake unaweza kung'aa kwa maua yaliyo pale, lakini miiba imo katika njia hiyo. Nuru ya matumaini inayoangaza mlangoni hufifia na kuingia katika giza la kukata tamaa, na watu wale wanaoifuata njia ile hushuka chini kwenye vivuli vya usiku usio na mwisho.

"Njia ya haini huparuza," lakini njia za mwenye hekima "ni njia za kupendeza sana, na mapito yake yote ni amani." Mithali 13:15; 3:17. Kila tendo la kumtii Kristo, kila tendo la kujinyima kwa ajili yake, kila taabu unayoistahimili, kila ushindi unaojipatia dhidi ya majaribu ni hatua ya kusonga mbele kwenye utukufu wa ushindi ule wa mwisho. Tukimkubali Kristo awe kiongozi wetu, atatuongoza salama. Hata mwenye dhambi sana si lazima akose njia. Kila aitafutaye njia hiyo kwa kutetemeka, si lazima akose kwenda katika nuru ile safi na takatifu. Ingawa njia ni nyembamba sana, tena ni takatifu sana hata dhambi haziwezi kuvumiliwa humo, hata hivyo, njia imepatikana kwa ajili ya wote, wala hakuna mtu mwenye mashaka, atetemekaye awezaye kusema hivi, "Mungu hanijali mimi hata kidogo."

Njia hii inaweza kuparuza, na mwinuko wake kuwa mkali; huenda pakawa na mitego upande wa kuume na wa kushoto; pengine itatupasa kuvumilia taabu katika safari yetu; kama tumechoka na kuwa na hamu ya kupumzika, pengine

itatubidi kujikokota kwa shida kwenda mbele; kama tunazimia, huenda itatubidi

kupigana tu vita; tunapovunjwa moyo, itatub idi kuendelea kutumaini; lakini tukiwa na Kristo kama kiongozi wetu, hatimaye hatutashindwa kufika kwenye bandari ile tunayoitamani. Kristo mwenyewe amepita katika njia hiyo inayoparuza kabla yetu na kuisawazisha njia hiyo kwa ajili ya nyayo zetu.

Na katika njia hiyo yote kupanda miinuko mikali inayokwenda kwenye uzima wa milele ziko chemchemi za furaha kuwaburudisha hao waliochoka. Wale waendao katika njia za hekima, hata wakiwa katika dhiki, watafurahi mno, kwa kuwa yule ambaye mioyo yao inampenda anatembea, bila kuonekana kwa macho, kando yao. Kila hatua wanayopanda kwenda juu wanatambua kwa wazi zaidi mguso wa mkono wake; kila hatua wanayokwenda nuru ya utukufu kutoka kwa yule Asiyeonekana kwa macho inazidi kumulika katika njia yao; na nyimbo zao za sifa, huzidi kuimbwa kwa sauti ya juu zaidi, hupanda juu kuungana na nyimbo za malaika walio mbele ya kiti kile cha enzi. “Njia ya wenye haki ni kama nuru ing’aayo, ikizidi kung’aa hata mchana mkamilifu.” Mithali 4:18.

“Jitahidini Kuingia Katika Mlango Ulio Mwembamba.”
Luka 13:24.

Msafiri aliyechelewa, akiharakisha kulifikia lango la mji kabla ya jua kuchwa, hakuweza kugeuka upande kukiangalia kitu cho chote kipendezacho kando ya ile njia. Akili zake zote zilielekezwa kwenye kusudi moja tu la kuingia ndani ya lango lile. Kusudi lenye mkazo uo huo, Yesu alisema, linatakiwa katika maisha ya Kikristo. Asema, Nimekufunulia uzuri wa tabia, ambao ndio uzuri halisi wa utukufu wa ufalme wangu. Huo haukupi ahadi yo yote ya kushiriki enzi ya duniani; hata hivyo unastahili kuutamani sana na kutumia juhudi yako yote kuupata. Sikuiti ufanye vita kwa ajili ya utawala wa dola kuu ya dunia, lakini usifikiri kwamba hakuna vita inayopaswa kupiganwa, wala ushindi unaopaswa kupatikana. Nakuagiza ujitahidi, uteseke, ili upate kuingia katika ufalme wangu wa kiroho.

Maisha ya Kikristo ni pambano na kusonga mbele. Lakini ushindi unaopaswa kupatikana haupatikani kwa uwezo wa kibinadamu. Uwanja wa mapambano ni moyoni. Vita vinavyotupasa kupigana—yaani, vita vilivyo vikali mno kuzidi vyote vilivyopata kupiganwa na mwanadamu—ni vile vya kujitoa nafsi zetu kufanya mapenzi ya Mungu, yaani, kuutoa moyo wetu utawaliwe na pendo lake. Utu ule wa kale, uliozaliwa kwa damu na kwa mapenzi ya mwili, hauwezi kuingia katika ufalme wa Mungu. Mielekeo yetu tuliyozaliwa nayo, na mazoea ya zamani, sharti yaachwe.

Yeye akusudiaye kuingia ufalme wa kiroho atagundua kwamba nguvu na tamaa

zote za utu wa kale usioongoka, zikisaidiwa na nguvu za ufalme wa giza,

zinapingana naye. Kujipenda nafsi na kiburi vitashindana na kitu cho chote kitakachovidhihirisha hivyo kuwa ni dhambi. Sisi, kwa uwezo wetu wenyewe, hatuwezi kuzishinda tamaa mbaya na mazoea yanayojitahidi kuitawala mioyo yetu. Hatuwezi kumshinda yule adui mwenye nguvu anayetushika utumwani mwake. Mungu peke yake ndiye awezaye kutupatia ushindi. Yeye ataka sisi tutawale nafsi zetu, mapenzi yetu na njia zetu. Lakini yeye hawezi kutenda kazi ndani yetu bila ya sisi kukubali na kushirikiana naye. Roho wa Mungu hufanya kazi yake kupitia uwezo na nguvu walizopewa wanadamu. Nguvu zetu zinatakiwa zishirikiane na Mungu.

Ushindi haupatikani bila ya kuwa na maombi mengi ya dhati, na kujidhili kila hatua tunayokwenda. Nia zetu hazitakiwi kulazimishwa kushirikiana na uwezo wa Mungu, ila inatupasa kwa hiari yetu kumpa Mungu nia zetu. Kama ingewezekana kushinikiza juu yako mvuto wa Roho wa Mungu kwa nguvu inayozidi mara mia, isingeweza kukufanya wewe kuwa Mkristo, yaani, raia anayefaa kwenda mbinguni. Ngome ya Shetani isingeweza kuvunjwa. Nia zetu sharti ziwekwe upande wa mapenzi ya Mungu. Wewe, kwa nguvu zako mwenyewe, huwezi kuyafanya makusudi yako na tamaa zako na mwelekeo wako kutii mapenzi ya Mungu; lakini kama "unakubali kufanywa utake," basi, Mungu ataikamilisha kazi hiyo kwa niaba yako, hata "kuangusha mawazo na kila kitu kilichoinuka, kijiinuacho juu ya elimu ya Mungu; na tukiteka nyara kila fikara ipate kumtii Kristo." 2 Wakorintho 10:5. Ndipo tutawezeshwa kuutimiza wokovu wetu wenyewe "kwa kuogopa na kutetemeka. Kwa maana ndiye Mungu atendaye kazi ndani yetu, kutaka kwenu na kutenda kwenu, kwa kulitimiza kusudi lake jema." Wafilipi 2:12,13.

Lakini wengi wanaovutwa na uzuri wa Kristo na utukufu wa mbinguni, huyakataa masharti ambayo kwayo tu mambo hayo yanaweza kuwa yao. Katika njia pana kuna watu wengi ambao hawaridhishwi kabisa na njia ile wanayokwenda. Wanatamani kutoka katika utumwa wa dhambi, na kwa nguvu zao wenyewe wanajaribu kushindana na mazoea yao mabaya. Wanaitazama njia ile nyembamba na mlango wake mwembamba; lakini anasa zao binafsi, kuipenda dunia, kiburi, kutaka makuu yasiyopatana na utakatifu, haya yote huwa kipingamizi kati yao na Mwokozi. Kuyaacha mapenzi yao, na kutengana na mambo yao wanayoyapenda waliyoyachagua au wanayoyatafuta, kunataka kujinyima ambako kunawafanya wasitesite na kujikwaa na kurudi nyuma walikotoka. "Wengi watataka kuingia, wasiweze." Luka 13:24. Wanataka lililo jema, wanajitahidi kwa kiasi fulani ili walipate; lakini hawalichagui; hawana nia thabiti ya kulipata kwa kupata hasara ya mambo yote.

Tumaini pekee tulilo nalo kama tutashinda ni kuunganisha mapenzi yetu na

mapenzi ya Mungu na kufanya kazi tukishirikiana naye, saa kwa saa na siku kwa

siku. Hatuwezi kubaki na nafsi yetu na bado tukaweza kuingia ufalme wa Mungu. Kama tutaufikia utakatifu, itakuwa ni kwa njia ya kuikana kabisa nafsi yetu na kupokea nia iliyokuwamo ndani ya Kristo. Majivuno na kujiona kuwa sisi wenyewe tunafaa ni lazima visulibishwe. Je, tuko tayari kulipa gharama tunayotakiwa kulipa? Je, tunataka mapenzi yetu yapatane na mapenzi ya Mungu? Mpaka hapo tutakapotaka, neema ya Mungu inayotubadilisha tabia haiwezi kuonekana juu yetu.

Vita vile ambavyo hatuna budi kupigana ni "vita vile vizuri vya imani." 1 Timotheo 6:12. Mtume Paulo alisema, "Mimi najitaabisha kwa neno lilo hilo, nikijitahidi kwa kadiri ya kutenda kazi kwake atendaye kazi ndani yangu kwa nguvu." Wakolosai 1:29.

Yakobo alipokabiliwa na jambo kuu katika maisha yake, alijitenga kando kuomba. Alikuwa na kusudi moja kuu—yaani, kutafuta kubadilishwa tabia yake. Lakini alipokuwa akimsihi Mungu, mtu fulani, ambaye alimdhania kuwa ni adui, aliweka mkono wake juu yake, na Yakobo akashindana naye usiku kucha kujiponya roho yake.

Lakini kusudi la moyo wake lilikuwa halijabadilika kutokana na hatari ile ya kupoteza maisha yake. Nguvu zake zikiwa karibu zimekwisha, Malaika alitumia nguvu zake za Uungu, na alipomgusa, Yakobo akamtambua Yeye aliyekuwa akipigana naye. Akiwa ameumizwa na kudhoofika, akaanguka kifuani pa Mwokozi, akamsihi ambariki. Hakukubali kuondolewa wala kuacha kuomba, kisha Kristo akatimiza haja ya mtu yule aliyedhoofika, mwenye toba, kulingana na ahadi yake hii, "Azishike nguvu zangu, afanye amani nami; naam, afanye amani nami." Isaya 27:5. Yakobo aliomba kwa moyo thabiti, "Sikuachi, usiponibariki." Mwanzo 32:26. Moyo ule thabiti ulivuviwa na Yeye aliyeshindana na mzee yule. Yeye ndiye aliyemwezesha kushinda, na kulibadilisha jina lake kutoka Yakobo kuwa Israeli, akisema, "Umeshindana na Mungu, na watu, nawe umeshinda." Mwanzo 32:28. Ule mbaraka ambao Yakobo aliushindania bure kwa nguvu zake mwenyewe, aliupata kwa njia ya kujitoa mwenyewe na kwa imani yake thabiti. "Huku ndiko kushinda kuushindako ulimwengu, hiyo imani yetu." 1 Yohana 5:4.

"Jihadharini na Mana bii wa Uongo." Mathayo 7:15.

Watatokea waalimu wa uongo watakaojaribu kuwavuta mtoke katika njia nyembamba na mlango mwembamba. Jihadharini nao; ingawa wamejificha kwa kuvaa mavazi ya kondoo, ndani ni mbwa-mwitu wakali. Yesu anatoa kipimo ambacho kwacho waalimu hao wa uongo wanaweza kubainishwa na wale wa kweli. "Mtawatambua kwa matunda yao," asema. "Je, watu huchuma zabibu

katika miiba, au tini katika mibaruti?”

Hatuambiwi tuwapambanue kwa maneno yao mazuri na kwa vile wanavyojidai kuwa ni watu wema. Hawana budi kupimwa kwa neno la Mungu. “Waende kwa sheria na ushuhuda; ikiwa hawasemi sawasawa na neno hili, bila shaka kwa hao hapana asubuhi,” (yaani, hawana nuru ya Mungu ndani yao). “Mwanangu, acha kusikia mafundisho ukitaka tu kuyaasi maneno ya maarifa.” Isaya 8:20; Mithali 19:27. Waalimu hawa huleta ujumbe wa namna gani? Je, unakuongoza kumheshimu Mungu na kumcha? Je, unakufanya udhihirishe upendo wako kwake kwa kuzitii amri zake? Wanadamu wasipouona uzito wa sheria hiyo ya maadili; kama wanazidharau amri zake; kama wakivunja hata moja tu iliyo ndogo sana katika amri zake, na kuwafundisha watu hivyo, hawatapewa heshima yo yote kule mbinguni. Twaweza kujua kwamba madai yao hayana msingi. Wanafanya kazi ile ile iliyoanzishwa na yule aliye mkuu wa giza, adui wa Mungu.

Si wote wanaokiri kwamba wanamjua Mungu na kujivika alama yake ambao ni watu wake Kristo. Yesu alisema, Wengi ambao wametoa mafundisho kwa jina langu, mwishowe wataonekana wamepunguka. “Wengi wataniambia siku ile, Bwana, Bwana, hatukufanya unabii kwa jina lako, na kwa jina lako kutoa pepo, na kwa jina lako kufanya miujiza mingi? Ndipo nitawaambia dhahiri, Sikuwajua ninyi kamwe; ondokeni kwangu, ninyi mtendao maovu.”

Wako watu wanaosadiki kwamba wao ni wenye haki, hali wakiwa ni wakosaji. Wakidai kuwa Kristo ni Bwana wao, na kutangaza wazi kuwa wanafanya kazi zilizo kubwa kwa jina lake, na huku wakiwa wanatenda maovu. “Kwa vinywa vyao hujifanya kuwa wenye upendo mwingi, lakini mioyo yao inatafuta faida yao.” Kwao mwenye kulitangaza neno la Mungu ni “kama wimbo mzuri sana wa mtu mwenye sauti ipendezayo, awezaye kupiga kinanda vizuri; maana, wasikia maneno yake, lakini hawayatendi.” Ezekieli 33:31,32.

Kujidai tu kuwa mfuasi wa Kristo hakufai kitu. Imani kwa Kristo inayomwokoa mtu, si kama inavyoelezwa na wengi. Wao husema, “Amini, amini tu, wala huna haja ya kuishika sheria.” Lakini imani isiyotuongoza kuzitii amri za Mungu, siyo imani, ila ni ufidhuli. Mtume Yohana asema, “Yeye asemaye, Nimemjua, wala hazishiki amri zake, ni mwongo, wala kweli haimo ndani yake.” 1 Yohana 2:4. Asiwepo mtu anayefikiri kwamba maongozi ya Mungu ya pekee wanayopewa na miujiza waitendayo huthibitisha uhalali wa kazi yao wanayofanya au mawazo yao wanayoyatetea. Watu wakilidharau neno la Mungu, na kufanya mawazo yao, hisia zao, na ibada yao kuwa ni bora kuliko kanuni ya Mungu, twaweza kujua kwamba nuru haimo ndani yao.

Utii ndicho kipimo cha ufuasi. Ni kuzishika amri zake kunakothibitisha ukweli wa madai yetu kuwa tunao upendo kwake. Mafund isho ya dini tunayoyapokea kama

yanaiua dhambi moyoni, yanaitakasa roho na uchafu, yanazaa matunda ya

utakatifu, basi twaweza kujua kwamba mafundisho hayo ni kweli ya Mungu. Kama ukarimu, upole, upendo, na huruma huonekana katika maisha yetu; kama furaha ya kutenda haki imo mioyoni mwetu; tukimtukuza Kristo, wala siyo nafsi zetu wenyewe, hapo twaweza kujua kwamba imani yetu ni imani ya kweli. "Na hivi twajua ya kuwa tumemjua, ikiwa tunashika amri zake." 1 Yohana 2:3.
"Isianguke; Kwa Maana Misingi Ya ke Imewekwa Juu ya Mwamba." Mathayo 7:25.

Watu walikuwa wameguswa sana mioyoni mwao kwa maneno ya Kristo. Walivutwa na uzuri wa kanuni za mbinguni; na maonyo ya Kristo yalikuwa kwao kama sauti ya Mungu achunguzaye moyo. Maneno yake yalikuwa yameligonga shina halisi la mawazo yao na kauli zao za zamani; kuyatii mafundisho yake kungehitaji badiliko katika mazoea yao yote ya kufikiri na kutenda. Hilo lingewafanya wagongane na waalimu wao wa dini; maana hilo lingehusisha kuupindua mfumo mzima ambao kwa vizazi vingi waalimu wao walikuwa wakiulea. Kwa hiyo, ingawa mioyo ya watu wale ilivutwa kwa maneno yake Yesu, ni wachache tu ndio walikuwa tayari kuyapokea na kuongozwa nayo katika maisha yao.

Yesu alimaliza fundisho lake mlimani kwa kutumia mfano uliowadhihirishia wazi kwa namna ya kushangaza sana umuhimu wa kuyaweka katika matendo maneno aliyokuwa ameyasema. Miongoni mwa wale makutano waliomsonga Mwokozi walikuwamo wengi ambao wamekaa karibu na Bahari ya Galilaya maisha yao yote. Walipokuwa wameketi pale mlimani, na kuyasikia maneno ya Kristo, waliweza kuyaona mabonde na makorongo vilimopita vijito vya mlima ule kwenda baharini. Wakati wa kiangazi mara nyingi vijito hivi vilitoweka kabisa, na kuacha vikorongo vyake vilivyokauka na kuwa mavumbi tu. Lakini mvua kubwa zenye upepo wa baridi ziliponyesha kwa nguvu vilimani, mito ile ikawa na nguvu nyingi, maji mengi yenye kishindo yakaenda kasi, na wakati mwingine kufurika mabondeni, na kuvichukua vitu vyote kwa kufurika kwao kusikozuilika. Vibanda vibovu vya wakulima wale maskini vilivyojengwa katika uwanda ule wenye nyasi, vilivyoonekana kana kwamba viko mbali na hatari, vilichukuliwa na maji. Lakini juu kule vilimani palikuwa na nyumba zilizokuwa zimejengwa juu ya mwamba. Katika sehemu fulani za nchi ile palikuwa na makazi yaliyojengwa kwa mawe matupu, na mengi yake yalikuwa yamesimama imara dhidi ya tufani za miaka elfu moja. Nyumba hizi zilijengwa kwa kazi ngumu na kwa shida. Haikuwa rahisi kuzifikia, na mahali zilipojengwa hapakuwa pa kupendeza sana kama pale uwandani penye nyasi. Lakini zilijengwa juu ya msingi wa mwamba; na upepo na mafuriko na tufani vikazipiga nyumba zile, zisianguke.

Yesu alisema ya kwamba wenye kuzijenga nyumba zao katika miamba walikuwa mfano wa mtu yule anayepokea maneno yake aliyowaambia, na kuyafanya msingi

wa tabia na maisha yake. Karne nyingi kabla yake, nabii Isaya alikuwa

ameandika, “Neno la Mungu wetu litasimama milele” (Isaya 40:8); na miaka mingi baada ya mahubiri yale Mlimani, Petro akiyanukuu maneno haya ya Isaya, aliongeza kusema maneno haya, “Neno hilo ni neno lile jema lililohubiriwa kwenu” (1 Petro 1:25). Neno la Mungu ndilo kitu cha pekee kilicho thabiti ambacho ulimwengu wakijua. Hili ndilo msingi ulio imara. “Mbingu na nchi zitapita,” alisema Yesu; “lakini maneno yangu hayatapita kamwe.” Mathayo 24:35.

Kanuni kuu za sheria, ambazo ni tabia halisi ya Mungu, zimo ndani ya maneno ya Kristo aliyoyasema mlimani. Ye yote ajengaye juu yake hujenga juu ya Kristo, Mwamba wa Kale. Tunapolipokea hilo neno, tunampokea Kristo. Na ni wale tu wanaoyapokea maneno yake ndio wanaojenga juu yake. “Maana msingi mwingine hakuna mtu awezaye kuuweka, isipokuwa ni ule uliokwisha kuwekwa, yaani, Yesu Kristo.” 1 Wakorintho 3:11. “Wala hakuna wokovu katika mwingine awaye yote, kwa maana hapana jina jingine chini ya mbingu walilopewa wanadamu litupasalo sisi kuokolewa kwalo.” Matendo 4:12. Kristo, Aliye Neno, ufunuo wa Mungu—anayeidhihirisha tabia yake, sheria yake, upendo wake, maisha yake,—ndiye msingi pekee ambao juu yake tunaweza kujenga tabia yetu itakayodumu milele.

Tunajenga juu ya Kristo kwa kulitii neno lake. Si yule anayeifurahia tu haki yake, ambaye ni mwenye haki, bali ni yule atendaye haki. Utakatifu siyo kuwa na furaha nyingi moyoni; ni matokeo ya kujitoa kwa Mungu pamoja na vyote tulivyo navyo; ni kufanya mapenzi ya Baba yetu aliye mbinguni. Wana wa Israeli walipojenga kambi lao mipakani mwa Nchi ya Ahadi, haikutosha kwao kujua tu habari za Kanaani, ama kuimba nyimbo za Kanaani. Hilo tu lisingewafanya wayamiliki mashamba ya mizabibu na mizeituni mingi katika ile nchi nzuri. Wangeweza kuifanya nchi ile kuwa yao kabisa kwa kuingia na kuimiliki, kwa kutimiza masharti waliyopewa, kwa kuwa na imani hai kwa Mungu, kwa kuzitumia wenyewe ahadi zake, huku wakiyatii maagizo yake.

Dini ni kuyatenda maneno ya Kristo; si kuyatenda ili kupata upendeleo wa Mungu, bali kwa sababu, sisi tukiwa hatustahili kabisa, tumepata kipawa cha pendo lake. Kristo anampa wokovu mwanadamu, si kwa kukiri kwake kwa kinywa tu, bali kwa imani inayodhihirishwa kwa matendo ya haki. Ni kutenda, siyo kusema tu, kunakotakiwa kwa wafuasi wa Kristo. Ni kwa matendo tabia inajengwa. “Kwa kuwa wote wanaoongozwa na Roho wa Mungu, hao ndio wana wa Mungu.” Warumi 8:14. Si wale ambao wanaguswa mioyo yao na Roho, si wale ambao kwa wakati fulani tu wanajitoa na kujiweka chini ya mvuto wake, bali ni wale wanaoongozwa na Roho, hao ndio wana wa Mungu.

Je, unataka kuwa mfuasi wa Kristo, lakini hujui jinsi ya kuanza? Je, umo gizani,

na hujui namna ya kuipata nuru? Ifuate nuru ile uliyo nayo. Kaza moyo wako

kulitii neno la Mungu ulijualo. Uwezo wake, uzima wake hasa, umo ndani ya neno lake.

Unapolipokea neno hilo kwa imani, litakupa uwezo wa kulitii. Kadiri unavyoifuata nuru uliyo nayo, nd ivyo utakavyopata nuru kubwa zaidi. Unaendelea kujenga juu ya neno la Mungu, na tabia yako itajengwa kwa mfano wa tabia ya Kristo.
Kristo, aliye msingi wa kweli, ndiye jiwe lililo hai; uzima wake unatolewa kwa wote waliojengwa juu yake. "Ninyi nanyi, kama mawe yaliyo hai, mmejengwa mwe nyumba ya Roho." "Katika yeye ninyi nanyi mnajengwa pamoja kuwa maskani ya Mungu katika Roho." 1 Petro 2:5; Waefeso 2:21. Mawe yataunganishwa na msingi na kuwa kitu kimoja; maana uzima mmoja umekaa ndani ya wote. Hilo ndilo jengo lisiloweza kuangushwa na tufani yo yote, kwa maana—

"Kile kinachoshiriki uzima wa Mungu, Kikiwa naye kinastahimili yote."

Lakini kila jengo lijengwalo juu ya msingi mwingine usio wa neno la Mungu litaanguka. Mtu awaye yote, kama wale Wayahudi wa siku za Kristo, ajengaye juu ya mawazo na kauli za kibinadamu, na desturi na kawaida za ibada zilizovumbuliwa na mwanadamu, ama juu ya matendo yo yote awezayo kutenda bila kuitegemea neema ya Kristo, anajenga jengo lake la tabia juu ya mchanga unaohama-hama. Tufani kali za majaribu zitaukumba msingi huo wa mchanga, na jengo lake kubomolewa na kubakia magofu matupu katika pwani ile ya wakati. "Kwa ajili ya hayo Bwana, Mungu, asema hivi,... Nami nitafanya hukumu kuwa ndiyo kanuni, na haki kuwa ndiyo timazi; na mvua ya mawe itachukulia mbali hilo kimbilio la maneno ya uongo, na maji yatapagharikisha mahali pa kujisitiri." Isaya 28:16,17.

Lakini leo rehema inamsihi sana mwenye dhambi. "Kama mimi niishivyo, asema Bwana Mungu, sikufurahii kufa kwake mtu mwovu; bali aghairi mtu mwovu, na kuiacha njia yake mbaya, akaishi, Ghairini, ghairini, mkaache njia zenu mbaya; mbona mnataka kufa?" Ezekieli 33:11. Sauti ile inayonena leo na wale wasiotubu ndiyo sauti yake yeye ambaye kwa maumivu ya roho alilia alipouona ule mji alioupenda: "Ee Yerusalemu, Yerusalemu, uwauaye manabii na kuwapiga kwa mawe waliotumwa kwako, mara ngapi nimetaka kuwakusanya watoto wako kama vile kuku avikusanyavyo vifaranga vyake chini ya mbawa zake, wala hamkutaka. Angalieni mmeachiwa nyumba yenu!" Luka l3:34,35. Yesu alipouangalia Yerusalemu, aliona mfano wa dunia ambayo ilikuwa imeikana na kuidharau neema yake. Alikulilia wewe, ewe mwenye moyo mgumu! Hata wakati ule Yesu alipotoa machozi yake pale mlimani, Yerusalemu bado ungaliweza kutubu, na kuepukana na hukumu yake. Kwa kitambo kidogo tu yule aliyekuwa Kipawa cha

mbinguni bado alingoja kupokewa nao. Kadhalika kwako wewe, Ee moyo, Kristo

bado anasema nawe kwa sauti ya upendo: “Tazama, nasimama mlangoni, nabisha; mtu akiis ikia sauti yangu, na kuufungua mlango, nitaingia kwake, nami nitakula pamoja naye, na yeye pamoja nami.” “Tazama, wakati uliokubalika ndio sasa; tazama, siku ya wokovu ndiyo sasa.” Ufunuo 3:20; 2 Wakorintho 6:2.

Wewe uwekaye tumaini lako juu ya nafsi yako mwenyewe unajenga juu ya mchanga. Lakini hata sasa bado hujachelewa mno kuyakwepa maangamizi ambayo yamekaribia sana. Kabla tufani haijavuma, mkimbilie yeye aliye msingi ulio imara. “Bwana, Mungu, asema hivi, Tazama, naweka jiwe katika Sayuni, liwe msingi, jiwe lililojaribiwa, jiwe la pembeni lenye thamani, msingi ulio imara; yeye aaminiye hatafanya haraka.” “Niangalieni mimi, mkaokolewe, enyi ncha zote za dunia; maana mimi ni Mungu; hapana mwingine.” “Usiogope, kwa maana mimi ni pamoja nawe; usifadhaike, kwa maana mimi ni Mungu wako; nitakutia nguvu, naam, nitakusaidia, naam, nitakushika kwa mkono wa kuume wa haki yangu.” “Ninyi hamtatahayarika, wala kufadhaika, milele na milele.” Isaya 28:16; 45:22; 41:10; 45:17.

Musa L. Budodi

One-Soul Audience Ministry Kagongwa, Kahama

+255-784-825-660